**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Februari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo nimearifiwa na Serikali na nimekubali kwamba tuwatambue vijana wetu waliomaliza darasa la saba na wakafaulu vizuri kitaifa. Imekuwa ni utamaduni wetu hasa kwa ajili ya vijana ili kutoa mfano mwema kuwaenzi na kuwatambua ili kuhamasisha wengine wote waweze kufanya vizuri. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Bunge) aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni ili kuwawezesha wageni kuingia ndani ya Bunge mara baada ya maswali.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA BUNGE KURUHUSU WANAFUNZI WAALIKWA KUINGIA BUNGENI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Naomba kutumia Kanuni ya 124 kuomba ruhusa yako tutengue Kanuni ya Bunge ili kuweza kuwaruhusu vijana wetu waliofanya vizuri katika masomo yao waweze kuingia katika Bunge hili. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ya Bunge ili Kuruhusu Wanafunzi waalikwa Kuingia Bungeni ilikubaliwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja ya kutengua Kanuni ili kuwawezesha wageni kuingia Bungeni imekwishatolewa na imeungwa mkono. Nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge) kwa leo siku ya kwanza kuweza kutoa hoja katika Bunge. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 *(Mzumbe University Annual Report and Accounts for the year ended 30th June, 2005)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 27

### Haki za Wananchi Wanaopewa Mashamba Mapya Dodoma

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kutokana na kasi ya ukuaji wa Mji wa Dodoma, Serikali imekuwa ikichukua mashamba ya wananchi na kupima viwanja vya makazi na kwa kuwa wananchi wengi wameathirika vibaya na zoezi hilo ikizingatiwa kuwa, fidia wanayopewa ni kidogo sana na kwa kuwa kilimo cha Dodoma si cha mazao ya kudumu:

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, wakulima wanaokumbwa na zoezi hilo na ambao tayari hali zao za maisha ni duni sana wanazidi kuathirika zaidi kiuchumi na kimaisha?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia wananchi kama hao kwa kuwapatia nyenzo na hali na mali za kuhamia kwenye mashamba hayo mapya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, naomba kutoa maelezo machache yafuatayo:-

Mpango wa kuwezesha ukuaji wa Mji Mkuu, ulitangazwa kwa tangazo la Serikali Na. 8 la tarehe 25 Novemba, 1979 na kutolewa katika Gazeti la Serikali tarehe 25 Januari, 1980. Maeneo yaliyokuwa yamehusika ni Tambukareli, Kikuyu, Chamwino na Chinangali, ambako wakazi walihakikiwa na kulipwa fidia.

Wananchi waliruhusiwa kuendelea kutumia maeneo ya akiba kwa kilimo cha mazao ya muda. Kuhusu uendelezaji mwingine ulioonyesha utata katika suala la upanuzi wa mji kwa kupima viwanja, kama vile nyumba, miti, makaburi na kadhalika. Utaratibu wa kulipa fidia ulitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo mapya ya Mji Mkuu katika Vijiji vya Ntyuka, Nzuguni, Ngong'ona, Iyumbu na Mapinduzi, vinavyopitiwa na eneo la Chuo Kikuu kipya cha Dodoma, utwaaji wake utazingatia sheria mpya ya ardhi Na. 4 ya 1999 inayotumika hivi sasa. Thamani ya mali inajumuisha majengo, ujenzi na uendeshaji wowote uliofanyika juu na chini ya ardhi, mashamba, mazao, miti na uoto mwingine wa kupandwa kwa ajili ya vivuli, matunda au mapambo.

Thamani ya ardhi itahusu ukubwa wa eneo lililomilikiwa kwa kuzingatia thamani ya soko ya ardhi. Ukokotoaji wa gharama za usumbufu kwa kulazimika kuhama, utazingatia utaratibu/fomula iliyoelekezwa katika kanuni za sheria. Gharama nyingine ni kuhamisha vifaa visivyozidi tani kumi na mbili kwa umbali usiozidi kilomita 20, pango la miezi 36 kumwezesha mwananchi kutayarisha na kukamilisha ujenzi katika eneo jipya na kuhamia na kama ana biashara kulipa upotevu wa faida *(loss of profit)* kwa biashara yake kukatizwa kutokana na kuhamia eneo jingine.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya ardhi na ile ya utwaaji, mlipwaji fidia ndiye mwenye jukumu la kujitafutia nyenzo na makazi yake baada ya kulipwa thamani ya mali, usumbufu, thamani ya ardhi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yetu kuwa wananchi wanaokumbwa na utwaaji huo watatumia viwango vya fidia vilivyoongezeka kwa hekima na busara ili kujitengenezea makazi mengine bora ya kuishi bila kuathiri hali zao za uchumi na maisha. Maeneo ya Dodoma yaliyo wazi na yanafaa kwa makazi, kilimo na ufugaji kwa wananchi wengi ni mengi na siyo tatizo kuyapata.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge hili Tukufu, kwamba jitihada za makusudi zitaendelea kufanywa ili kuona kuwa wananchi hawaathiriki na utwaaji huu wa maeneo katika ukuaji na upanuzi wa Mji Mkuu.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini ningependa anipatie jibu kuhusu fidia kwa wale wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo ya Kata ya Nzuguni Kata ya Miuji na Kata ya Makole ambao wamekumbwa na tatizo hili. Wananchi hawa mashamba yao yalichukuliwa kitambo kidogo na mpaka sasa hivi baadhi yao bado hawajapata fidia ambayo wanastahili.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hiyo fidia inalipwa kwa wakati muafaka? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba wakazi wa maeneo hayo baada ya tathimini kufanywa ya thamani ya ardhi na mali

zilizokuwepo pale, walilipwa fidia. Hivyo kama kuna mtu ambaye kwa wakati ule alistahili kulipwa hajalipwa basi afanye taratibu afuatilie ili haki yake iweze kulipwa. (*Makofi*)

Na. 28

**Ukosefu wa Hospitali ya Wilaya – Morogoro Vijijini**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Morogoro Vijijini ni kubwa sana na kwa kuwa Wilaya hiyo haina Hospitali ya Wilaya, hivyo watu wake wote pamoja na wa Manispaa ya Morogoro kutumia Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kama Hospitali ya Wilaya pia:-

Je, ni lini Wilaya ya Morogoro Vijijini itapewa Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Morogoro Vijijini haina Hospitali ya Wilaya na hivyo wananchi wake wanatumia Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kama Hospitali ya Wilaya kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilishaona tatizo hilo. Hospitali ya Mkoa haiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi wanaostahili kupata huduma hizo. Hii ikiwa ni pamoja na umbali wa kutoka Kata kuja kupata huduma hiyo katika Hospitali ya Mkoa. Pia inasababisha mlundikano wa wagonjwa ambao wangepata huduma hizo kwa ukaribu na hivyo kuifanya Hospitali ya Mkoa kuchukua wagonjwa wa rufaa kutoka Hospitali za Wilaya tu.

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha Halmashauri cha Kamati ya Elimu, Afya na Maji, cha tarehe 14/09/2004 kilipitisha Azimio la kujengwa Hospitali ya Wilaya katika Tarafa ya Mvuha. Sababu kubwa ya kuchagua eneo hilo ni kutokana na urahisi wa kufikika toka maeneo mengine ya Wilaya. Halmashauri imetenga eneo la hekta 15 kwa ajili ya ujenzi huo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Morogoro Vijijini, itaanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kukamilisha suala la kibali, mchoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Morogoro Vijijini mpaka sasa ina Zahanati 71 na Vituo vya Afya 6 kati ya zahanati hizo 71, zahanati 56 ni za zamani na 15 ni mpya. Idadi ya wakazi wa Wilaya hiyo, ni jumla ya 263,920 kwa mujibu wa sensa ya Kitaifa ya idadi ya watu ya mwaka 2002. Aidha, kulingana na Sera ya Afya, zahanati inatakiwa kuhudumia wagonjwa 8,000 hadi 10,000 kwa mwaka na kituo cha afya kinatakiwa kuhudumia wagonjwa 50,000 kwa mwaka. Hivyo kwa vituo vya afya 6 na zahanati 71

zilizopo zinaweza kuhudumia idadi ya wakazi waliopo.Tunawaomba wananchi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini waendelee kutumia huduma zilizopo karibu wakati huu wakati taratibu zingine zinaendelea za ujenzi wa Hospitali hiyo ya Wilaya. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba vituo vya kutolea huduma za afya vinakuwa na watumishi na madawa ya kutosha.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni Diwani katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini na kwa kuwa ninajua kinachoendelea hapo kuhusu Hospitali ya Wilaya naomba nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba majibu aliyoyapata si ya kweli. Hakuna vituo vya afya 6 Morogoro Vijijini, viko vituo vya afya viwili tu Morogoro Vijijini kimoja kiko Lutumi kingine kipo Ngerengere. Sasa hivyo vingine sita havipo. (*Makofi*)

Kwa kuwa Morogoro Mjini hospitali ile ninyi Wabunge ni mashahidi imekuwa ni hospitali ya taifa sasa badala kuwa ya Mkoa watu kutoka Kisaki ambako ni km 194 mpaka Morogoro Mjini na wale wa Matombo na Mtombozi ambao nao kama km 70. *(Makofi/Vicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Je, ni lini Serikali kwa uhakika kabisa tutajengewa Hospitali ya Wilaya tunapata tabu sana na akina mama wanazalia kwenye nyumba na barabarani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Vijijini kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama nilivyokiri kwamba Wilaya ya Morogoro Vijijini, haina Hospitali ya Wilaya na kama nilivyokiri kwamba kuna mlundikano mkubwa wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ni Diwani, katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini, namwomba katika vikao vyao vya Halmashauri walipe kipaumbele suala la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Morogoro Vijijini. Hii itasaidia kwa Serikali, kuipa kipaumbele kwa sababu wenyewe wananchi wanachukulia hilo suala wanalipa kipaumbele. Kwa hiyo, hata Serikali wenyewe wakianza ina maana kwamba itawasaidia kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge ajitahidi, wafuate *process* ili waweze kujenga hiyo hospitali. Mimi nina uhakika kwamba wenzetu wa Bukombe wafanya hivyo wamejenga Hospitali ya Wilaya kwa nguvu zao na kuipa kipaumbele hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, waige mfano wa Bukombe na Wilaya nyingine ambazo zimejenga hospitali kwa nguvu zao. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika swali la msingi la Mheshimiwa Mwenegoha linafanana kabisa na tatizo lililoko katika Wilaya ya Moshi Vijijini, ambako wananchi wake wanatumia Hospitali ya Mkoa yaani ya Mawenzi kimsingi ni kwamba Wilaya ya Moshi Vijijini haina Hospitali ya Wilaya. Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Wilaya Moshi Vijijini Hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Naona hili lingestahili kuja kwa kipekee kama swali jipya. Nilimwona Mheshimiwa Mhonga Luhwanya. Basi amegaili.

Na. 29

**Vituo vya Kazi kwa Mahakimu**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo Mahakimu ambao wana vituo zaidi ya kimoja vya kazi hivyo kusababisha mrundikano wa kesi au ucheleweshaji wa kesi.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hili?

(b) Je, Serikali ina mpango gani na kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chilolo, Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu, kuwa kuna idadi kubwa ya mahakama kuliko zaidi ya Mahakimu. Kwa mfano kuna Mahakama za Mwanzo 1105 nchini kote wakati kuna Mahakimu wa Mahakama hizo 698 tu. Hali hii ndiyo inayolazimisha mahakimu kutoa huduma kwa Mahakama zaidi ya moja kwa utaratibu wa kutembelea Mahakama hizi zisizo na Mahakimu wa kudumu. Ili kupunguza tatizo hilo, Serikali inaendelea kuajiri Mahakimu kwa mfano kati ya mwaka 2003 – 2005, jumla ya Mahakimu wa Mahakama wa Mwanzo 96 na Mahakimu Wakazi 68 waliajiriwa. Katika mwaka 2006/2007 Mahakama ya Tanzania inatarajia kuajiri Mahakimu Wakazi 75 na wa Mahakama za Mwanzo 100. Ili kupata Mahakimu wengi wa Mahakama za Mwanzo, Serikali inaendelea na jitihada za kukipanua Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto ili kiweze kupokea na kutoa Mahakimu wengi zaidi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, wanakabiliwa na matatizo mengi sambamba na tatizo la kuwa Mahakama nyingi za kuendesha na kwa kuwa katika matatizo yao mengi ni pamoja na majengo mabovu wanayofanyia kazi ama mabanda. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna kila sababu ya kuanzisha mkakati wa kitaifa wa kuboresha majengo ya mahakama za mwanzo wakishirikiana na wananchi kama walivyofanya kwenye Mpango wa MMEM na MMES ili Mahakama za Mwanzo ziweze kupata hadhi ya Serikali kama ilivyo taasisi zingine za Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Idara ya Mahakama inakabiliwa na hili tatizo la kuwa na majengo mabovu kwa Mahakama za Mwanzo. Tunapoyatembelea kwa kweli hata sisi wenyewe tunaona hayaridhishi. Lakini Serikali katika mradi wake wa *Legal Sector Reform Program* ina

mkakati kabambe wa kujenga Mahakama nyingi za Mwanzo mpya. Lakini hata hivyo tungependa kuwaomba viongozi kuwahamasisha wananchi wajenge Mahakama kwa utaratibu wa kujitolea ili ku-*supplement* hizi *efforts* za Serikali katika kujenga hizi Mahakama. Katika kata ya Mbondo Wilayani Nachingwea wananchi pale walijenga wenyewe Mahakama yao na Serikali imewapelekea Hakimu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Dr. Zainab Gama, kabla hujauliza swali la nyongeza napenda kukupongeza kwa kuweza kwenda Hija na kurudi salama. (*Makofi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipongeza na kunipa nafasi. Bahati mbaya tangu *system* hii imeanza ndiyo leo mara yangu ya kwanza kuinuka kuchangia. Kwa hiyo, ndiyo maana nimechelewa. Kwa kuwa katika Bunge hili ilithibitika kutokana na upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, pia utoaji wa haki ulikuwa unaathirika kutokana na mahakimu wengi walikuwa na vyeti badala ya *diploma* na mkasema mtaondoa wa vyeti na kuweka wa *diploma*. Je, baada ya kutamka hilo ni wangapi wameondolewa wa vyeti na wangapi wa *diploma* wamewekwa? Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona swali hilo linahitaji takwimu pengine tutafaidika likiulizwa mahususi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Iramba ina kata 26 na kwa kuwa Wilaya ya Iramba ina idadi ya watu watu wasiopungua 450,000 lakini tuna Mahakama moja tu ya Wilaya. Mbali na mahakama hiyo moja ambayo haina jengo mahali ambapo Hakimu amekuwa akifanya shughuli zake kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Lakini tatizo lililopo mlundikano wa kesi. Tunaye Hakimu mmoja tu wa Wilaya ambaye anakaa Singida. Je, Wizara inasemaje itatupatia Hakimu na kutujengea jengo kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, tatizo la mlundikano wa kesi katika idara ya mahakama sasa hivi ni la nchi nzima na Serikali inachukua jitihada nyingi kubwa kujaribu kupunguza mlundikano huu kwa ku-*train* Mahakimu wengi ili tuweze kuwagawa katika Wilaya mbalimbali. Nashindwa kutoa ahadi ya dhati kabisa kwamba tutapeleka Hakimu Wilaya ya Iramba, kesho au kesho kutwa. Lakini nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, kwamba pindi tutakapo kamilisha vijana wetu pale Lushoto, basi tutawapatia hakimu ili aweze kupunguza mlundikano uliopo wa kesi huko Iramba.

Na. 30

**Ujambazi wa Kutumia Silaha**

**MHE. VUAI A. KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa ujambazi wa kutumia silaha umeshamiri katika Kisiwa cha Zanzibar na Tanzania Bara kwa Ujumla:-

(a) Je, Serikali, ina mikakati gani ya kuwa na vifaa vya kukabiliana na majambazi kama usafiri wa magari, zana za kisasa na askari imara?

(b) Je, kuna magari mangapi Zanzibar, ikizingatiwa kuwa majambazi hao mara nyingi hutumia gari aina ya *Suzuki Escudo* wakati wakifanya uhalifu huo?

(c) Je, Serikali imeandaa magari gani yenye uwezo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Vuai A. Khamis Mbunge wa Magogoni swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bila ya kutaja idadi ya nyenzo mbalimbali, Serikali inavyo vifaa vya aina kadhaa vya kukabiliana na uhalifu nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na magari, pikipiki, vifaa vya mawasiliano na zana nyingine za kukabiliana na uhalifu na askari imara. Aidha, mikakati mbalimbali imebuniwa na Jeshi la Polisi ikiwemo doria, misako, operesheni maalum, kuhakiki silaha, kushirikiana na vyombo vingine vya dola, polisi jamii na kadhalika. Ili kupambana na uhalifu, katika mwaka huu wa fedha Serikali kupitia Jeshi la Polisi, imetenga zaidi ya shilingi bilioni 8 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ulinzi na kila mwaka itaendelea kutenga fungu maalum katika Bajati yake kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usio pingika kwamba idadi ya magari yaliyopo hayatoshelezi mahitaji halisi, lakini viongozi wa Jeshi la Polisi, wamekuwa wabunifu kupanga doria makini ili kudhibiti uhalifu nchini na ndiyo sababu Jeshi letu limeendelea kumudu kuzuia uhalifu kwa kiwango cha kuridhisha. Naamini sote tunatambua upungufu huu wa vitendea kazi katika Jeshi letu kutokana na hali halisi ya uchumi wetu. Lakini nina imani pia mnatambua kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi katika mazingira haya. (*Makofi*)

**MHE. VUAI A. KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunao askari wazuri ambao wanaweza kupambana na majambazi na wanakamata si mara moja wala si mara mbili zaidi ya mara tatu kukamata majambazi. Kwa askari kama hao Serikali inatuambia nini? Je, tutawapa motisha gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niendelee kutoa pongezi kwa askari wanaofanya kazi nzuri ya kupambana na majambazi. *(Makofi)*

Lakini pale Wizarani kupitia Jeshi la Polisi kuna utaratibu maalum wa kutoa vyeti maalum kwa ajili ya wale ambao wanafanya kazi nzuri. Aidha, kuna utaratibu maalum unaotumika ndani ya jeshi kwa ajili ya kuwapongeza hawa wanaofanya kazi nzuri. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuunga mkono na kuliunga mkono jeshi la Polisi kwa kazi hiyo wanayoifanya. *(Makofi)*

Na. 31

**Ajali zinazosababishwa na wapanda Baiskeli**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na ongezeko la ajali za barabarani nyingi zikiwahusisha wapanda baiskeli na madreva wengine hasa nyakati za usika ambapo wapanda baiskeli huendesha baiskeli zisizo na taa za kutoa ishara za chombo hicho:-

(a) Je, Serikali haijaweka sheria za wapanda baiskeli kuwasha taa za vyombo vyao hasa nyakati za usiku ili kupunguza ajali hizo?

(b) Je, sheria inasemaje juu ya mtu aliyepakiwa kwenye baiskeli kuwa akae juu ya fremu ya baiskeli au akae kwenye kibao maalum cha nyuma?

(c) Je, hadi sasa ni ajali ngapi kubwa za vyombo vya barabarani zilizotokea na kuua watu zilizosababishwa na wapanda baiskeli na Serikali inachukua hatua gani kupungua ajali hizo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Hafidhi Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, swali lake lenye sehemu 9 (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za usalama barabarani *(traffic regulations)* kifungu na. 43 (i) kila baiskeli inatakiwa kuwa na taa inayotoa mwanga usiku. Aidha, baiskeli pia zinatakiwa kuwa na viakisi mwanga *(reflectors)* ili kuwawezesha madreva kuziona baiskeli kwa urahisi.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani namba 30 ya mwaka 1973 *(The Road* T*raffic Act, Cap. 168 R. E. 2002)* kifungu na 101 hairuhusiwi kumbeba mtu kwenye fremu ya baiskeli hata akiwa mwenza wako.

Sheria hiyo inamtaka mtu aliyebebwa kwenye baiskeli kukaa kwenye kibao maalum *(carrier)* kilicho nyuma ya baiskeli. Aidha, napenda kusisitiza kwamba anayeruhusiwa kubebwa kwenye baiskeli hiyo ni mtu mmoja tu.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2006 takwimu za ajali za baiskeli ni kama ifuatavyo:-

- Jumla ya ajali za baiskeli – 1087;

- Wapanda baiskeli waliofariki – 398; na

- Majeruhi wa ajali hizo – 1359.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza au kutokomeeza kabisa ajali hizo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Askari kuwaelimisha wapanda baiskeli kutii sheria za usalama wa barabarani.

2. Kuwatoza faini *(notification)* au kuwashtaki mahakamani wapanda baiskeli wanaobainika kukiuka sheria za usalama barabarani.

3. Kutoa elimu kwa watumiaji mbalimbali wa barabara wakiwemo wapanda baiskeli kupitia kipindi cha usalama wa raia kitolewacho katika Redio ya Taifa kila Jumapili saa 2.15 mpaka 2.30 usiku. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu kutokana na swali langu namba 31 lakini kwa ruhusa yako naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kutokana na maelezo yake na hasa alivyonukuu sheria.

Mheshimiwa Spika, kinachoonekana hivi sasa ndani ya miji yetu yote ya Tanzania uendeshaji wa baiskeli hawatumii taa hasilan. Hii ndiyo inayosababisha ajali nyingi. Je, tuseme Askari, *Traffic* wamechoka, hawaoni, hawataki kufuata sheria au ni dharau? Hilo la kwanza.

La pili, amezungumzia hapa suala la sheria inavyosema kwamba watu wasipakiwe katika fremu na wapakiwe katika kibao maalum. Ndani ya miji yetu bado utaratibu wa kupakiana kwenye fremu inaonekana ndiyo utaratibu maalum. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa wito gani kwa wananchi ili kuepusha ajali nzito za baiskeli zinazotokea nchini Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba askari wetu *traffic* bado hawajachoka, watafanya kazi na nataka nimhakikishie kwamba yale mapungufu ambayo ameyaona tutachukua jitihada za dharura ili kurekebisha mapungufu hayo ili matatizo haya ambayo yamejitokeza yaweze kupungua.

Kuhusu kubeba abiria wa baiskeli kwenye fremu, kama nilivyosema katika swali la msingi kwamba hili ni kosa, na nirudie kusema tena kwamba tutahimiza zaidi askari wetu kuhakikisha kwamba watu hawapakiwi kwenye fremu ili kuepusha ajali nyingi zinazotokea barabarani. Hili ni tatizo lakini nitapanga mkakati maalum wa kupambana na tatizo hili. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa usafiri wa baiskeli ni usafiri mkubwa unaotegemewa na wananchi wengi katika Mikoa mbali mbali na hasa vijijini na kwa kuwa wanaponunua baiskeli hakuna maelezo yoyote yanayotolewa na kwa kuwa mafunzo hayatolewi kwa hawa wanaondesha baiskeli isipokuwa inapotokea ajali ndio askari wa usalama barabarani wanapowafafanulia sheria.

Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba mafunzo yanatolewa kwa waendesha baiskeli wote na ikiwezekana wanaponunua baiskeli wale wauza baiskeli wawe na maelezo mafupi ya usalama barabarani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba mafunzo ni kitu muhimu ili wale watumiaji wa vyombo mbalimbali vya usalama barabarani waweze kuelewa. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba tunatoa elimu maalum kupitia redio kwa ajili ya kutoa taalum hiyo kwa wananchi wote ili waelewe wajibu wao na kuepuka kufanya makosa na siku zote sheria ni msumeno kwa hivyo kama umefanya makosa sheria itachukua mkondo wake.

Kutokujua sheria hakusababishii kuepuka kutenda kosa. Kwa msingi huo ningependa kutoa wito kwa wananchi wasikilize hiki kipindi cha usalama wa raia kinachotolewa kila Jumapili saa 2.15 na saa 2.30 usiku ili kuweza kujua vizuri suala za utaratibu wa usalama barabarani.

**SPIKA:** Naomba nitoe fursa maalum kwa Mheshimiwa Mbunge wa Nzega kuuliza swali la nyongeza kwa sababu Wilaya yake ndiyo ina baiskeli nyingi zaidi hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Bwana Spika, kwa kuniona. Kwa kuwa kumekuwa na taarifa za mkanganyiko wa baadhi ya Wakuu wa Polisi wa Mikoa kupiga marufuku waendesha baiskeli kusafirisha abiria kwa baiskeli maarufu kule kwetu kama daladala au ganagana. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa sababu usafiri huo unasaidia sana hasa kwa wanainchi wa vijijini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunalo tatizo hilo kiutendaji. Lakini pia kama nilivyokuwa nikitoa taarifa ya hali ya usalama nchini ipo sheria ambayo inazuia kwa wakati huu kwamba baiskeli na pikipiki siyo *public service vehicle* hiyo ndiyo sheria ilivyo mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, kwa wakati huu itabidi tuizingatie sheria hiyo mpaka hapo ambapo tutakapofanya marekebisho ya sheria hiyo. Kwa hiyo, hali imesimama hapo hapo, sheria ipo. Naomba wananchi waendelee kuzingatia sheria na kushirikiana na sisi.

Na. 32

**Tanki la Kuhifadhi maji katika Mradi wa Mwamashimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa maji toka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama utahudumia pia baadhi ya vijiji vya Tarafa ya Mwamashimba Wilayani Kwimba na kwa kuwa Vijiji vya Tarafa ya Mwamashimba vitasambaziwa maji baada ya maji hayo kufikishwa na kuhifadhiwa kwanza katika tanki la maji la mradi wa zamani wa Mwamashimba lililoko Mhalo katika Kata ya Bupamwa.

(a) Je, tanki hilo lina uwezo wa ujazo gani?

(b) Je, maji yatakayohifadhiwa katika tanki hilo la zamani yanaweza kuhudumia mifugo na binadamu waliopo kwa takwimu za sasa katika vijiji hivyo kwa kipindi gani iwapo maji yakikatika kwa kipindi kirefu katika mtandao wa kufikisha maji katika tanki hilo kutokana na hitilafu iwayo yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, lenye vipengele (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa zamani wa Mwamashimba ulijengwa kwa kutegemea vyanzo vya visima 7 vilivyochimbwa na Wizara yangu vyenye jumla ya uwezo wa kutoa maji kiasi cha meta za ujazo 720 kwa siku na ulisanifiwa ili kuhudumia vijijii 16 katika Tarafa ya Mwamashimba vyenye jula ya wakazi 44,256 na mifugo 65,000 kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2002. Vijiji hivyo ni Milyungu, Mwalujo, Nyang'honge, Ndamhi, Chibuji, Kawekamo, Mhande, Gulumwa, Sangu, Kikubiji, Mwalubungwe, Shilima, Chasalawi, Dodoma, Mhalo na Bupamwa. Mradi huo haukuweza kutoa huduma kutokana na matatizo ya uendeshaji.

Wakati tulipoanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga Wizara yangu iliamulia pia maji yapelekwe katika tanki lililopo katika kijiji cha Mhalo ili kuhudumia watu na mifugo iliyopo katika vijiji 16 vya Tarafa ya Mwamashimba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tanki la maji lilijengwa katika mradi wa zamani wa Mwamashimba lililoko Mhalo katika Kata ya Bupamwa lina uwezo wakuhifadhi maji hekta za ujazo 763. Ili liweze kutumika, litakarabatiwa kama sehemu ya utekelezaji wa mradi huu unaoendelea sasa.

Aidha, chini ya mradi unaoendelea nyumba ya mtumishi na *kiosk* kimoja cha maji kwa ajili ya kutoa huduma kitajengwa jirani na tanki hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, iwapo maji yatakatika kutokana na hitilafu yoyote na yasiweze kufika kwenye tanki hilo, maji yatakayokuwa yamehifadhiwa kwenye tanki yataweza kukidhi mahitaji ya maji kwa watu 44,256 na mifugo 65,000 yenye mahitaji ya meta za ujazo 720 kwa muda wa siku moja. Taratibu za kutoa huduma katika mradi huu ni kwa kujiendesha hivyo Serikali za Mitaa na Vijiji zitahitajika kulipia huduma hiyo kwa kutumia taratibu zitakazopangwa na wadau wote ili mradi huu uwe endelevu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tanki hili limejengwa kama miaka zaidi ya 20 iliyopita na idadi ya watu na mifugo imeongezeka. Je, Serikali ina mpango gani wa kufikiria kujenga tenki kubwa zaidi tena au kujenga tanki kama hili jingine katika Kata ya Chibuji na Mhande?

La pili, Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Naibu Waziri, gharama ya ukamilishaji wa mradi huu utahitaji vile vile uchangiaji wa wananchi.

Je, Serikali iko tayari sasa kuainisha michoro ya mradi katika vijiji husika ili wananchi waweze kujiandaa na hasa kwa sababu hivi sasa kuna *TASAF* kuna ruzuku ya maendeleo ambayo wangeweza kuitumia kuibua miradi hiyo ya maji katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza la maombi ya kuomba kujenga tenki lingine kubwa zaidi. Ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ili mradi huu uingizwe katika taratibu zingine ikiwemo ufadhili kwa kupitia miradi ya Benki ya Dunia na pia katika taratibu zingine ambazo Halmashauri huwa wanazo.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, ni kweli kabisa kwamba mradi wa Mwamashimba sasa hivi uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa sasa hivi kilichofanyika ni kwamba mradi huo, mabomba ya kipenyo cha milimita 300 yameshatandazwa kuanzia Mawile hadi kufika Kijijini kwenyewe, kwenye kijiji cha Mhale ambako tanki litajengwa na pia baada ya hapo hatua itakayofuatia itakuwa sasa kuelekeza vijiji gani michoro itakwenda na kwa taarifa tu vijiji vya Kwimba ambavyo vitahudumiwa viko 16 na katika hivyo vijiji 16 kila kijiji kitashirikiana na wataalam *Engineer* wa Halmashauri ya Wilaya katika kuelekeza wapi haswa vitakapokuwepo na baada ya hapo ndiyo sasa juhudi za kuwahamasisha wananchi zianze ili wananchi waanze kupokea mradi huo kama wao na waweze kuuchangia mapema iwezekanavyo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mradi huu wa Ziwa Victoria umeibua mambo mengi sana hasa katika miji ambayo inazunguka Ziwa Victoria kama Bunda, Geita, Muleba na sehemu zingine.

Katika maswali yetu hapa swali langu katika kipindi kilichopita walisema kwamba Geita tungeweza tukapata maji na sisi tukaenda kuwahamasisha wananchi kwamba maji yanakuja.

Je, Serikali inasemaje kuhusu hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mpango maalum wa kuwapatia maji Bunda, Geita, Misungwi, Tarime kama jinsi tulivyoahidi na miradi hii sasa hivi tuko katika maongezi na mfadhili *MCC Millenium Challenge Cor-operation* ambapo tumefikia hatua nzuri ya makubaliano ya awali na sasa hatua zingine zitafuata lakini dalili ni nzuri kwamba hawa watatusaidia na watafadhili miradi ifuatayo ikiwemo mradi wa maji Misungwi, mradi wa maji Bunda, mradi wa maji Bariadi, mradi wa maji Tarime, mradi wa maji Geita na mradi wa maji Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Na. 33

**Suala la Vijana Wengi kukimbilia Mijini**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA (k.n.y. MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Felister Bura Na. 178 tarehe 11/7/2006 hakutaja takwimu zozote za vijana wengi wanaokimbilia mijini, na kwa kuwa inasadikiwa kwamba katika nchi za Afrika (ikiwemo Tanzania) watu wake wanakimbilia Mijini kwa kasi kubwa kwa karibu mara mbili zaidi ya nchi za wenzetu wa *Latin America* na zile za Asia kwa kuwa, inasaidikiwa pia kwamba katika miaka 25 ijayo nusu ya wananchi za Afrika watakuwa wanaishi mijini kukaribia *Levels of Urbanization* ya zile za Ulaya bila kuwa na uwezo mzuri wa kiuchumi kuhimili ongezeko hilo la watu mijini:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo na imejiandaa vipi kukabiliana nalo?

(b) Je, Serikali inatambua kwamba, mkakati wowote wa ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini lazima uweke maanani suala zima la watu kuhamia mijini?

(c) Je, kwa nini jukumu la kuendesha miji limekuwa ni la Serikali za Mitaa *(Local Authorities)* ambazo kwa kiwango kikubwa zinakabiliwa na ukosefu wa Utawala bora na ukosefu wa uwezo wa rasilimali watu wenye ujuzi na fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la vijana kukimbilia mijini na tayari imeweka mikakati mbalimbali yenye lengo la kuweka mazingira mazuri sehemu za vijijini ili kuwafanya vijana wengi wabaki huko huko vijijini wakijishughulisha na uzalishaji mali na kujiongezea kipato. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mfuko wa vijana ili vijana waweze kubuni na kuanzisha miradi yao pale walipo kwa kukopeshwa fedha za mitaji kutoka kwenye mfuko huo.

(ii) Kuwahamasisha vijana wajiunge katika vikundi vya kuweka akiba na mikopo *(SACCOS)* vijijini ili waweze kukopeshwa kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali na kujiongezea mapato.

(iii) Vijana kupewa elimu ya ujasiriamali ili wanapokopa wawe na ujuzi wa kuiendesha miradi yao huko vijijini kwa ufanisi.

(iv) Mkakati wa kuwapatia vijana wetu mafunzo ya ufundi na stadi mbalimbali zinazolingana na mazingira yao ili waweze kuanzisha miradi inayozingatia mazingira yao, kama vile uvuvi, ufugaji, kilimo, useremala, ufugaji nyuki na kadhalika.

(v) Kuhamasisha shughuli za kilimo kupitia programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kutoa pembejeo, kupanua shughuli za ugani na pia kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo na usindikaji.

(vi) Serikali kuendelea hatua kwa hatua kuboresha miundombinu iliyopo vijijini ikiwa ni pamoja na barabara, mawasiliano, umeme vijijini, huduma za afya, maji, elimu na vituo vya michezo na burudani ili kuwafanya vijana waliopo vijijini watumie fursa zilizopo katika maeneo yao na hivyo kutotamani kukimbilia mijini.

Suala la kuendesha miji yetu lipo chini ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 iliyoanzisha mamlaka za Halmashauri za Wilaya na Sheria Na. 8 ya mwaka 1982 iliyoanzisha mamlaka za miji kwa lengo la kusogeza mamlaka karibu zaidi na wananchi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwa kuwa miundombinu ya barabara na umeme na maji anayozungumzia Mheshimiwa Waziri na kwa kuzingatia ukubwa wa nchi, miundombinu hiyo itachukua muda mrefu kutekelezwa wakati hivi sasa vijana wapo. Je, tusingechukua hatua muhimu za kuhakikisha kwamba mipango inafanyika pale ambapo vijana wapo katika miji kwa sababu hatuwezi kuwafukuza sasa?

Pili, kwa kuwa sekta ya kilimo ndiyo sekta mama inayoweza kusaidia ajira kwa vijana wengi, na kwa kuwa mipango hii Mheshimiwa Waziri anayoizungumzia katika baadhi ya Mikoa imeshindikana. Na yeye akiwa miongoni mwa Wabunge wanaotoka katika mikoa ya kilimo. Je, haoni kwamba inafaa kuanzisha programu maalum ya zana za kilimo na hususan majembe ya kukokotwa na ng'ombe kwa vijana ili wasilime na jembe la mkono kama babu zao? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali inatambua kwamba hata sasa wapo vijana ambao wako tayari mijini. Ndiyo maana katika mpango mzima wa Serikali Kuu haijafanya hatua ya kuboresha maeneo yaliyoko vijijini lakini pia tunafanya hatua za makusudi za kuboresha maeneo ya mijini. Kuvutia zaidi wawekezaji, kukuza sekta binafsi ili wale waliopo mijini waendelee kupata kazi na kujiajiri lakini vile vile Serikali inafanya mpango mkubwa wa kuboresha makazi ili kwamba zoezi hili la watu kuhamia mijini lisilete athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kwamba kwa sasa zaidi ya asilimia 70 ya makazi yetu yamejengwa kiholela na ndiyo maana Serikali katika hii miaka miwili mitatu iliyopita imeweza kutekeleza mpango wake wa kutengeneza viwanja vipya 55,000 ambavyo tayari vimepatikana. Serikali haitakaa kimya itaendelea kufanya hivi.

Lakini vile vile Mheshimiwa Spika, mpango mkubwa wa kilimo ambao ulifundishwa kwa Bunge uliona hayo yote ya zana za kilimo. Nataka niwahakikishie kwamba tulipotoa mafunzo kwa Bunge letu kuhusu mpango wa kilimo wa sasa *ASDP* tumedhamiria kweli kweli kuutekeleza. Tunaomba Wabunge tushirikiane katika kuutekeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimebaini tuko nyuma sana ya wakati Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nitakwenda haraka kidogo. Swali linalofuata ni Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake.

Na. 34

**Watanzania wanaofanya kazi nje**

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa wasomi wengi wametoroka nchini na kwenda kufanya kazi nje ya nchi:-

Je, Serikali ina takwimu zinazoonyesha kuna Watanzania wasomi wangapi nje?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa tunao wasomi wengi waliopo nje ya nchi ambao wanafanya kazi mbalimbali kama Madaktari, Wahandisi, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu, Manesi, Wachumi, Wanasheria na kadhalika.

Hata hivyo si sahihi kuwaita wasomi wote wanaofanyakazi nje ya nchi kuwa ni watoto kwa kuwa wamekuwa wanafuata taratibu zote za uhamiaji kabla ya kuondoka nchini. Hivyo sio watoro bali ni wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi hili la wasomi kutoka Tanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ni kundi muhimnu kwa kuwa linachangia kwa njia mbalimbali katika pato la Taifa. Kwa kutambua umuhimu wao Serikali inao utaratibu wa kuwatambua na kuwaorodhesha kupitia katika balozi zetu za nje. Hadi hivi sasa wamekwisha tambuliwa wasomi 8,570 waliopo katika nchi 27 duniani. Kwa kuwa zoezi hili bado linaendelea idadi hii itaongezeka baada ya wasomi wote waliopo nje kuorodheshwa kupitia Ofisi zetu za ubalozi. *(Makofi)*

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa nchi nyingi duniani sasa hivi zinafuatilia raia wao wako wapi na wanafanya nini na wanapata *revenue* kutokana na kazi wanazofanya.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja sasa ya kujaribu kupata *revenue* kutoka kipato cha Watanzania walioko nje kwa sababu Serikali iliwasomesha kwa pesa nyingi?

Swali la pili kwa kuwa *revenue* inapotea, wenzetu wa *West Africa* wanafanya hivyo na nchi nyingine. Naomba Waziri asinijibu kwamba kufanya kazi hiyo ni ngumu kukusanya *revenue* kutoka kwa Watanzania kwa sababu Serikali inahitaji *revenue?*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, wazo lake ni muhimu kufuatilia kipato cha Watanzania wanaoishi nje ni wazo zuri. Lakini jambo kubwa kuliko yote ambayo Serikali inakusudia ni kufanya watu wetu hawa wapende kuja kuwekeza nchini. Kwa hiyo, mazingira tunayotaka kutengeneza kwanza wajenge moyo wa kuipenda nchi yao. Muda wote wajisikie kuwekeza. Tunaamini kwa kuchukua vihela vidogo vidogo vya kuwafuatilia hawataleta mazao makubwa kwa Taifa kama watakavyoamua kuja kuwekeza kwenye nchi yao. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na majibu ya Naibu Waziri, na kutokana na majibu yaliyotolewa ndani ya Bunge lako hili jana kwamba madaktari walioko nje hawajulikani, na leo Waziri anasema kwamba wamefuata taratibu zote za kutoka nje ya nchi, na Waziri amewaita kwamba hawa sasa ni wajasiliamali.

Je, ni kauli ya Serikali kwamba hawa waliotoroka kama tulivyoambiwa jana ndio wajasiliamali wanaondoka na kutumia kodi ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kadri ambavyo

inawezekana Serikali ingependa Watanzania walioko nje wapewe moyo na sio kutengenezewa mazingira ya kutishwa, umetoroka, ulikimbia na kadhalika. Tunataka Watanzania waipende nchi yao warudi kujenga nchi yao. Hiyo ndio changamoto kubwa ya Serikali kwa sasa. Kwa hiyo, watafanya kazi hii kwa upendo kama tutawapa moyo, Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuwapa moyo Watanzania ama warudi ama wachangie kutoka huko waliko. *(Makofi)*

Na. 35

**Ukarabati wa Mpwapwa High School**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa shule ya sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School)* haijafanyiwa ukarabati mkubwa kwa muda mrefu sasa na kwa kuwa baadhi ya majengo yamechakaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia ukarabati mkubwa ikiwa ni pamoja na kuweka uzio katika shule hiyo?

(b) Kama mpango huo upo. Je, utekelezaji wake utaanza lini?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, kuweka uzio katika shule hiyo kutasaidia sana suala la ulinzi na usalama katika shule hiyo kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje mbunge wa Mpwapwa lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishafanya ukaguzi wa kina kubaini mahitajhi ya ukarabati wa majengo ya shule ya sekondari ya Mpwapwa, ambao utagharimu takribani shilingi milioni 250. Kwa kuwa mahitaji hayo ni makubwa, ukarabati wa shule hiyo utafanywa kwa awamu. Katika mwaka huu wa 2006/2007, shilingi miioni 100 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo. Ujenzi wa uzio haukuzingatiwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

(b) Taratibu za manunuzi zinaandaliwa ili ukarabati wa majengo ya shule hiyo uanze mwezi Machi, 2007.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kwelikuwa kuweka uzio katika shule hiyo kutasaidia sana katika suala la ulinzi na usalama wa shule. Tunatoa wito

kwa jamii kusaidia katika ujenzi wa uzio kama sehemu nyingine wanavyofanya.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kniweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba wametenga milioni 250 kwa ajili ya ukarabati wa shule ya sekondari ya Mpwapwa na kwa kuwa shule hii ina historia ndefu ina miaka 81 sasa tangu imeanzishwa na je Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kuacha majengo hayo bila kukarabati kwa muda mrefu yanailetea gharama kubwa Serikali, na kwa kuwa shule hii hata Mheshimiwa Ngeleja amesoma pale ilikuwa na historia ndefu?

Ningeomba niulize kwa kuwa hivi sasa kuna shule ya Serikali ya *Government Secondary School* na *Community Secondary School* na kwa kuwa walimu wote hao na wanalipwa na Serikali Kuu yaani Wizara ya Elimu. Sasa kwanini hizi shule za wananchi tunaachiwa kwamba wananchi ndio wajenge majengo yote na Serikali sasa hivi MMES haifahamiki.

Je, Serikali ina mpango gani kuongeza fedha kwa ajili ya kujenga shule za wananchi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):**: Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kweli shule ya sekondari ya Mpwapwa ni ya muda mrefu na inahitaji matengenezo makubwa.

Lakini ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba yote haya yanategemea uwezo wa Serikali, kwenye Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka wa fedha 2006/2007 tulitenga bilioni moja kwa ajili matengenezo na shule zilizokuwa zinahitaji matengenezo ni shule 100 kwa hiyo tukaona ni vizuri tuchukue chache tukatenga 16 ambazo tuliona zinahitaji msaada wa haraka sana katika matengenezo, moja wapo ikiwa ni shule ya Mpwapwa Sekondari. Kwa hiyo, hata hilo tu Mheshimiwa nadhani ungekubaliana na Wizara ya Elimu kwamba tumetumia busara kuiweka shule ya Sekondari ya Mpwapwa ikiwa mojawapo kati ya zile shule 16.

Kwa hiyo, kile kilichopatikana basi kitagawanya katika shule hizo 16 mwaka wa fedha mwingine tutaangalia kadri fedha zitakavyoapatikana na kuendelea kuiangalia hiyo shule ya Mpwapwa kama alivyoahidi na Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, la pili kama mlivyoshuhudia mwaka huu peke yake kuanzia Januari mpaka mwezi huu tayari tunaandikisha shule 647 shule mpya na kutokana na ongezekeo kubwa la vijana wetu wanaomaliza elimu ya msingi ambayo tunatarajia mwaka kesho laki nane, naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi kwamba tungesubiri uwezo mdogo wa Serikali hata robo ya shule hizo tusingeweza

naomba nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, muendelee kuhimiza wananchi kama mnavyofanya sasa hivi kuchangia nguvu zao mpaka kufanikisha shule mpya 647 ambapo tungesubiri Serikali tusingefikia hata kidogo. *(Makofi)*

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, wakati Mheshimiwa Rais anazindua Bunge letu tarehe 30/12/2005 moja ya kitu ambacho alikizungumza kwa msisitizo mkubwa ni kuwa na shule za kitaifa na shule ya sekondari ya Mpwapwa ni moja ya shule ya zamani sana ambayo ina hadhi ya kuwa shule ya kitaifa, ikiwemo pia *Tabora Girls* ambayo pia ina matatizo kama ya Mpwapwa.

Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu hizo rasilimali ambazo zinapatikana chache zielekezwe katika shule hizo za kitaifa ili kuendana na wazo la Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ziko shule za kitaifa na Mheshimiwa Rais alisisitiza hilo na ndio maana Wizara yetu ilitoa kipaumbele katika kuzikarabati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yako shule ambazo zitafanyiwa ukarabati mwaka huu mkubwa naomba nizitaje, ni shule ya Bagamoyo, *Tanga Technical,* Ruvu, Jangwani, Pugu, Minaki, Mpwapwa yenyewe, Ifunda, Tosamaganga, Bukoba, *Bwiru Girls,* Isumba, *Maswa Girls,* Mirambo, *Tabora Boys,* na Galanosi. Tumeona shule hizi ni za kitaifa na ziko nyingi, lakini hizi baada ya uthamini uliofanywa kwa wataalamu wetu zilibainika kwamba zinahitaji matengenezo ya haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naomba tukubaliane na Waheshimiwa Wabunge mahitaji ni makubwa uwezo wa fedha ni mdogo naomba tuzidishe subira.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni 54(1) Spika anaruhusiwa wakati wowote kulihutubia Bunge. Waheshimiwa Wabunge itakumbukwa wakati wa Mkutano wa Bunge wa Tano. Na naomba radhi leo *Order Paper* imekosea, sio Mkutano wa Tano ni wa Sita huu tunaoendelea nao. Masuala kadhaa yalijitokeza ambayo yalihusu ama mwongozo wa Spika ama kuhusu utaratibu. Maswala hayo yamenitaka nitoe maamuzi badala ya kuyatolea maamuzi wakati ule ule, niliona ni vyema niyapeleke kwenye Kamati za Kudumu za Bunge ili zifanye uchambuzi katika kunisaidia kutoa maamuzi ya wazi na ya haki.

Nafurahi kulitaarifu Bunge kwamba Kamati hizo zimemaliza kazi zake na kuandika taarifa na kunikabidhi, nimezisoma taarifa hizo na kwa mada zote zilizoletwa mbele yangu nimefikia maamuzi. Kwa vile taarifa hizo ni zangu na mimi ndiye ninayepaswa kutoa uamuzi ninatangaza kuwa uamuzi huo nitautoa leo mara baada ya shughuli za kuwapokea vijana waliofanikiwa zaidi darasa la saba na nitatoa uamuzi katika mambo matatu kati ya manne. Lile moja, bado tunalifanyia maandiko, kuliandikia vizuri zaidi.

Natoa taarifa hiyo Waheshimiwa Wabunge ili wale ambao wanapenda kunywa chai na wakati huo wajue tu ili nisisome maamuzi hayo muhimu Bunge likiwa Wabunge wengi hawapo. Hivyo ningependa Waheshimiwa Wabunge kadri itakavyowekezakana muwepo ukumbini ili msikilize maamuzi yangu kuhusu masuala hayo.

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika ahsante Ndugu Spika kabla ya kuuliza swali hili ningependa kutoka ufafanuzi ufufuatao. Swali hili na mengine niliuliza kabla ya kuteuliwa kwangu kuwa Mjumbe wa Baraza la Ushauri la Elimu katika Wizara hii. Kwa hiyo, napenda kutoa uamuzi rasmi kwamba kwa maswali mengine yapelekwe kwenye Baraza lakini kwa leo nikubali tu kwamba hili lijibiwe. ahsante sana.

Na. 36

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Mashuleni**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti na uchambuzi wa kina wa matumizi ya lugha za kufundishia unaonyesha kuwa vijana huelewa masomo kwa urahisi kama masomo yanafundishwa kwa lugha inayozungumzwa na watu wengi katika nchi *(Lingua Franca)* kama ilivyo lugha ya Kiswahili nchini kwetu:-

(a) Je, Serikali imetumia vigezo gani katika uamuzi wa kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia katika shule za sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu?

(b) Kama hoja ya kutumia lugha hiyo kufundishia imetokana na sababu kwamba, leo Kiingereza ni Kiswahili cha Dunia. Kwa nini ili kukidhi lengo hilo Serikali isipate walimu bora na Kiingereza kifundishwe kama somo la lazima kwa ngazi zote za elimu na kuruhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia masomo yote katika ngazi zote za elimu nchini?

(c) Je, wananchi wanasema nini kuhusiana na suala hilo katika dunia hii ya utandawazi ambapo dunia inazidi kuwa kama kijiji kimoja kwa kutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza bila kuathiri misingi ya utoaji elimu bora kwa watu wengi na kwa gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Mvangila Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vya elimu ya juu unatokana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995.

Kwa mujibu wa Sera hiyo mkazo umewekwa kwenye lugha ya Kiswahili na Kiingereza ambapo umahiri katika lugha ya Kiswahili utaimarisha utamaduni wetu, wakati Kiingereza kitawawezesha Watanzania kupata maarifa, kuelewa Sayansi, Teknolojia na kurahisisha mawasilano na nchi zingine katika ulimwengu wa utandawazi.

Aidha, kwa kuwa somo la Kiingereza linaanza kufundishwa tangu Darasa la Kwanza wahitimu wa Darasa la Saba wanategemewa kuwa na Stadi za kutosha kumudu kuzungumza na kuandika lugha hiyo ambavyo vinahitajika katika Elimu ya Sekondari na Ulimwengu wa kazi Naomba kusema kwamba agizo hili lipo kwenye Sera ya mafunzo ya mwaka 1995 Kifungu Namba 5.4.9.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati madhubuti ya kuboresha ufundishaji wa somo la Kiingereza ili kuwawezesaha wanafunzi kumudu masomo ya sekondari yanayofundishwa kwa lugha hiyo. Hatua zilizokwisha kuchukuliwa ni pamoja na kuboresha mitaala na mihutasari ya somo hili, kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kulifanya somo hilo kuwa la lazima tangu darala la kwanza hadi kidato cha nne. Aidha, Serikali inaendelea kuajiri walimu wa somo hilo na walimu waliopo hupewa mafunzo kazini ya mara kwa mara.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haijafanya utafiti hivi karibuni kupata maoni ya wananchi kuhusiana na suala hili katika dunia ya utandawazi. Kwa kuwa suala hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara upo umuhimu wa kufungua milango ya mjadala kuhusiana nalo ili wananchi watoe maoni yao.

Na. 37

**Ruzuku Katika Mbolea**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kutoa ruzuku katika mbole ama kuigawa Tanzania nzima katika jitihada zake za kuboresha kilimo nchini na hivyo kupiga vita umaskini:-

Je, Wilaya ya Singida na hasa katika jimbo la Singida Kusini wamepelekewa mbolea kiasi gani na imegawanywa vipi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge Singida Kusini, ningependa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Katika utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea, Wizara yangu inaratibu majukumu yote ya utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni pamoja na:-

- Kupata fedha ya ruzuku ya mbolea.

- Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya makubaliano kati ya makampuni na Serikali.

- Pia Wizara yangu inahusika na utoaji wa fidia katika makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya mbolea ya ruzuku ya Mkoa ina jukumu la kuhakikisha kuwa mbolea ya ruzuku inafikishwa katika vituo vikuu na kutoa taarifa Wizarani. Aidha, Mkoa unapaswa kuweka utaratibu wa kusimamia mbolea ya ruzuku na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watakao kiuka utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya mbolea ya ruzuku ya Wilaya inawajibika kuteua mawakala watakaonunua na kusambaza mbolea kwa mkulima ili itumike kama ilivyokusudiwa. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2005/2006 Serikali iliutengea Mkoa wa Singida jumla ya tani 330 za mbolea. Kati ya hizo jumla ya tani 22.5 zilinunuliwa na kutumiwa na wakulima kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Manyoni tani 1
(b) Wilaya ya Iramba tani 14.5
(c) Wilaya ya Singida (V) na Manispaa tani 1.8.

Mwaka 2006/2007 Serikali imeutengea Mkoa wa Singida jumla ya tani 820; tani 100 za *DAP*, tani 250 za *UREA*, tani 100 za *CAN* na tani 120 za *NPK*.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Katika swali langu la msingi mbali na maelezo mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, niliuliza pia mgao wa mbolea hii katika Wilaya yangu ya Singida lakini husasan katika Jimbo langu la Singida Kusini. Ni kiasi gani na maeneo gani na Mheshimiwa Naibu Waziri hakunisaidia mgawanyo wa mbolea katika Jimbo langu. Je, atakuwa tayari sasa kunieleza katika Jimbo la Singida Kusini na mbolea kiasi gani imepelekwa na imegawanywa wapi? Hilo la kwanza.

La pili; kwa kuwa yapo maelezo ya baadhi ya Wataalam wa kilimo kwamba mbolea inayopatikana Minjingu inafaa zaidi kwa mazingira ya Mkoa wa Singida. Je, Serikali inalifahamu hilo na inatoa kauli gani juu ya suala hilo na kama ni kweli inaweka utaratibu gani kutupatia sisi watu wa Mkoa wa Singida mbolea kutoka Minjingu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mbolea ambayo imetengwa kwa Mkoa wa Singida mwaka huu ama msimu huu ni tani 820. Tani zilizofika Singida ni tani 152 katika hizo ni tani 14 tu ambayo ni sawa na asilimia tisa ambazo zimenunuliwa bado Mbolea ipo kwenye maghala ya *Export Trading* pamoja na *Kilimanjaro Agrovet.*

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge akiwa ni mmoja wa wajumbe wa ile Kamati ya Wilaya alitakiwa yeye awe anajua kabisa kwamba ni kiasi gani ambacho kimeenda katika Jimbo lake lakini pia katika Wilaya hii au Mkoa wa Singida inaonekena kuna uhamasishaji mdogo wa utumiaji wa mbolea kwa mfano mwaka jana walitengewa tani 320 lakini walitumia tani 22.5 ambayo sawa na asilimia saba tu, na mwaka huu kama ninavyosema kwamba tayari zipo tani 152 ambazo zilikuwa pale na sasa hivi ni tani 14 tu ndizo zimekwisha nunuliwa. Kwa hiyo, uhamasishaji ni mdogo kwa watumiaji hakuna elimu ya kutosha kwa wale ambao wanatumia ile mbole lakini pia hakuna uhamasishaji kwa mawakala ambao ndiyo wanawauzia ile mbolea.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kusaidiana na Wanakamati kusudi waweze kutoa elimu ya kutosha kwa wale wasambazaji lakini pia na wakulima waweze kutumia mbolea. Kwa sababu kuna mawazo kwamba mbolea ya chumvi chumvi kule Singida inakausha ardhi wanapenda kutumia mboji au samadi.

Mbolea ya chumvi chumvi imepimwa inafaa kutumika kwa hiyo tunaomba usaidie uhamasishaji wewe ni mjumbe pamoja na Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Afisa Usalama, pamoja na Bwana Shamba wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika kuhusu mbolea ya Minjingu, kiwanda kilianza uzalishaji si zaidi ya mwaka mmoja na mwaka jana Disemba ndiyo ilikuwa wafikie kiasi kikubwa cha uzalishaji na sasa hivi bado wanauza hiyo mbolea. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe kwamba Serikali baadaye itatamka utaratibu wa kuweza kupata mbolea ile ya Minjingu.

Na. 38

**Mfuko wa Ukarabati wa Matrekta Yaliyochakaa Nchini**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE ( k.n.y. MHE. ELIETTA SWITI)** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali imekwishaanzisha mfuko wa kukarabati matrekta yaliyochakaa kwa nchi nzima:-

Je, upo uwezekano wa mfuko huo kutoa huduma zake Mikoani na Wilayani kadri ya mahitaji ili kuondoa usumbufu kwa wakulima wanaofuata huduma hiyo Dar es Salaam.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elietta Switi Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Serikali haijaanzisha Mfuko wa kukarabati matrekta machakavu kama ilivyoelezwa katika sehemu ya utangulizi ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Kilichoanzishwa na Serikali ni Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ambao pamoja na kutoa mikopo ya pembejeo inatoa pia mikopo ya ununuzi wa matrekta mapya na kukarabati matrekta machakavu. Mfuko wa pembejeo ulianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1994. Madhumuni yake ya awali yalikuwa ni kugharamia:-

- Uagizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo;

- Zana ndogo ndogo za kilimo; na

- Zana za mifugo na vifungashio vya mazao ili kuhakikisha kuwa zinawafikia wakulima na wafugaji kwa wakati mwafaka na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini umuhimu wa kumwezesha mkulima kuondokana na jembe la mkono na ili kuongeza uzalishaji, Serikali iliuagiza mfuko wa pembejeo kuanza kutoa mikopo ya kukarabati matrekta machakavu pamoja na ununuzi wa matrekta mapya kuanzia msimu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifutavyo:-

Katika utaratibu wa sasa maombi ya mikopo ya kukarabati matrekta inapaswa kuanzia katika ngazi ya Wilaya.

Maafisa zana wilayani ndio wanaokagua matrekta chakavu na kumshauri mwombaji, namna ya kuandaa na kuwasilisha maombi yake ya mkopo. Baada ya hapo mwombaji hujaza fomu za maombi ambazo zinapatikana katika ofisi za Afisa Kilimo Wilaya na hatimaye kuzipitishia kwa *DED*. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya huzipitia fomu hizo kabla ya kuziwakilisha kwenye mfuko wa Pembejeo Makao Makuu. Kwa kufuata utaratibu huo tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa usumbufu kwa wakulima wanaofuata huduma hiyo Dar es Salaam.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa kuna umangimeza mkubwa katika Mfuko huo wa Pembejeo ambao mimi mwenyewe binafsi nimeuona kwa sababu nilishiriki katika kufuatilia mkopo na kwa kuwa pia taratibu zenyewe zilizopo ni ndefu mno zinachukua kama unaomba kukarabati trekta labda usubiri mwaka mmoja au miwili.

Trekta jipya utakwenda, nenda rudi nenda rudi mwaka mzima na zaidi. Sasa nataka kumwuliza Waziri. Je, anaweza kuanzisha utaratibu gani wa kuharakisha

mchakato huu ili wananchi wakarabati haya matrekta waweze kununua matrekta mapya dawa na pembejeo kwa upesi inavyowezekana kwa kasi ya wakati huu?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na manung'uniko ambayo mojawapo ya manung'uniko yaliletwa na Mheshimiwa Mrope mwenyewe kwamba alijaribu kukopa na ikamchukua muda mrefu.

Lakini uchunguzi ambao niliufanya mimi mwenyewe katika kujaribu kusaidia kutatua tatizo hili ilionekana ya kwamba kulikuwa na matatizo ya ku-*register collateral* ya Mheshimiwa Mrope katika Wizara ya Ardhi ambayo ilichelewa kidogo na kwa hiyo kuchelewesha upatikanaji wa mkopo.

Lakini nimekwisha uagiza mfuko huu uharakishe na kuondoa vikwazo vinavyohusiana na mambo haya. Vilevile nimeuagiza Mfuko huo uchukue hatua za kurahisisha utoaji wa mikopo na tarehe 26 mwezi huu Bodi ya Mikopo ilikutana na kuunda Kamati ndogo ya kuchunguza na kuweka utaratibu ambao utarahisisha utoaji wa mikopo ili kuhakikisha kwamba mikopo hii inawafikia walengwa kwa haraka inavyowezekana.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mrope na wale wengine wanaoomba watuvumilie wakati tunajaribu kuchukua hatua za kurahisisha jambo hili. *(Makofi)*

Na. 39

**Athari za Mvua Zilizonyesha**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, mvua za vuli za mwaka uliopita (2006)ambazo zimeendelea hadi hivi sasa hasa katika maeneo ya Mikoa ya Kati zimeleta athari kubwa sana ikiwemo kuharibika kwa barabara, kubomoka kwa madaraja na nyumba, mafuriko na kadhalika na kwa kuwa, tayari Serikali ilishaweka ma-*contractor* kwa ajili ya utengenezaji wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mkoa wa Singida likiwemo Jimbo la Iramba Magharibi; na kwa kuwa ma-*contractors* hao walivunja madaraja ya zamani, bila kukamilisha madaraja mapya hatua ambayo imesababisha misongamano:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa ma-*contractors* hao ambao ni wakaidi na hawako tayari kutoa msaada wowote wa kunasua magari yanayokwama kwa kisingizio kwamba, ni nje ya Mkataba?

(b) Kwa kuwa hali hii ni mbaya sana katika daraja la Isuna, Msisi na mlima Sekenke hali inayosababisha kuwepo na msongamano wa zaidi ya magari 800 hadi 1000. Je, Serikali imetoa msaada gani kwa kipindi chote hasa kwa Vijiji vya Isuna, Msisi, Misigiri na Kibigiri ambavyo vimekumbwa na tatizo hilo na vimekuwa

vikipokea wageni bila kutegemea kwa kiwango kikubwa na kusababisha kutumia akiba yao ya chakula na kadhalika?

(c) Kwa kuwa, msongamano ni mkubwa na sura kama uhalifu unajitokeza, magonjwa ya mlipuko na huduma zingine za kibinadamu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha huduma kama *Mobile Ambulance*, huduma ya ulinzi (Polisi) na kadhalika. Maafa hayo yaliyolikumba Jimbo la Iramba Magharibi na Mkoa mzima wa Singida?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)** alijibu

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, mvua nyingi ambazo zimenyesha mikoa ya kati, ukiwemo Mkoa wa Singida, katika kipindi cha miezi ya Desemba 2006 na Januari, 2007 zimesababisha uharibifu mkubwa wa barabara zinazojengwa za Manyoni – Singida na Singida – Shelui na hivyo kuleta madhara ya kukwama kwa magari ya abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tukio hilo Wizara yangu iliwaelekeza makandarasi wa miradi hiyo kuzifanyia matengenezo barabara kwenye maeneo yaliyoharibika ikiwa ni pamoja na kusaidia kuvuta magari yanapokuwa kwenye sehemu zao. Makandarasi wote wanatekeleza na wataendelea kutekeleza maelekezo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na barabara kutopitika kama ilivyo kawaida, kumekuwepo na msongamano wa magari na watu katika baadhi ya vijiji vikuu sambamba na barabara ya kati kama vile Isuna, Msisi, Sekenke na maeneo mengine. Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Singida iliandaa utaratibu wa kuhakikisha usalama wa watu na mali zao katika maeneo hayo yaliyoathiriwa na mvua. Aidha, hapakujitokeza tatizo lolote la njaa.

Ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa mkoa wa Singida na wananchi wote ambao wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa wananchi waliokwama. Lakini iwapo vijiji vilivyopokea wageni wengi waliotokana na kukwama kwa magari vitakumbwa na upungufu wa chakula katika akiba yao, hilo litachukuliwa kama ni tatizo la kitaifa na litashughulikiwa na Serikali kulingana na taratibu zilizopo.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri kutokana na mipango na taratibu nzuri za uongozi wa mkoa wa Singida, hatukupata taarifa yaliyokumbwa na msongamano wa magari na watu wakati wa kipindi cha mvua na kama magonjwa ya namna hiyo yangejitokeza yangeshughulikiwa ipasavyo. Aidha, uongozi wa mkoa umeendelea kusimamia masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika maeneo hayo.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninamaswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa mwaka jana kipindi cha Bajeti wakati tunachangia Wizara ya Miundombinu Wabunge wa Mkoa wa Singida tulilalamikia juu ya wajenzi wa barabara hii ya kati toka Dodoma kwenda Singida mwisho mpakani mwa Mkoa wa Tabora  na tulilalamika kwa sababu uwezo wao ulikuwa mdogo kiutekelezaji na Waziri Mkuu kwa bahati nzuri alikwenda kule na alipokwenda kule akarejea lakini bado utaratibu ule wa utekelezaji bado ni hafifu. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wale makandarasi ambao utekelezaji wao ni mbovu?

La pili, Je, Wizara sasa haioni umuhimu kwamba sasa ishirikishe Kamati za Vijiji hasa kwa suala la uangalizi wa barabara kwa sababu hao *TANROADS* wameshindwa kuweza kuzimudu hizo barabara hasa kwa wakati wa mvua?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba makandarasi ambao wanajenga barabara hizo ambazo zimetajwa wamekuwa hawana utekelezaji wa kuridhisha na Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za Kimkataba za kuwaonya na za kuwasisitiza waendelee na kazi kama ambavyo inatakiwa na imefika mahali kwa kweli Serikali imeaamua kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba barabara hizi zinakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo haya na wananchi wote baada ya muda mfupi siyo zaidi ya wiki moja tutakuwa tumetoa taarifa kamili, tunachukua hatua gani, kama kutakuwa na haja ya kukatisha Mkataba kwa baadhi ya Makandarasi na tupate Mkandarasi mwingine atakayeweza kukamilisha barabara hasa ile inayotoka Manyoni kwenda Singida ambayo kwa kweli Mkandarasi ameonyesha uhafifu mkubwa katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kipindi kifupi, tutaamua kwamba Mkandarasi yule, basi aishie kilomita 63 na kilomita 55 zilizobaki tuweze kumpa mkandarasi mwingine aweze kukamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia Kamati za Vijiji badala ya *TANROADS* mimi nadhani *capacity* ambayo *TANROADS* wanayo ni kubwa kuliko ukisema kwamba utoe hii kazi ya kusimamia hizi barabara kwa Kamati ya Vijiji ambao kwa kweli hawawezi kuwa na *capacity* hasa kwa hizi barabara kuu ambazo zinahitaji kwanza uwezo mkubwa wa kifedha na Kamati za Vijiji hazitakuwa na uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, nadhani kinachotakiwa kifanyike kwa mfano, katika barabara hizi ni kuhakikisha kwamba zinapitika. Hao Makandarasi kama wasingekuwa na matatizo waliyokuwanayo walitakiwa wahakikishe kwamba barabara zinapitika kwa wakati wote ili magari yasiendelee kukwama kwa kuwa na vifaa na kuhakikisha kwamba wanafika kwenye maeneo yenye matatizo haraka iwezekanavyo na tumeendelea kuwasisitiza.

Mheshimiwa Spika, juzi mimi nilikuwa huko na wengi ni mashahidi kwamba niliongea nao na kusisitiza hilo na wameahidi kwamba wataendelea kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika na magari hayakwami kama ambavyo inatokea sasa hivi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niseme tu kwamba naongeza muda kidogo kwa sababu tuliutumia muda wa Maswali kwa matangazo ambayo yameupunguza muda huo.

Na. 40

**Sheria na Taratibu za Uanzishaji na Uendeshaji wa Mtandao wa Simu za Mkononi**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ya simu hasa za mkononi ni muhimu sana katika kuchochea shughuli za biashara na kuchangia maendeleo hata kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi:-

Je, ni sheria na taratibu gani zinazofuatwa katika kuanzisha na kuendesha mtandao wa simu za mikononi hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuanzisha na kuendesha mtandao wa simu hapa nchini, zipo taratibu mahsusi zinazotakiwa zifuatwe. Taratibu hizo zinatokana na sheria zinazoongoza uendeshaji wa masuala ya mawasiliano *(ICTs)* kama zifuatazo:-

(i) Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*The Tanzania Communications Regulatory Authority Act*. No. 12/2003 ambayo inatamka mwombaji awasilishe maombi yake kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambayo imepewa uwezo wa kutoa leseni na kudhibiti Sekta ya Mawasiliano nchini.

(ii) Sheria ya Mawasiliano *(The Tanzania Communication Act. No. 18/1993)* ambapo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepewa uwezo wa kutoa masharti ya leseni za mawasiliano.

(iii) Kanuni za Leseni za Mawasiliano, *The Tanzania Communication (Licensing) Regulation, 2005* ambapo utaratibu umewekwa wa kuomba Leseni za Mawasiliano. Kuanzia Februari, 2005, Mamlaka ilianzisha mfumo mpya wa leseni, *Converged Licensing Framework* ambapo leseni zilitolewa bila kujali

teknolojia na huduma *(technology service neutrality)*. Katika mfumo huu, mwombaji anaweza kuomba leseni zifuatazo:-

(a) Kumiliki miundombinu *(network facilities);*
(b) Kuendesha miundombinu *(network services);*
(c) Kutoa huduma za mawasiliano *(application services);* na
(d) Kutoa habari kwa njia ya Luninga au redio *(Content services).*

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata taratibu nilizozitaja hapo juu, mtu yeyote mwenye nia anaweza kuanzisha shughuli za mawasiliano ya simu za mkononi iwapo masafa ya kutosha yapo; iwapo mtu anao ujuzi au wafanyakazi wenye ujuzi katika fani zinazotakiwa; iwapo mtu huyo atakuwa na mtaji wa kutosha wa kuwezesha kufikisha huduma zake mahali alipopangiwa na kuwa na mpango wa kibiashara unaonyesha pia *rollout* ya kufikia katika maeneo mbalimbali, kutoa taarifa mbalimbali za kiufundi na iwapo kanuni na taratibu zilizowekwa amezielewa na kukubali kuzizingatia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu za mkononi yataweza kuchochea shughuli za kibiashara na kuchangia maendeleo hata kwenye maeneo ya pembezoni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ,amejibu vizuri kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichukue fursa hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa vile sasa Serikali imeamua kwamba itajenga Kiwanda Mama cha Chuma kule Liganga; na kwa vile kiutaratibu ingetegemea miundombinu pamoja na mawasiliano vitangulie kuwepo; naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni mikakati gani inachukuliwa kuwahamasisha wawekezaji kuanza kuwekeza katika mawasiliano hasa ya simu za mikononi katika maeneo yanayozunguka Liganga?

La pili, kwa vile Chama cha Mapinduzi kinahimiza kwamba katika kipindi hiki maeneo ya pembezoni mwa nchi yapewe msukumo katika maendeleo; na kwa vile eneo la Mwambao wa Ziwa Nyasa hasa katika Wilaya ya Ludewa kati ya Mbinga na Kyela liko mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa kiasi cha kilomita 500; na kwa vile ni pembezoni na wale wananchi ni Watanzania kama sisi wana haki ya kupata mawasiliano kama watu wengine na linahitaji ulinzi kwa sababu liko mpakani; Je, Wizara ina mikakati gani kuhakikisha kwamba eneo lile nalo la mwambao linakuwa na mawasiliano ya simu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kwamba tukianza suala la ujenzi wa Kiwanda cha Chuma cha Liganga tunahitaji pia miundombinu ya mawasiliano ya simu. Nadhani sio mawasiliano ya simu tu, ni pamoja na barabara, umeme na mambo yote yanayoendana ya kufanya kiwanda hicho ili kifanye kazi na kizalishe na wananchi

wanaoishi katika maeneo ya Liganga wapate mafanikio ya kiwanda hicho. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba masuala haya yanashughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika masuala aliyozungumzia ya simu katika maeneo ya pembezoni mwa nchi yetu, ni i kweli ninakubaliana naye kwamba Serikali imetoa upendeleo wa umuhimu kwamba maeneo ya pembezoni tuweze kupeleka mawasiliano ya simu. Kwa mfano, kule Mbeya tunapakana na Zambia na Malawi tuna-*connections*. Kule Kenya tuna *connections* Tanga na Namanga, Mtwara vilevile na Rwanda na Burundi na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mpango Kabambe ambao hivi sasa ni mapema sana kuusema, lakini mawasiliano ya simu yatafika katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema.

Mheshimiwa Mbunge nakuomba uvute subira kwa sababu juhudi kubwa za mawasiliano ya simu zinafanywa sio kwa makampuni ya simu za mikononi peke yake, lakini hata kwa Kampuni ya Simu ya *TTCL.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeongeza dakika kumi nadhani zimetosha. Sasa matangazo. Nawaomba mtambue uwepo wa wageni wa Mheshimiwa Bernadeta Mushashu ambao ni Joyce Mushashu na Hussein Kombo, hakusema wanamhusu vipi, lakini ni wageni wake. Naomba msimame wageni mliotajwa. Wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza awali, tutakuwa na wageni hapa, baadhi yao wataingia humu ndani ya Bunge. Ni vijana sita waliofanya vizuri sana katika mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2006. Sasa wao wako hapa kwa hiyo, tutawaona.

Ila napenda tu kutangaza kwamba wamesindikizwa na Walimu, Viongozi wa Elimu kutoka Wilaya na Mikoa inayohusika na muhimu zaidi pia na wazazi wao. Jumla yao wako 23, nawaomba wote wasimame. Wale pale. Ahsante sana. Kwa wazazi hongera sana kwa kuwalea vyema watoto wetu hao. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Malima Lubelje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati yake ya Katiba, Sheria na Utawala Saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa John Cheyo anaomba Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali wakutane saa 5.00 asubuhi, (sijui kama itawezekana) mara baada ya matukio mbalimbali muhimu ya humu Bungeni Chumba Namba 231 katika jengo la Utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane (nadhani nayo niirekebishe) baada ya matukio hapa, katika Ukumbi namba 432 ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Mara baada ya matukio hapa Kamati ya Maendeleo ya Jamii leo tarehe 01 Februari, 2007.

Mwisho, kutakuwa na hafla ndogo saa 6.30 mchana pale kwenye eneo letu la hafla mbalimbali kwenye Jengo la Utawala kwa ajili ya kuwaenzi hao watoto wa Darasa la Saba ambao sasa wameingia Kidato cha Kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, ni hafla fupi, lakini ni vizuri tuwe nao pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa ni mgeni rasmi. Kwa hiyo, siyo kitu kidogo.

Sasa naomba niwasomee utaratibu, *Serjeant at Arms* awe macho. Vijana sasa hivi wasimame kwenye mlango wa kuingia ndani ya Bunge. *Serjeant at Arm* msimamie hilo. Baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atoe maelezo mafupi kuhusu jambo lenyewe. Baada ya maelezo hayo mafupi nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, sijui yupi aliyepangwa lakini Mheshimiwa Mwantumu Mahiza simwoni ndani ya Ukumbi. Ah, Yupo na wanafunzi kule. Yeye sasa anatakiwa awataje mmoja mmoja ili waingie tuwatambue yupi ni yupi kwa mafanikio yapi. Wamepangiwa viti mkono wangu wa kulia, viti sita hivyo. Watakaa katika sehemu iliyopangwa kila mmoja akiingia.

Sasa baada ya hapo Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza nitamwomba tena asimame katika kipaza sauti hapa cha Waheshimiwa Mawaziri awataje mmoja mmoja washikane mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu na wakishashikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu watasimama mbele ya rungu la Spika wakiwatazama Waheshimiwa Wabunge mpaka waenee wote sita. Halafu watatoka kwa pamoja. Sasa naomba *Serjeant at Arms* tuendelee na utaratibu huu.

## TUKIO LA KUWAENZI VIJANA WALIOFANYA VIZURI MTIHANI WA DARASA LA SABA KITAIFA

*(Hapa vijana wahusika waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Vijana, simameni kwanza hapo mlipo. Nitamwomba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza amwite mmoja mmoja ili waende kukaa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kumtambulisha kwa Waheshimiwa Wabunge, Seif R. Mwingiliko, kutoka Shule ya Mapinduzi, Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namtambulisha Shedrack M. Wilson, kutoka shule ya msingi Mapinduzi, Serengeti. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawa wamepangwa kwa mujibu wa kufaulu kwao.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, namtambulisha Godfrey Isalu kutoka *Roken Hill Kahama,* Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namtambulisha Pauline Raphael, kutoka Kashishi Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, namtambulisha Azida A. Hassan, kutoka *Mvumi Mission* Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, namtambulisha Janeth Ayub, kutoka Kwesasu Same. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aelezee jinsi walivyopatikana na wamepangwa namna gani.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuzungumza kwa kifupi kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nimesimama mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kutoa shukrani za dhati kwa kukubali kuwatambua vijana wetu sita waliofanya vizuri zaidi katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka, 2006.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limeruhusu kutambulishwa vijana hawa kutokana na kuthamini umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo nchini. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa kuwatambua wanafunzi hawa itakuwa chachu kubwa sana kwa vijana wetu wa Tanzania waliomo mashuleni wafanye kazi kwa bidii zaidi na kufaulu kwa hali ya juu ili kuleta maendeleo nchini kama ilivyo kusudio la Mpango wa *MMEM* ambao unasimamiwa kwa karibu sana na Serikali ya Awamu ya Nne ambayo inaongozwa na Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua wanafunzi hawa hapa Bungeni Mheshimiwa Waziri Mkuu atawakabidhi vyeti na zawadi zilizoandaliwa katika hafla fupi itakayofanyika saa 6.00 kutokana na mambo mengi yaliyopo katika siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba umruhusu Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Mwantumu Mahiza atoe maelezo mafupi ya namna ambavyo wamefaulu. Tunawashukuru sana. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO Y A UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimtambulishe kwa Waheshimiwa Wabunge, kijana Seif Mwingiliko, kutoka Shule ya Mapinduzi, Rufiji ambaye ni kijana wa kwanza ambaye amepata jumla ya alama 230 kati ya 250. Nitataja kufaulu kwake. Kijana Seif alipata alama katika somo la Kiswahili 44, somo la Kiingereza 45, somo la Maarifa 45, somo la Hisabati 49, somo la Sayansi 47 Daraja 'A'. Seif naomba usimame. *(Makofi)*

**SPIKA:** Basi Kijana Seif upite ushikane mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu na usimame mbele ya rungu la Spika.

*(Hapa Kijana Seif Mwingiliko alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, huyo ndiye kijana wa kwanza kati ya maelfu ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Darasa la Saba mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pauline Raphael, ndiye binti msichana wa kwanza kati ya maelfu ya wasichana waliofanya mtihani wa Darasa la Saba mwaka uliopita kutoka Shule ya Kashishi, Kahama. Alipata alama katika somo la Kiswahili 44, somo la Kiingereza 46, somo la Maarifa 44, somo la Hisabati 46 na somo la Sayansi 48, jumla alipata alama 228 Daraja 'A'. *(Makofi)*

*(Hapa Pauline Raphael alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Akinamama vigelegele kwa binti!!! *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, binti anayefuatia kwa nafasi ya pili kwa wasichana katika mtihani wa Darasa la Saba uliopita ni Azida Hassan kutoka *Mvumi Mission*. Azida alipata alama katika somo la Kiswahili 40, somo Kiingereza 49, somo la Maarifa 41, somo la Hisabati 50, somo la Sayansi 46. Jumla alipata alama 226 Daraja 'A'. *(Makofi)*

*(Hapa Azida Hassan alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, anafuata kijana wa pili, Shedrack Wilson kutoka Mapinduzi, Serengeti. Shedrack Wilson yeye ameshika nafasi ya pili kwa wavulana, alipata alama katika somo la Kiswahili 46, somo la Kiingereza 47, somo la Maarifa 39, somo la Hisabati 48, somo la Sayansi 49 ana jumla ya alama 229 Daraja 'A'. *(Makofi)*

*(Hapa Shedrack Wilson alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, mwanafunzi Janeth Ayub, anayetoka Shule ya Kwasasu Wilayani Same alishika nafasi ya tatu kwa wasichana alipata alama katika somo la Kiswahili 45, somo la Kiingereza 45, somo la Maarifa 41, somo la Hisabati 49, somo la Sayansi 46 ana jumla ya alama 226 Daraja 'A'. *(Makofi)*

*(Hapa Janeth Ayub alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, mvulana wa tatu ni Godfrey Isalu, anatoka *Roken Hill,* Kahama, kufaulu kwake katika somo la Kiswahili alama 44, somo la Kiingereza 47, somo la Maarifa 43, somo la Hisabati 48, somo la Sayansi 47 alipata jumla ya alama 229 Daraja 'A'. *(Makofi)*

*(Hapa Godfrey Salu alipata fursa ya kushikana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangaza hapo awali kwamba kijana Seif Mwingiliko, kutoka Wilaya ya Rufiji, Shule ya Mapinduzi ndiye mwanafunzi wa kwanza katika mtihani wetu wa Darasa la Saba wa mwaka jana uliofanyika mwezi Septemba, 2006. Naomba wote tumpongeze kijana kwa mara ya pili na kupata mkono wa Mheshimiwa Waziri. Naomba upate mkono wa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wamesimama. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo kawaida yetu, nadhani nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aseme machache tu kwa niaba yetu kwa sababu wote hatuwezi kusema, Kiongozi wa Shughuli za Serikali yuko hapa basi aseme machache kwa niaba yetu sote.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nina hakika nitakuwa nasema kwa niaba yetu sisi wote, nikisema tumefurahi sana kwa vijana hawa walivyofanya vizuri. *(Makofi)*

Nimefurahishwa zaidi na yule wa kwanza kwa sababu ametoka Rufiji kwamba inawezekana kabisa na umbali wa Rufiji bado akapatikana mwanafunzi mwenye uwezo kuliko wengine wote. Natoa changamoto kwa shule nyingine nchini kuiga mifano ya hawa ili na wenyewe walete wanafunzi wao tuwapongeze hapa Bungeni kwa heshima kama hawa tuliyowapa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Walimu wao, walifanya kazi nzuri sana na tunawataka waendelee kufanya kazi nzuri. Tunakazania sana *quality* ya elimu na tunawaomba waendeleze ubora wa elimu yetu ili iendelee kuwa bora ili kutoa Watanzania wanaomudu karne na mapambano ya karne 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na kuwapongeza sana wazazi wao ambao wameamua kuwasindikiza wanapokuja kupata heshima hii. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia mtihani na kufanya jambo nzuri kama hili mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Basi *Serjeant at Arms* na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, nawaomba sasa muwatoe vijana kama walivyoingia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia hapo awali, sasa natoa maamuzi kuhusu hoja za taratibu na zilizotaka mwongozo wangu katika Mkutano wa Tano. Natoa maamuzi haya chini ya kanuni 4(2) na(3). Haya ni maamuzi ya Spika, hayana mjadala. Baada ya hapo, asiyeridhika anaruhusiwa chini ya Kanuni 4(3) kukata rufaa kwa Kamati ya Kanuni.

## UAMUZI WA SPIKA *(SPEAKER'S RULING)* KUHUSU UTHIBITISHO WA MAELEZO YALIYOTOLEWA BUNGENI NA MHE. JOHN M. SHIBUDA (MB.) NA MHE. JOHN M. CHEYO (MB.) TAREHE 6 JULAI, 2006 KUHUSIANA NA MFUKO WA KUENDELEZA ZAO LA PAMBA NA BODI YA WADHAMINI YA MFUKO WA ELIMU MKOA WA SHINYANGA

*[Umetolewa chini ya Kanuni ya 4(2) ya Kanuni za Bunge]*

Waheshimiwa Wabunge, kiini cha shauri hili ni madai (*allegations*) yaliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa John M. Cheyo dhidi ya Mheshimiwa John M. Shibuda kwamba, Mheshimiwa John M. Shibuda alisema uongo Bungeni, kinyume na ilivyo marufuku ya kufanya hivyo, kama ilivyo katika Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004).

Tarehe 6 Julai, 2006 wakati wa majadiliano ya kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mbunge wa Jimbo la Maswa, pamoja na mambo mengine, alieleza jinsi Mfuko wa Elimu wa Wakulima

ulivyosaidia katika ujenzi wa Shule za Sekondari katika Mkoa wa Shinyanga kwa maneno yafuatayo ambayo nayanukuu:-

"Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuja kuibua na kuzindua ari ya kujenga Mfuko wa Elimu. Mkoa wa Shinyanga elimu ni duni. Mfuko wa Elimu wa Wakulima katika Mkoa wa Shinyanga umejenga Sekondari 87. Nikirejea katika Wilaya yangu, katika miaka 45 toka tupate uhuru, Shule ya Sekondari ya Serikali ni moja. Katika Mkoa mzima tuna Sekondari 105. Juzi juzi tumeweza kujenga Sekondari 42 ambazo zimechangiwa na Mfuko wa Wakulima" [Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* za tarehe 6.7. 2006, uk. 37].

Baada ya Mheshimiwa Shibuda kuhitimisha mchango wake, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, alisimama na kutamka yafuatayo: Nanukuu tena:-

"Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 50, ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumza ameliambia Bunge hili kwamba, Shinyanga tumejenga *Secondary Schools* kwa kutumia Mfuko wa Pamba. Huo ni uongo kabisa na ingefaa atoe uthibitisho kwa hilo. Mheshimiwa Spika, tumewachangisha wananchi wa Bariadi na sehemu nyingine na sio kutumia Mfuko wa Pamba. Hela iliyo ndani ya Mfuko wa Pamba inaliwa na watu wasiojulikana na hilo linajulikana ndani ya Serikali. Kwa hiyo, nilitaka atoe uthibitisho au afute usemi wake."

Kufuatia madai ya Mheshimiwa John M. Cheyo ya kutaka Mheshimiwa John M. Shibuda athibitishe usemi wake, niliamua kulipeleka suala hilo mbele ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ili lifanyiwe uchunguzi wa kuthibitisha ukweli au vinginevyo wa kauli ya Mheshimiwa Shibuda.

Kamati hiyo ilifanya uchunguzi wake na baada ya kukamilisha uchunguzi wake, iliwasilisha taarifa yake kwangu. Napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Gedion Cheyo na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa kufanya kazi yao kwa haraka na kwa umakini.

Lakini pia, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote ambao, kwa namna moja au nyingine, waliisaidia Kamati hiyo ya Bunge katika kufanya uchunguzi wake kuhusiana na suala hili.

## Hoja za msingi *(issues)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 50 (1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004), pamoja na mambo mengine, inatamka kuwa, nanukuu: "Ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni".

Kwa hiyo, katika suala hili, hoja za msingi zilizoniongoza kufikia uamuzi ni tatu, nazo ni:-

(a) Je, matamshi ya Mheshimiwa John M. Shibuda Bungeni yalikuwa ya ukweli au ya uwongo?

(b) Je, Mheshimiwa John M. Cheyo alikuwa au hakuwa na haki ya kumtaka Mheshimiwa John M. Shibuda athibitishe ukweli wa yale aliyoyasema Mheshimiwa Shibuda Bungeni?

(c) Je, kutokana na mambo yaliyothibitika Mheshimiwa John Cheyo alikuwa sahihi kwa kumtuhumu Mheshimiwa Shibuda kuwa alisema uwongo siku ile?

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika uchunguzi wa suala hili, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ilibaini kwamba:-

(a) Mfuko wa Elimu Mkoa wa Shinyanga umechangia katika ujenzi wa Shule za Sekondari 42 kama alivyoeleza Mheshimiwa John M. Shibuda Bungeni;

(b) Mheshimiwa John M. Shibuda alithibitisha kuwa yale aliyoyasema Bungeni yalikuwa ni sahihi na hayakuwa mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Maamuzi yangu bado. Haya nayasoma ni mapendekezo ya Kamati kunishauri mimi;

(c) Mheshimiwa John M. Cheyo hakumtendea haki Mheshimiwa John M. Shibuda, kwa kudai kuwa aliyoyasema Mheshimiwa Shibuda Bungeni ni uongo, kabla ya Mheshimiwa Shibuda hajatoa uthibitisho kuhusiana na maelezo yake.

**Uchambuzi wa Majibu ya Hoja za Msingi**

Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge, pamoja na mambo mengine, inatamka kwamba, "Spika au Mbunge yeyote aweza kumdai Mbunge anayetoa maelezo Bungeni atoe uthibitisho wa usemi wake."

Fasili ya Kanuni hii inajibu hoja ya msingi ya kwanza kwamba, Mheshimiwa John M. Cheyo alikuwa na haki ya kumtaka Mheshimiwa John M. Shibuda athibitishe ukweli wa yale aliyoyasema Bungeni.

Matokeo ya uchunguzi wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi yanajibu hoja ya pili ya msingi kwamba, Mheshimiwa John M. Shibuda amethibitisha ukweli wa yale aliyoyasema Bungeni. Aidha, pia yanabainisha kuwa matamshi ya Mheshimiwa John Cheyo dhidi ya Mheshimiwa John Shibuda hayakuwa sahihi.

**Madhumuni ya Kanuni ya 50(1)**

Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge, imewekwa na Bunge kwa madhumuni ya kuzuia na kupiga marufuku Mbunge kusema uwongo anapokuwa anatoa maelezo Bungeni na pia kuhakikisha kwamba, maelezo yanayotolewa na Mbunge Bungeni ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu.

Kama zilivyo Kanuni nyingine, Kanuni hii ni ya muhimu sana katika kulinda na kudumisha heshima na Mamlaka ya Bunge kama Taasisi. Bungeni si mahali pa kusema uongo au kutoa maelezo ya kubuni au ya kubahatisha tu.

**Matumizi (*Application*) ya Kanuni ya 50(1)**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004), pale ambapo itaonekana kuwa kuna haja ya kuhakikisha kwamba, maelezo yanayotolewa Bungeni ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au kubahatisha tu, Spika au Mbunge yeyote mwingine ana haki ya kumtaka Mbunge anayetoa maelezo hayo athibitishe ukweli wa maelezo hayo.

Kwa mujibu wa Kanuni hii, jukumu la kuthibitisha *(burden of proof)* ukweli wa maelezo yaliyotolewa Bungeni lipo kwa Mbunge aliyetoa maelezo husika Bungeni. Jukumu la kufanya hivyo halipo kwa Spika au Mbunge mwingine yeyote anayedai uthibitisho wa yale yanayozungumzwa na Mbunge husika Bungeni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote anayedai uthibitisho wa yale yaliyozungumzwa Bungeni, hatakiwi kutoa maelezo mengine ya ziada yenye lengo la kumhukumu Mbunge aliyetoa maelezo husika kuwa, amesema uongo kabla ya uthibitisho unaotakiwa haujatolewa.

**Uamuzi wa Spika**

Kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi juu ya suala hili na kwa kuzingatia ufafanuzi wa Kanuni husika ya Bunge nilioutoa hapo juu, natoa uamuzi kwamba:-

(a) Mheshimiwa John M. Shibuda amethibitisha kwamba, yale aliyonukuliwa kuyasema Bungeni tarehe 6 Julai, 2006 wakati akichangia hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, yalikuwa ni ya kweli.

(b) Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa uelewa wake wa suala husika, alikuwa na haki ya kumtaka Mheshimiwa John M. Shibuda athibitishe yale aliyokuwa ameyasema Bungeni.

(c) Pamoja na haki hiyo, hata hivyo, kwa matamshi yake kwamba "Huo ni uwongo kabisa", Mheshimiwa John Cheyo hakumtendea haki Mheshimiwa John M. Shibuda kwa kutoa hukumu kabla ya

uthibitisho alioutaka utolewe na Mheshimiwa John M. Shibuda ulikuwa haujatolewa.

(d) Kwa matamshi hayo ambayo ni dhahiri hayakumtendea haki Mheshimiwa John M. Shibuda, namtaka Mheshimiwa John M. Cheyo amwombe radhi Mheshimiwa John M. Shibuda, kwa njia yoyote inayofaa na iliyo bayana kabla ya Mkutano wa Bunge wa Sita kumalizika.

Uamuzi huu umetolewa Dodoma tarehe 1 Februari, 2007. *(Makofi)*

Sasa naketi kwa sekunde chache kama kuna rufaa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, hakuna rufaa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Suala la pili.

## UAMUZI WA SPIKA *(SPEAKER'S RULING)* KUHUSU UTHIBITISHO WA KAULI YA MHE. CHACHA ZAKAYO WANGWE, MBUNGE WA JIMBO LA TARIME, ALIYOITOA BUNGENI TAREHE 10 JULAI, 2006.

*[Umetolewa chini ya Kanuni ya 4 (2) ya Kanuni za Bunge]*

### Maelezo *(facts)*

**SPIKA:** Mnamo tarehe 10 Julai, 2006, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Jimbo la Tarime na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maji, alipokuwa akitoa maoni ya Kambi hiyo, pamoja na mambo mengine, alitamka kwamba:-

"Natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Tarime, kwa kusimama imara kuitetea Demokrasia ya kweli katika nchi hii, bila kujali vitisho, majeraha na mauaji wakanichagua mimi mnyonge mwenzao na kukataa takrima ili niwe sauti ya wasiokuwa na sauti hapa Bungeni. Waliopoteza maisha yao, Mungu awarehemu."

Baada ya matamshi hayo, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti (Mb), alisimama na akamtaka Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) athibitishe matamshi yake, kwa maneno yafuatayo:-

"Mheshimiwa Chacha Wangwe, katika maelezo yake ameeleza hapa kwamba, wapiga kura wake walimchagua, pamoja na mauaji yaliyofanyika. Sasa tunataka athibitishe kauli yake na kama hana uwezo wa kuthibitisha, basi aiondoe hiyo kauli."

Mheshimiwa Chacha Wangwe hakuiondoa kauli. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Wangwe kueleza kwamba alikuwa tayari kuthibitisha ukweli wa hayo aliyoyasema Bungeni, niliamua kulipeleka suala hilo mbele ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ili kufanyiwa uchunguzi wa kuthibitisha iwapo aliyoyasema Mheshimiwa Wangwe Bungeni ni ya kweli au la.

Kamati hiyo ya Bunge ilitakiwa kuthibitisha, kuwepo ama kutokuwepo kwa mauaji yaliyodaiwa na Mheshimiwa Wangwe kutokea katika Jimbo la Uchaguzi la Tarime wakati wa mchakato wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2005.

Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilifanya uchunguzi wake na kuwasilisha taarifa yake ya uchunguzi kwangu. Napenda kumshukuru Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Kusila na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kufanya kazi yao ipasavyo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Uchunguzi uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama umebaini kuwa, ni kweli kulikuwepo na fujo, vitisho, vurugu, vitendo vya kujeruhi na mauaji kwenye Jimbo la Tarime, katika kipindi cha mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2006.

Kamati pia ilibaini kwamba, fujo, vitisho, vurugu, vitendo vya kujeruhi na mauaji hayo hayakufanywa na Chama chochote cha Siasa au Serikali na kwamba, waliofanya vitendo hivyo ni watu binafsi na walifanya hivyo kwa malengo yao binafsi na si kwa maslahi ya Chama chochote cha Siasa wala Serikali.

Vile vile Kamati ilibaini kwamba, katika kipindi hicho kulikuwa na matukio mengi ya uhalifu Wilayani Tarime yaliyosababisha majeruhi na mauaji. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, tukio moja husika la mauaji lilitokana na ugomvi uliosababishwa na ushabiki binafsi na kwa namna yoyote ile, mauaji hayo hayakuchochewa na Chama chochote cha Siasa wala Serikali.

Kamati pia ilibaini kwamba, katika kipindi hicho cha mchakato wa Uchaguzi Mkuu, watu kadhaa walijihusisha katika kufanya vitendo vya kihalifu katika Jimbo la Tarime kwa manufaa na malengo yao binafsi.

Kamati vile vile ilibaini kuwa, katika Wilaya ya Tarime kuna matukio mengi sana ya uhalifu, ikiwa ni pamoja na wizi wa mifugo, ugomvi na mapigano ya koo mbalimbali *(clan or cultural clashes)* yanayosababisha matukio mengi ya mauaji. Kwa hiyo, kwa kutafakari nikazingatia hoja za msingi zifuatazo ili kufikia uamuzi:-

**Hoja za msingi *(issue)***

Hoja za msingi hapa ni mbili tu zifuatazo:-

(a) Je, kauli ya Mheshimiwa Wangwe ina tafsiri gani?

(b) Je, kutokana na uchunguzi uliofanywa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wangwe amethibitisha ama hajathibitisha ukweli wa kauli yake aliyoitoa Bungeni?

**Majibu ya Hoja za Msingi**

Ni dhahiri kabisa, kauli ya Mheshimiwa Wangwe inaweza kutafsiriwa kwamba, yeye ni shujaa aliyechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Tarime, bila wananchi hao kujali vitisho, majeraha na mauaji yaliyokuwa yanafanywa ya kumzuia yeye asichaguliwe.

Vile vile kauli hiyo ya Mheshimiwa Wangwe inaweza kupewa tafsiri ya kwamba, vitisho, majeraha na mauaji aliyokuwa anayazungumzia, yalifanywa kwa sababu za kisiasa na kwa malengo ya kisiasa *(politically instigated)* kwa lengo la kumzuia yeye asichaguliwe.

Aidha, ni dhahiri kabisa kwamba, kwa taathira yake *(by implication)*, kauli ya Mheshimiwa Wangwe ilikuwa inamaanisha kwamba, vitisho, majeruhi na mauaji yaliyofanyika katika Jimbo lake la Uchaguzi la Tarime wakati wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2005 ni vitendo ambavyo vilifanyika kwa sababu za kisiasa na kwa malengo ya kisiasa.

Ni ukweli ulio wazi kwamba, kauli kama hiyo, hasa pale inapohusisha kitu kibaya kama mauaji, ni hatari na inaweza kuleta madhara makubwa katika jamii. Maelezo niliyoyatoa hapo juu, yanajibu hoja ya Kwanza ya msingi kuhusu tafsiri ambayo kauli ya Mheshimiwa Wangwe inapaswa kupewa.

Taarifa ya Uchunguzi wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama imethibitisha kutokea kwa vitisho, majeraha na mauaji katika Jimbo la Uchaguzi la Tarime wakati wa mchakato wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2005.

Hata hivyo, uchunguzi huo wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama umebaini pia kuwa, vitisho, majeraha na mauaji hayo hayakuwa ya kisiasa na wala hayakufanyika kwa maslahi na malengo ya kisiasa.

Matokeo ya uchunguzi huo yanajibu hoja ya pili ya msingi kwamba, kwa mujibu wa tafsiri ya kauli ya Mheshimiwa Wangwe niliyoitoa kwenye aya ya 4.1 hadi 4.4 hapo juu, Mheshimiwa Wangwe ameshindwa kuthibitisha ukweli wa kauli yake aliyoitoa Bungeni tarehe 10 Julai, 2006, yaani kuthibitisha kwamba vitisho, majeraha na mauaji hayo yalikuwa ni ya kisiasa *(politically instigated).*

**Uamuzi *(Ruling)***

Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, baada ya uchunguzi wake, iliridhika kwamba, Mheshimiwa Wangwe alikuwa amethibitisha ukweli wa kauli yake aliyoitoa

Bungeni, yaani, kuwepo kwa vitisho, majeraha na mauaji yaliyodaiwa na Mheshimiwa Wangwe kutokea katika Jimbo la Uchaguzi la Tarime wakati wa mchakato wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Desemba, 2005.

Hata hivyo, kwa mujibu wa tafsiri ya kauli ya Mheshimiwa Wangwe iliyotolewa kwenye aya ya 4.1 hadi 4.4 hapo juu, Mheshimiwa Wangwe hajakidhi matakwa ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) kwa sababu, kwa mujibu wa kauli yake, haitoshi kwa yeye kuthibitisha tu kuwepo kwa vitisho, majeraha na mauaji aliyodai kuwa yalitokea, bali pia alipaswa athibitishe kuwa, vitisho, majeraha na mauaji hayo yalikuwa ni ya kisiasa na yalifanywa kwa maslahi na malengo ya kisiasa *(Politically instigated).*

Kwa kuzingatia mwongozo na ufafanuzi nilioutoa hapo juu, ni wazi kwamba, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe ametenda kosa la kusema uongo Bungeni chini ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) na anastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Hata hivyo, kwa kuwa hilo ni kosa la kwanza kwa Mheshimiwa Wangwe, ambalo bila shaka amelitenda kutokana na ugeni wake kuhusu taratibu na Kanuni za Bunge, ninatoa uamuzi kwamba, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe asichukuliwe hatua zozote za nidhamu za kuadhibiwa na Bunge, badala yake namtaka afute kauli yake aliyoitoa Bungeni tarehe 6 Julai, 2006 kabla ya Mkutano wa Bunge wa Sita kumalizika kuondoa hisia kuwa vitisho, majeraha na mauaji Wilayani Tarime mnamo mwaka 2005 vilikuwa ni vitendo vya kisiasa.

Vile vile natoa mwongozo kwa Mheshimiwa Wangwe kwamba, kwa siku za usoni anatakiwa awe makini na mwangalifu zaidi katika kauli zake Bungeni ili asirudie kosa kama hilo.

Uamuzi huu nimeutoa tarehe 1 Februari,2007 hapa Bungeni Dodoma. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wabunge, naona hakuna rufaa. Uamuzi wangu wa tatu na wa mwisho.

**UAMUZI WA SPIKA *(SPEAKER'S RULING)* KUHUSU SHAURI LA UTOVU WA NIDHAMU DHIDI YA MHE. KABWE ZUBERI ZITTO MBUNGE WA KIGOMA KASKAZINI**

[*Umetolewa chini ya Kanuni ya 4 ya Kanuni za Bunge*]

**Maelezo (*facts*)**

**SPIKA:** Tarehe 2 Novemba, 2006, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya Uchaguzi wa kuwachagua Wabunge wa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uchaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni

zinazohusika na Uchaguzi huo, *(The East African Legislative Assembly Election Rules)* zilizotungwa chini ya Kanuni ya 9A ya Kanuni za Bunge.

Katika Uchaguzi huo, baadhi ya Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani Bungeni, walisusia na kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge, wakidai kutoridhishwa na jinsi ambavyo Uchaguzi huo ulivyoendeshwa.

Baada ya kususia Uchaguzi huo, Wabunge hao walikutana na vyombo mbalimbali vya habari kuelezea sababu zilizowafanya wachukue uamuzi wa kususia Uchaguzi huo na hatua walizopanga kuchukua.

Miongoni mwa Wabunge waliosusia Uchaguzi huo na kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge ni Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, (CHADEMA) ambaye, alinukuliwa na Magazeti ya NIPASHE na TANZANIA DAIMA ya tarehe 3 Novemba, 2006, pamoja na mambo mengine, nanukuu: "Akihoji uelewa wangu nikiwa Spika wa Bunge hili wa Kanuni za Bunge zilizotumika kuendesha Uchaguzi huo, kwamba ama hazijui au anazijua, lakini aliamua kuzipindisha kwa makusudi ili kusaidia Chama chake."

Baada ya hapo, tarehe 6 Novemba, 2006 Bungeni, nilimtaka Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe aniombe radhi ndani ya siku tano, kwa kauli yake nje ya Bunge, iliyoonesha dharau na utovu wa nidhamu kwangu binafsi na kwa nafasi yangu kama Spika wa Bunge hili. Muda huo wa siku tano, uliisha bila Mheshimiwa Kabwe kuniomba radhi.

Kwa kuwa Shauri hili linahusu maadili ya Mbunge hususan, kuonyesha dharau kwa Spika na kutotii maelekezo yake, kinyume na kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988, nilipeleka shauri hili mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili lishughulikiwe. Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ililichunguza suala hili na kuwasilisha taarifa yake kwangu.

Nawashukuru sana Mwenyekiti - Mheshimiwa Juma S. N'hunga na Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa kutekeleza kazi yao ipasavyo na kuwasilisha taarifa yao kwangu katika muda muafaka.

## Uchunguzi wa Kamati

### Utetezi wa Mheshimiwa Kabwe

Alipoitwa mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Kabwe alikiri kuongea na Waandishi wa Habari na kwamba alielezea kutoridhika kwake na namna uchaguzi husika ulivyoendeshwa.

Hata hivyo, Mheshimwia Kabwe alikanusha kutoa matamshi yaliyonukuliwa na Vyombo vya Habari ambayo yanaonesha kunidharau mimi Spika wa Bunge.

Aidha, Mheshimiwa Kabwe alijitetea kuwa, katika mazungumzo yake na Waandishi wa Habari hakutamka kuwa Mheshimiwa Spika hafahamu Kanuni za Bunge na hatarajii kutoa kauli kama hiyo.

Mheshimiwa Kabwe pia alijitetea kuwa, wakati nikitoa tamko la kumtaka aniombe radhi, yeye alikuwa safarini nchini Ujerumani, kwa ruhusa rasmi ya Ofisi ya Spika, iliyoshughulikiwa na Mheshimiwa Halima Mdee. Baada ya kurejea kutoka Ujerumani, Mheshimiwa Kabwe alifanya jitihada kadhaa za kuonana nami ili kuniomba radhi, lakini jitihada hizo hazikufanikiwa kutokana na mimi kuwa ama nje ya nchi ama safarini ndani ya nchi.

**Matokeo ya Uchunguzi**

Kamati ilibaini kuwa, matamshi ya Mheshimiwa Kabwe yalikuzwa na Vyombo vya Habari. Isitoshe, Mheshimiwa Kabwe ameonesha kwa vitendo, kujutia yote yaliyotokea. Vilevile Kamati iliridhika kuwa, Mheshimiwa Kabwe alifanya jitihada za kukutana nami ili aniombe radhi.

Aidha, kwa maombi yake, kupitia kwa Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Mheshimiwa Kabwe alipata nafasi ya kuonana nami Ofisini kwangu, Dar es salaam na kuniomba radhi mnamo tarehe 20 Januari, 2007. *(Makofi)*

**Hoja za msingi (*issues*)**

Ili kulitolea uamuzi suala hili, tunapaswa Waheshimiwa Wabunge tujiulize na kujibu hoja tatu za msingi:-

(a) Je, Mbunge anayo au hana haki ya kuhoji uamuzi wa Spika au utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge?

(b) Je, ni kosa au si kosa kwa Mbunge kutoa kauli inayomdharau Spika ndani au nje ya Bunge?

(c) Je, vitendo alivyovifanya Mheshimiwa Kabwe ni vya utovu wa nidhamu na ukiukaji wa maadili ya Mbunge au la?

Hoja hizi nitazijibu ipasavyo kwa kuzingatia Kanuni za Bunge, pamoja na msimamo wa Sheria inayohusika, yaani Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, 1988 (No. 3 of 1988*)].

**Majibu ya Hoja za msingi**

Fasili ya Kanuni ya 4(3) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) inatoa jibu lililo wazi kwa hoja ya kwanza kwamba, Mbunge yeyote anayo haki ya kuhoji uamuzi wowote wa Spika kama haridhiki nao. Spika ni binadamu, sio Malaika, yawezekana wakati fulani

uamuzi wake ukawa sio sahihi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na taratibu nyingine za Kibunge *(human error).*

Katika hali kama hiyo, Mbunge yeyote ambaye haridhiki na uamuzi wa Spika, anayo haki ya kuhoji uamuzi huo kwa utaratibu wa kanuni.

Ibara ya 100 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inaweka na kulinda, pamoja na mambo mengine, uhuru wa utaratibu, na uhuru huo haupaswi kuvunjwa wala kuhojiwa mahali penginepo nje ya Bunge.

Ibara ya 100 (1) haimzuii Mbunge au mtu mwingine yeyote kuhoji utaratibu, kwa maana ya uendeshaji wa shughuli za Bunge, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, bali kinachokatazwa na Ibara hiyo ni kuhoji utaratibu huo mahali penginepo nje ya Bunge.

Nitakuwa na maelezo zaidi katika shauri la nne ambalo nalo nitalitolea uamuzi linalohusu malalamiko ya Mheshimiwa Malima, Mbunge wa Mkuranga na Bwana Mengi - Mwenyekiti wa *IPP* hapo baadaye kidogo.

Kifungu cha 24 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988 kinatamka kuwa: "Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la kumdharau Spika *(contempt)* iwapo, kwa maneno au vitendo, ataonyesha dharau kwa Spika."

Kwa mujibu wa Kifungu cha 24 (e) cha Sheria hiyo: "ni kosa vile vile la dharau *(contempt)* kwa mtu yeyote, kwa makusudi kufanya kitendo chochote cha kudharau mwenendo wa shughuli za Bunge au kumdharau mtu yeyote ambaye ni Mwenyekiti wa shughuli hizo." Yaani Naibu Spika, Wenyeviti wetu wanapokaa hapa, ukimdharau ni kosa la *contempt* na lina adhabu yake.

Kwa mujibu wa vifungu hivyo vya Sheria, ni dhahiri kwamba, ni kosa kwa Mbunge kutoa kauli au kutenda kitendo chochote, kinachomdharau Spika, iwe ni ndani au nje ya Bunge.

Kwa mujibu wa uchambuzi na ufafanuzi uliotolewa hapo juu, nimeridhika kwamba, Mheshimiwa Kabwe alifanya makosa yafuatayo:-

(a) Kutoa kauli au matamshi yanayoonyesha dharau kwangu nikiwa Spika wa Bunge hili, kinyume na kifungu cha 24(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988; na

(b) Kuonyesha dharau kwangu nikiwa Spika wa Bunge hili, kwa kitendo chake cha kutokutii maelekezo yangu ya kumtaka aniombe radhi ndani ya kipindi cha siku tano.

**Uamuzi *(Ruling)***

Kwa kuzingatia mwongozo na ufafanuzi nilioutoa hapo juu, ni wazi kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto alitenda makosa ambayo alistahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge.

Hata hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Kabwe alifanya jitihada za dhahiri za kunitafuta ili kuniomba radhi;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Kabwe alikuja kwangu, akiongozana na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa N'hunga na kuniomba radhi;

Na kwa kuwa hilo ni kosa la kwanza kwa Mheshimiwa Kabwe, ambalo bila shaka, amelitenda kutokana na ugeni wake kuhusu taratibu za Bunge;

Uamuzi wangu ni kwamba, nimemsamehe Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe na kwa hiyo, hataadhibiwa na Bunge hili. Hata hivyo, natoa mwongozo kwamba, kwa siku za usoni, awe makini na mwangalifu ili asirudie makosa kama haya.

Uamuzi huu umetolewa Dodoma tarehe 1 Februari, 2007.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Itifiki ya Nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Africa *(The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of Women in Africa)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha itifaki hiyo, naomba uniruhusu nianze kwa kuwatakia Waheshimiwa Wabunge wote heri na fanaka ya Mwaka Mpya wa 2007. Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai na kuanza Bunge letu Tukufu mwaka 2007 tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza katika Bunge hili kuongea, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, wewe Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumpoteza mwenzetu na ndugu yetu mpendwa, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti ambaye alipoteza maisha wakati akitekeleza

majukumu ya kitaifa. Serikali na Bunge letu vimepata pigo kubwa kwa kumpoteza kiongozi mchapa kazi na mwenye upendo kwetu sote.

Nachukua nafasi hii pia kuwapa pole familia ya Marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Tunduru. Hatuna budi kukumbuka na kuyaenzi yote mema aliyofanya na aliyokusudia kuyafanya kabla mauti hayajamfika. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Dr. Asha-Rose Migiro alikuwa Mbunge mwenzetu na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Ni dhahiri kuwa Bunge letu Tukufu pamoja na wananchi wa Tanzania kwa ujumla, wanayo kila sababu ya kuona fahari na kujivunia uteuzi wake. Mheshimiwa Migiro ameifanya Tanzania iendelee kujulikana na kupata sifa kubwa katika medani ya kimataifa. Tunayo furaha kubwa hasa sisi akina mama, kuona mwenzetu Dr. Migiro anakuwa Balozi na mwakilishi wa Bunge letu Tukufu na Bara letu la Afrika kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na uwezo wa kufanya kazi zake kwa ari mpya, nguvu na kasi mpya na kwa ufanisi mkubwa. Yote hayo ni matunda ya imani iliyojengwa na Marehemu Baba wa Taifa Mwl. Nyerere.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Wiliam Ngeleja kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Tunawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushrikiano wao wakati wa kuleta Itifaki hii katika Bunge lako. Itifaki hii ilipitishwa na Mawaziri wa Afrika tarehe 28 Machi, 2003 Mjini Addis Ababa, Ethiopia. Itifaki hii ni nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu *(The African Charter on Human and People's Rights)* ambao Tanzania iliridhia tarehe 16 Februari, 1984.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 Wakuu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, kama ulivyoitwa wakati huo, walipitisha Azimio kuitaka Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu kufafanua nafasi na haki ya mwanamke Barani Afrika ambazo hazikuelezwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu. Ili kutekeleza Azimio hilo, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu ilipendekeza kuwepo kwa Itifaki ya Mkataba huo itakayohusu haki za wanawake wa Afrika. Tanzania iliweka saini Itifaki hii tarehe 5 Novemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria za Kimataifa zinatoa wajibu kwa nchi wanachama au nchi zinazosaini Mikataba na kuridhia kutekeleza masharti ya Mikataba hiyo bila kusukumwa, kushurutishwa wala kulazimishwa ikiwa ndiyo njia pekee ya utekelezaji wa makubaliano katika Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika, ni muhimu kuridhia Itifaki hii kwa sababu tumekwisharidhia Mkataba ambao

ndio msingi wa Itifaki hii. Aidha, ni ukweli kwamba wanawake wa kiafrika wamekuwa wakinyimwa haki zao za msingi sanjari na nafasi yao kutotambulika katika jamii. Hivyo basi, Itifaki hii ina lengo la kusaidia kutambua na kulinda haki za wanawake dhidi ya unyanyasaji na ubaguzi wa aina zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Itifaki hii imezingatia masuala yafuatayo:-

(a) Kuzuia na kuondoa unyanyasaji, udhalilishaji na ubaguzi dhidi ya wanawake;

(b) Kupinga mila mbaya hasa zinazopingana na haki za binadamu kama vile ukeketaji na kurithi wajane;

(c) Kuwepo na haki sawa kati ya wanandoa, mfano, kutolazimishwa kuoa/kuolewa, umri wa kuolewa uwe miaka 18 au zaidi na mali za wanandoa kugawanywa kwa usawa pale ndoa inapovunjika;

(d) Kuwepo na hatua za makusudi za kuweka nafasi sawa katika ngazi zote za uongozi na maamuzi;

(e) Kuwepo na ulinzi kijamii, kisheria na katika mipango yote ya kimaendeleo kwa wanawake wakimbizi na walio katika migogoro ya kivita;

(f) Wanawake na hasa watoto wa kike kupewa nafasi sawa za elimu shuleni, mitaala kutokuwa na lugha ya kibaguzi wa kijinsia ili kuleta uwiano mzuri wa kijinsia;

(g) Wanawake wajengewe uwezo kiuchumi ili waweze kufanya kazi mbalimbali hususan katika sekta binafsi; na

(h) Nchi zihakikishe kuwa haki mbalimbali za wanawake zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kusoma Azimio kama ifuatavyo:-

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifiki ya Nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Africa *[The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of Women in Africa]***

KWA KUWA; nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (A.U) mwaka 1982 zilipitisha Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu ambao Tanzania iliweka saini mwaka 1982 na kisha kuuridhia mwaka 1984;

NA KWA KUWA; Umoja wa Afrika katika kikao cha nchi wanachama kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 5 Machi,2003 ulipitisha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika;

NA KWA KUWA; Itifaki hiyo inakusudia kuongeza mambo muhimu katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika kama nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilivyokubaliana;

NA KWA KUWA; lengo kuu la Itifaki hiyo ni kuongeza vipengele vya kuzuia na kuondoa unyanyanyasaji, udhalilishwaji na ubaguzi dhidi ya wanawake; kupinga mila mbaya hasa zinazopingana na Haki za Binadamu kama vile ukeketaji na kurithi wajane; kuwepo na haki sawa kati ya wanandoa, kama kuoa au kuolewa; kuweka umri wa kuolewa kuwa si chini ya miaka 18; kugawanya mali za wanandoa kwa usawa linganishi; kuwepo na hatua za makusudi za kutoa nafasi sawa katika ngazi zote za uongozi na maamuzi; kuwepo na ulinzi kijamii, kisheria na katika mipango yote ya kimaendeleo kwa wanawake wakimbizi na walio katika migogoro ya kivita; kuwapa wanawake na hasa watoto wa kike nafasi sawa za elimu na ulinzi mashuleni; kuweka mitaala yenye lugha isiyobagua jinsia moja ili kujenga uwiano mzuri wa kijinsia na kuwajengea wanawake uwezo kiuchumi;

NA KWA KUWA; katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 25 Oktoba, 2006 Baraza la Mawaziri liliazimia kuridhiwa kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Wanawake wa Afrika;

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii na manufaa ambayo Tanzania itapata kwa kuuridhia, Bunge hili katika Mkutano wa Sita na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka, 1977, Sura ya pili, linaazimia kwamba Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Wanawake wa Afrika *(Optional Protocol to the African Charter on Human and People's Rights on the Rights of Women in Africa),* iridhiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JOHN P. LWANJI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala

kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu Kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika *(The Protocol to the African Charter on Human and People's Rights on the Rights of Women in Africa, 2003).*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha kwa niaba ya Kamati na Mwenyekiti kuwasilisha salamu za rambirambi kwa Serikali, Wabunge na familia ya Marehemu ndugu yetu Juma Jamaldin Akukweti aliyetutoka. Wakati huohuo pia ningeomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Pia nichukue nafasi hii kupongeza uteuzi wa Mheshimiwa Dr, Batlida Salha Burian, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudance Kayombo. Kamati inawaahidi ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, niendelee kuwasilisha maoni ya Kamati. Kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Bunge, uliipatia Kamati yangu kazi ya kujadili Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2006 (*The Written Laws (Miscellaneous (Amendment) (No.2) Bill, 2006)* likiwemo Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika kama nilivyolitaja awali.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuthibitishia kuwa, Kamati yangu ilitekeleza kazi hii tarehe 15 – 16 Januari, 2007 katika vikao vyake vilivyofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu azma ya kuwasilisha Azimio hili Bungeni. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa masuala ya haki za binadamu na haki za wanawake kwa ujumla yamepewa kipaumbele katika sehemu mbalimbali duniani, Kamati yangu inaafiki kuwa huu ni wakati muafaka wa kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo, ningependa nigusie maeneo machache yaliyojitokeza wakati wa kujadili Itifaki hii. Kama alivyoeleza mtoa hoja, pamoja na mambo mengine, Itifaki hii ina lengo la kutambua na kulinda haki za wanawake, kuzuia na kulinda unyanyasaji, kupinga mila mbaya na kushughulikia mali za wanandoa.

Katika maeneo haya, Kamati ilijadili kwa kina kuwepo kwa mila za makabila mbalimbali nchini Tanzania zikiwemo mila zinazoruhusu upande wa kike *(matrimonial)* kuwa na kauli katika urithi, watoto na kadhalika.

Aidha, Kamati ilitafakari juu ya taratibu za mirathi zilizopo katika baadhi ya dini kama ya Kiislamu ambayo imefafanua bayana utaratibu wa ndoa na mirathi ulivyo. Pia Kamati ilieleza wasiwasi wake juu ya kutokamilika kwa tafiti mbalimbali zilizofanywa na asasi zisizo za Kiserikali kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali kuhusu upungufu uliopo katika sheria za ndoa, mirathi na kutokuwepo kwa sheria ya ukeketaji.

Kamati iliona kuwa pamoja na nia nzuri ya Itifaki hii, kama mambo haya hayatashughulikiwa kikamilifu, utekelezaji wa Itifaki hii utakabiliwa na vikwazo. Hivyo, pamoja na ufafanuzi na ahadi iliyotolewa na Serikali kuwa inayashughulikia kikamilifu masuala hayo, Kamati inasisitiza kuwa Serikali izingatie matakwa yaliyoelezwa katika Protokali ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika, ikiwemo haki ya kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa chakula bora na cha kutosha kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 15 ya Protokali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari haya ndiyo yalikuwa maoni ya jumla ya Kamati yangu wakati ilipojadili Itifaki hii. Kama nilivyosema hapo mwanzo masuala ya haki za binadamu ni mojawapo ya ajenda muhimu zilizopewa kipaumbele duniani. Kwa sababu hiyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lilipokee Azimio hili na kulipitisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake kuwasilisha vyema Azimio hili mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao mizuri iliyoboresha Itifaki hii kufikia hatua inayoonekana. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Athumani S. Janguo - Mjumbe, Mheshimiwa Rajab H. Juma - Mjumbe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Mjumbe, Mheshimiwa Charles N. Keenja - Mjumbe, Mheshimiwa John P. Lwanji - Mjumbe, Mheshimiwa Fatma Maghimbi - Mjumbe na Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno - Mjumbe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Halima J. Mdee - Mjumbe, Mheshimiwa - Nimrod E. Mkono - Mjumbe, Mheshimiwa Salim Y. Mohammed - Mjumbe, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu - Mjumbe, Mheshimiwa Dk. Wilbrod Slaa - Mjumbe, Mheshimiwa Stephen Galinoma - Mjumbe na Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mjumbe. *(Makofi)*

Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Kamati, Ndugu Emanuel Mpanda, Ernest Zulu na Charles Mloka, kwa kuihudumia vyema Kamati wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI , OFISI YA RAIS UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifiki ya Nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Africa *[The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of Women in Africa]*

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote kwanza, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Micheweni natoa rambirambi kwa ndugu, jamaa wa Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti, pamoja na Marehemu wote waliofariki katika ajali ya ndege iliyotokea Mkoani Mbeya. Mwenyezi Mungu awalinde katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5) (b) (c) na 70(2) Toleo la 2004, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio laBunge kama nilivyolitaja hapo juu. Kabla sijatoa maoni hayo, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Bernad Membe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa William Ngeleja.

Mheshimiwa Spika, Katika Tanzania, sheria ya ndoa inayotumika hadi hivi sasa ni sheria ya ndoa Na.15 ya mwaka 1971. Kabla ya hapo kulikuwa na sheria mbalimbali za ndoa kwa ajili ya watu mbalimbali kutegemea rangi, dini, utamaduni mila au hali ya mtu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sheria hizo pia ziliwanyima kabisa sauti wanawake na kufanya maslahi yao kutokuwa na ulinzi wowote kisheria. Kwa mfano katika ndoa za kimila, mwanamke hakuwa na uhuru wa kuchagua mchumba anayempenda. Wazazi ndio waliokuwa na sauti juu ya mume gani amwoe binti yao. Haya yote yanahusisha ni umri gani, kila tamaduni inatambua umri kwa mtu kuoa au kuolewa. Hii kwa ujumla wake inatambuliwa kama ndoa za kimila ambazo mpaka sasa Serikali inazitambua kuwa ni ndoa kamili na zinatambulika kisheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Sita ya Azimio hili inaeleza bayana kuwa muda unaotakiwa kwa mwanamke kuolewa usiwe chini ya miaka 18. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie sheria zote zinazokinzana na kifungu hiki ikiwa ni pamoja na kuangalia utamaduni wa mila mbalimbali hapa kwetu zinazokwenda kinyume na azimio hili lakini bila kuathiri taratibu nyingine za kidini na kimila kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Saba ya Azimio hili inayohusu kutengana na kuachana katika vifungu vyote yaani (a)-(d) havielezi pindi mmoja wa wanandoa

akitaka kuvunja ndoa bila mwenzake kuridhia, kwa sababu ya kupata au kutokuwa mwaminifu kwa mwenzake na ikatokea mali nyingi ni za yule asiyetaka kuvunjika kwa ndoa hiyo na hawajapata mtoto katika ndoa yao. Kambi ya Upinzani inataka maelezo katika hili.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inayohusu haki ya usalama wa chakula, katika kifungu cha (a) cha ibara hiyo kinachotaka wanawake wawezeshwe kupata maji safi na nishati kwa ajili ya matumizi majumbani. Kambi ya Upinzani inakiona kifungu hiki kuwa ni bora Serikali ikakiwekea mkazo zaidi ili kuondoa uwezekano wa maeneo mengi ya nchi yetu kugeuka jangwa kutokana na matumizi makubwa ya miti kuwa nishati kwa matumizi ya nyumbani kitu kinachoharibu vyanzo vya maji.

Aidha, zaidi ya hapo bado wakinamama wanaoishi Mijini wanakosa maji safi na nishati kwa ajili ya matumizi majumbani kutokana na sababu ambazo Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Serikali haina mipango mizuri na dhamira ya dhati ya kuwaondolea wakinamama tatizo la nishati na maji safi.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilihakikishie Bunge hili kuwa imeweka mikakati mahsusi ya kuhakikisha ibara ya 15 (a) inatimizwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, Kambi ya Upinzani haina tatizo na Azimio hili, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuweza kuchangia Azimio hili ambalo limekuja kwa wakati wake. Lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba nami niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa pole kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Waziri wetu na pia wataalamu wote waliopata ajali na kufariki katika ajali hiyo, naomba familia zao Mungu awape nguvu za kuweza kuvumilia msiba huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Iringa kumpongeza Mheshimiwa Asha Rose Migirio kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kuweka historia katika nchi yetu na katika Bara la Afrika na kwa wakati huu tunaporidhia Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Batlida Buriani kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Bunge na kuwa *Chief Whip* wa pili mwanamke katika Bunge la Jamhuri ya Muungano baada ya *Chief Whip* mwanamke wa kwanza Mheshimiwa Anna Makinda. *(Makofi)*

Naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Ngeleja, na Mheshimiwa Kayombo kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa Manaibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kwanza niunge mkono kuridhia Itifaki hii na naunga mkono kwa sababu Azimio hili limekuja wakati ambao ni muafaka, wakati ambao nchi yetu inapitia sheria mbalimbali ambazo zinahusu mwanamke na ambazo zimepitwa na wakati. Kwa maana hiyo ni kwamba, kwa kuridhia Azimio hili itakuwa imesaidia kuharakisha nchi yetu kuweza kuzipitia sheria nyingi ambazo tumekuwa tunazipigia kelele kwamba zirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiangalia suala la katika *article* ya 21 inayozungumzia masuala ya kugawa mgao wakati wa urithi, kati ya watoto wa kike na watoto wa kiume. Ni kweli kwamba kuwepo na tatizo la mgao hasa wazazi wanapofariki, watoto wa kiume kupewa mgao na watoto wa kike kutopewa mgao kwa sababu tu ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuweko Itifaki hii itatusaidia kuhakikisha kwamba mambo yote haya yanaangaliwa na kuweza kuhakikisha kwamba watoto wote wanapewa haki sawa ikiwa ni haki pia ya kurithi mali ambazo zimeachwa na wazazi wao. Hii pia inaangaliwa katika *article* ya 22 ambayo inazungumzia ulinzi maalumu kwa wanawake wazee.

Mheshimiwa Spika, wanawake wazee, wote tunaelewa hapa nchini wamekuwa wanauwawa sana hasa katika Mkoa wa Shinyanga na Mikoa mingine kwa sababu tu ya kuwa na umri mkubwa na kuwa na macho mekundu, bila kuangalia kwamba labda macho mekundu yameletwa kwa sababu ya uduni wa nishati ambazo tunatumia ikiwa ni pamoja na nishati ya kuni ambayo ni moshi unaowaharibu akina mama. Lakini, badala yake wanatuhumiwa kwamba ni wachawi na kuuwawa. Kwa maana hiyo, kwa kuridhia Itifaki hii, itatusaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wanawake pia wamekuwa wanauwawa kwa imani za kishirikina, wengine wanawauwa labda wakifikiri watapata utajiri. Kwa hiyo, hii itatusaidia kuwalinda wanawake wazee.

Mheshimiwa Spika, lingine pia kwenye hiyo hiyo *Article* ya 22, ni suala la wanawake wazee kuwa waangaliwe kwa uangalifu na kulindwa na kuthaminiwa. Tunaelewa kwamba wanawake wazee wametoa mchango mkubwa sana. Sasa hivi tunavyozungumzia, watoto wenye shida na watoto yatima wote wako mikononi mwa wazee.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wako mikononi mwa wanawake wazee bila kuwa na rasilimali na bila kuangaliwa. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba Wizara husika baada ya kuridhia hii itifaki itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na *safety net* za kuwaangalia hawa wazee wanaotunza watoto.

Lakini pia kwenye maeneo mengine kuhakikisha kwamba zinakuwepo kambi za wazee ambapo wazee hawa wanaweza kulindwa ili wasiweze kuuwawa na pia kupewa matibabu yanayostahili. Wamekuwa wakipata matibabu, lakini wanapokwenda hospitali mara nyingine huduma ni duni, hawana fedha za kunua dawa na wanaugulia nyumbani.

Lakini wakati mwingine kwa ajili ya kulea watoto wenye shida, wanaamua wao kuwatibu watoto na wenyewe wanabaki bila matibabu. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba Wizara italiangalia hili baada ya kuwa tumeridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopenda kulizungumzia ni suala la usafirishaji wa wanawake na wasichana ambalo hili ni *trafficking* ya wasichana na wanawake. Biashara hii ambayo imeshamiri katika nchi mbali mbali Duniani na mpaka imekuja kufika hapa nchini kwetu. Tunaelewa watoto wetu wanahamishwa kutoka sehemu mbali mbali na kuna Mikoa ambayo kabisa inajulikana kwamba yenyewe ndiyo inayotoa watoto bora kwa ajili ya kutumikishwa. Kwa hiyo, kwa kuridhia Itifaki hii, itatusaidia kuhakikisha kwamba watoto wetu wanalindwa. Watoto wanasafirishwa, wananyanyasika na tunasoma hata kwenye magazeti yakielezea kwamba watoto wanasafirishwa kwa makontena kupitishwa mipakani na kupelekwa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kuridhia Itifaki hii kutaisaidia pia Wizara kuhakikisha kwamba kunakuwa na utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba wale wote wanaohusika na vitendo vya kusafirisha hawa watoto wanachukuliwa hatua, lakini wale watoto ambao wameathirika kutokana na kuingizwa kwenye hii biashara, pia wanapewa *rehabilitation* ambayo inafaa kuweza kuhakikisha kwamba wanakuwa raia wema na wanapewa nyenzo za kuweza kujipatia kipato kwa sababu wakati mwingine wanasafirishwa kwa kudanganywa kwamba watapewa ajira bora. Kwa hiyo wale wanaorudishwa, wanatakiwa pia wapewe ajira au miradi ya kiuchumi ambayo itawawezesha kuweza kupata mahitaji yao ya kila siku. Hii ni pamoja na wahusika wale wanaowakusanya hawa watoto.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam watoto wengi wamewekwa kwenye madanguro na wakati mwingine ukisoma magazeti, yanatangaza kwamba wale watu wote wanaotaka watoto wafanyakazi wa ndani ya nyumba, sisi tuna watoto. Sasa, sielewi Serikali kama huwa inachunguza hawa wote ambao wanawakusanya watoto halafu wanawatafutia ajira. Kwa kwa kuridhia hii, itatusaidia pia kuweza kuweka utaratibu mzuri wa kuyashughulikia haya masuala.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja na ninaomba liridhiwe na nchi nyingi upesi ili liweze kukubalika kwenye *AU* na kuweza kutumika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika kuunga mkono Itifaki hii ambayo imeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi naomba niungane na wenzangu wote ambao wametoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais pamoja na familia husika waliofiwa kwenye ajali ya ndege akiwemo Waziri wa Nchi Masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma Akukweti. Vile vile, na mimi kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa

Pwani, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kabisa, tumefurahishwa sana na uteuzi wa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kuwa Naibu Katibu Mkuu wa *UN*. Hali kadhalika, wale wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi za Uwaziri na Naibu Waziri katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, mimi nasema Itifaki hii imekuja wakati muafaka. Sisi Watanzania tunakwenda na wakati. Nafikiri mengi yaliyoelezwa humu ndani baadhi tayari tumeishayapitia na yanatekelezwa na Serikali yetu. Lakini bado kuna mengine, naona kuna haja ya kuyasukuma zaidi kwa sababu hii Itifaki inaendana na sheria ya nchi yetu, nikianzia na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 - baadhi ya Wabunge wengine mwaka huo ndio wamezaliwa, wamo humu ndani. Sheria hiyo bado iko pale pale. Humu ndani Itifaki inasema Ndoa isifungwe, bali iwe na mtu ambaye yuko katika umri wa miaka 18. Lakini sheria yetu bado iko inafanyiwa marekebisho, sijui itaisha lini. Vinginevyo tutakuwa hatuendi na wakati.

Mheshimiwa Spika, sheria ya mwaka 1971, umri wa mtoto unaleta mkanganyiko. Kwenye kupiga kura, inazungumzia miaka 18, lakini kwenye ndoa inazungmzia miaka 14/16. Sasa, hii ni mapungufu. Vinginevyo hii Itifaki hata tukiiridhia, hatutakuwa tunakwenda na wakati, badala yake tutakuwa tunaendeleza ule unyanyasaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema hili tatizo la sheria hii, Wizara husika ifanye jitihada za hali ya juu, sheria hii itoke haraka sana, aidha, iendane sambamba na kuridhiwa kwa Mkataba huu au isichukue muda mrefu ili na sisi tuweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Ibara ya 15 ya Itifaki hii inazungumzia suala la Chakula bora na cha kutosha kwa wanawake, hali kadhalika bila kusahau maji safi na salama. Hapa tatizo linakuja, mwanamke ndiye mkulima mkuu.

Sijui Serikali yetu itaweka mikakati gani ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Vijijini. Mpaka sasa hivi, wao ndio wanaoteseka. Kilimo duni, hali duni, zana duni, matokeo yake ndiyo waathirika wakuu. Hata hicho chakula chenyewe wanacholima, akikipata, akifika nyumbani, yeye jukumu lake kubwa ni kukipika na kukipakua, lakini hata anapokula anakuwa bado ana mawazo, anasubiriwa akalete mzigo wa kuni, anasubiriwa akachote maji, anasubiriwa akafanye vitu vingi. Sasa, unakuta hata huu Mkataba tukisema tunaridhia lakini bado tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukawasaidia hawa akina mama hasa hawa wakulima wakuu wa huko Kijijini.

Mheshimiwa Spika, pia Itifaki hii imezungumzia suala la kuwezesha kwenye bajeti. Mimi hapa ninazungumza kitu kimoja. Tulipokuwa kwenye kipindi cha bajeti, hakuna Wizara ambayo imepata fungu dogo zaidi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, hii Wizara ndiyo Mhimili Mkuu katika Taifa. Ninaposema mhimili mkuu kwa maana ya kwamba wanawake wamo humo, wanaume wamo humo, vijana hata kama hawakutajwa lakini na wenyewe wamo katika Wizara hii. Lakini sasa Wizara hii ndiyo inayopaswa iwezeshwe sana.

Humu kwenye Itifaki inazungumzia elimu itolewe kwa mapana. Mtu wa kutoa hii elimu ni hii Wizara. Wizara yenyewe bajeti yake ndogo, itawafikiaje hawa wananchi huko Vijijini ili waweze kuielewa, waelewe hii Itifaki na ikawalinda na hasa hawa wanawake tunaowazungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kwa makini, itupie macho Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Hii ndiyo Wizara ambayo inatakiwa iwezeshwe. Hii Wizara ikiwezeshwa itapeleka elimu huko hata zile mila ambazo zimepitwa na wakati zitapungua.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la watoto kuolewa kabla ya umri wao, mimba za utotoni, hawa ndiyo watu wanaopaswa kupeleka elimu kwa kutumia wafanyakazi wao waliokuwa katika Wizara ile. Kwa hiyo, mimi nasema ili tuweze kwenda sambamba na hii Itifaki, haya mambo ni muhimu tuyazingatie.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, tunapozungumzia elimu, tuangalie kuanzia ngazi ya Chekechea. Mtoto wa kike anapoanza elimu, kuna mazingira ya aina tofauti, kuna mazingira ambayo yanamlinda mtoto wa kike na kuna mazingira ambayo mtoto wa kike hayawezi kumlinda. Tunapozungumzia suala la majengo ya shule zetu, tuangalie majengo yale na vyoo viende sambamba kwa sababu mahitaji ya mtoto wa kike ni tofauti na mahitaji ya mtoto wa kiume katika maeneo tunayoishi, hata kwenye mashule, hata kwenye maofisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba suala hili la Itifaki hii liangaliwe kwa makini. Baada ya kusema hayo, naomba na mimi niunge mkono, lakini nasisitiza tena kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii iangaliwe, iongezewe bajeti yake na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 irekebishwe kwa sababu mwanamke ndiye anayebeba mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii mtoto analelewa kwa Shilingi mia moja. Wewe mtoto ukimpa Shilingi mia moja tu, nenda nayo shule hii, anakutizama mara tatu kuanzia chini mpaka juu. Ni dhahiri haimtoshi hata nauli ya daladala, ndiyo maana ananyanyaswa. Sasa, leo mama anapewa Shilingi mia ndiyo amtunze mtoto! Kwa kweli hapa kuna haja twende na wakati. Kama tunakwenda na nguvu mpya, ari mpya, kasi mpya, basi na sheria zetu na tuziangalie ili tuweze kwenda na Itifaki tunazoridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi hii nichangie hili Azimio lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hili Azimio, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole sana kwa Familia ya Mbunge Mwenzetu, Marehemu Akukweti aliyefariki mwaka huu. Natoa pole kwa familia pamoja na familia nyingine ambazo ndugu zao walipoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kwa kazi nzuri aliyowaonyesha Watanzania na kwa kuwa Katibu Mkuu huyo amemwona Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro ana uwezo, ni kutokana na nchi yetu kumwezesha kumpa nafasi hiyo ya Mambo ya Nje. Hilo naomba nafasi hii kusema kwamba wanawake tuna uwezo na uwezo huo umedhihirika wazi.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpa pongezi sana Mheshimiwa Dr. Buriani kwa kuchukua nafasi nzuri ya kuwa Waziri kutoka kwenye Unaibu Waziri. Hongera sana wifi yangu.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Kayombo na Mheshimiwa Ngeleja kwa kupewa nafasi hiyo ya kushika nafasi ya Unaibu Waziri. Mheshimiwa Kayombo ni Naibu Waziri Mipango na Uwezeshaji na Mheshimiwa Ngeleja, Naibu Waziri Nishati na Madini pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje - Mheshimiwa Membe kwa kuchukua nafasi ya Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nimesikitika. Nilitegemea Rais wetu baada ya kutoka mama, angeingia mama. Lakini yote kheri, tunategemea huko baadaye anaweza akatutolea Mheshimiwa Membe akawekwa nafasi nyingine, siyo kutolewa kwenye *System*, hiyo nafasi akapewa mwanamke. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono Azimio lililoko mbele yetu kabla sijasahau nikiendelea mbele. Lakini, Azimio hili lisiwe tu kumlinda mwanamke, naomba lijulikane kuwa ni kutoa haki kwa wanawake huko tunakokwenda, sio kumlinda mwanamke.

Mheshimiwa Spika, nalizungumzia hili la kukataa kwamba kumlinda mwanamke, bali ni kutoa haki kwa mwanamke, kwa sababu tukiangalia mila potofu ambazo zilikuwa zikimgandamiza mwanamke ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu, huko nyuma wanawake walikuwa hawapewi nafasi sawa katika kupewa elimu. Mwanamke alikuwa anaambiwa kachunge ng'ombe, mtoto wa kiume anakwenda Shule. Lakini sasa Azimio hili ambalo linampa haki mwanamke naye apewe haki sawa linaonyesha sasa wameliona hili ni wajibu wa mwanamke apewe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine limethibitishwa leo. Mmetenda haki kuwaleta vijana wa Darasa la Saba wasichana watatu na wavulana watatu. Hii inaonyesha kwamba na wasichana sasa wameishaanza kuwekwa katika usawa wa kusomeshwa ukiendana sambamba na nafasi za wavulana. Hilo nalipongeza sana. Serikali yetu ya Tanzania imeliona hili kwa makini kwamba watoto wa kike walikuwa wameachwa nyuma katika suala la elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye *Article* Na. 9, haki ya mwanamke katika maamuzi, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba wanawake walikuwa wameachwa katika maamuzi ya uongozi/utendaji. Lakini, nashukuru katika nchi yetu ya Tanzania Rais wetu ametuwezesha wanawake, kwa kweli ninasema kwa moyo wangu mkunjufu kwamba ametujali wanawake katika uchaguzi uliofanywa mwaka 2006 kutuonesha wazi kwamba ametupa Mawaziri wengi wanawake, Manaibu Waziri wengi tu wanawake, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, wanawake wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado nafikiri hii Itifaki ikipita zaidi itazingatia sana kuongeza juhudi ya kuongeza uwingi wa wanawake katika kutoa nafasi katika maamuzi ya uongozi kwenye Majimbo. Wanawake tutakapojitokeza kwenye Majimbo, wasituone kwamba hatuna uwezo wa kugombea. Uwezo huo tunao na tunasubiri mwaka 2010, tutaingia kule kwenye Majimbo. Kwa hiyo, wananchi waone na sisi wanawake uwezo huo tunao.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, haki katika ndoa. Nimeshukuru sana Itifaki hii imeeleza katika *Article* Na. 6. Kwa kweli mabinti zetu huko nyuma kuna makabila ambayo binti chini ya miaka 18 alikuwa akilazimishwa tu kuolewa, hana maamuzi ya kukataa. Wazazi wakishakaa, wakiamua huyu ndiko ana miaka 9, ana miaka 10 anapelekwa kwa mwanaume na mbaya zaidi wanaolewa na wazee. Lakini sasa hii Itifaki imenifurahisha sana, nikasema angalau basi mwanamke atakapopewa miaka hii chini ya miaka 18 atakuwa na maamuzi yake ambayo na yeye atatoa maamuzi yake ambayo na yeye atatoa ushauri wake kwa wazazi wake ili aweze na yeye kwenye ndoa yake aende kwa maamuzi aliyoyatoa mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni akina mama katika mgawanyo wa kazi. Kuna makabila mengine huko, bado hawajazingatia. Mwanamke anaambiwa yeye ni mtu wa kulima, baba halimi, mama ni wa kubeba mtoto tu mgongoni, baba hamsaidii kubeba mtoto.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa Itifaki hii tukiipitisha, naona basi akina baba na wenyewe wataona umuhimu wa kuchangia katika kazi za binadamu wanazozifanya wote. Kama wote tulime, tulime. Mbaya, zaidi wanawake walikuwa wanalima lakini akishaivisha yale mazao, hana haki tena ya kuyapangia ndani ya familia, anaamuliwa na mzee ambaye yeye alikuwa haendi hata shamba. Basi kama Itifaki hii itapitishwa, itawasaidia akina mama kwenye makabila ambayo walikuwa wakinyanyaswa kiasi hiki na wenyewe basi wakachangia mawazo yao katika kuhakikisha mgawanyo wa mali zao walizonazo ndani ya nyumba wanazipanga wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, lingine, kwa sababu Itifaki hii imeandikwa kwa Kiingereza na wanawake wengi wako Vijijini, hawajui haki zao hao akina mama huko waliko, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii anayehusika na hii Itifaki, atusaidie sana baada ya kuiridhia na nchi nyingine, mtusaidie kuhakikisha kwamba tunatoa nakala nyingi tuzisambaze kwa akina mama huko Vijijini ili na wenyewe waelewe kwamba ni nini Serikali yao au nchi zao zinasemaje kuhusu haki ya akina mama. Basi nimwombe tu wazitengeneze vizuri kwa lugha ya Kiswahili au lugha nyepesi ambayo inaweza na

wenyewe akina mama wakachangia kujadili katika maeneo yao tukiwahimiza wajiunge pamoja kwenye *SACCOS* ili wajiendeshe kupunguza umaskini, lakini wakiwa wanaendelea na kujadili haki zao wanazostahili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mimi yangu yalikuwa ni machache hayo na naomba turidhie haraka sana ili tuweze kuwakomboa akina mama. Ahsante sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, ahsante sana! Nadhani sasa kwa niaba ya wanaume, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir Atusaidie.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kama walivyochukua wenzangu ya kutoa pole kwa familia ya mwenzetu Mheshimiwa Akukweti. Kama tunavyosema katika dini mbalimbali, wawe na moyo wa subira na hiyo ni amri ya Mwenyewe *Subhna-huwa-taala*.

Mheshimiwa Spika, la pili, nitoe hongera kwa wale wote ambao wamepata nyadhifa mbalimbali ambao wameshatajwa, sina haja ya kurudia. Lakini kama kawaida lazima tuchukue nafasi hii kuwapongeza wenzetu mbalimbali waliopata nyadhifa na vile vile tuwatakie kila la kheri katika shughuli hizo, waweze kutuwakilisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine, mimi niseme kama walivyosema wenzangu kwamba naliridhia Azimio hili na hasa tukitilia maanani kwamba wengi walitajwa hapa au mkazo zaidi umetiwa kwa akina mama katika kupata haki zao, lakini pia watoto na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, mimi nirudi nyuma kidogo, labda Mheshimiwa Waziri baadaye atakuja kunisaidia. Azimio hili wakati tukiletewa hapa Bungeni, nilikuwa nikitarajia baadhi ya mambo ambayo yamefanyika zamani na watoto wengi ambao baadhi yao wazee wetu na wengine sisi tumerithi. Wazee hao walikumbwa na mikasa mbalimbali ya kusafirishwa na kwenda nchi za nje na kupata madhira mbalimbali. Hivi Azimio hili linatueleza nini katika hilo? Sisi kama Watanzania, basi wale ambao wamekumbwa na mambo kama hayo wana wajibu wa kufanyiwa nini? Labda Mheshimiwa Waziri baadaye aje atusaidie.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu hivi sasa tumekuwa tukizungumza madhira mengi ambayo yanawapata akina mama na watoto hapa. Lakini kuna mambo yamefanyika hapo zamani ambapo yalikuwa yanataka yazingatiwe na yawekewe mikakati ili kwa bahati mbaya labda yasirudie tena na tuna hakika hayatorudi lakini: Je, wale waliokumbwa na mambo hayo wako vipi?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine limezungumzwa hapa suala la kuwalinda watoto na zaidi tunasema kwamba tunalinda watoto hasa katika ukeketaji, kuwapa haki zao na mambo kama hayo. Hili somo limekuwa likisemwa kila siku, elimu imekuwa ikitolewa.

Nami nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa elimu kwa hata wale wataalam waliokuwa wanakeketa hawa vijana, kwamba hivi sasa wameelekea kulifahamu hili suala kwamba ni baya na wengine wamefika pahali kujitokeza hadharani kusema kwamba kweli nimekubali kwamba ni baya na wanaliacha.

Mheshimiwa Spika, lakini, bado naendelea kuiomba Serikali pamoja na Wizara iendelee kutoa elimu kwa wale waliobakia, maana bado wapo na wengine wanafanya kinyemela. Sasa tufike pahali tuone kwamba suala hili limemalizika.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati tukizungumza suala la ukeketaji, Mheshimiwa Waziri wakati analeta Azimio hili, ameangalia vipi kuhusu hawa akina mama walioanzisha mtindo wa kuchukua watoto wadogo wa kike na wakawa wanawauza? Wanawauza kimwili na wanawauza kwa mambo mengine. Analifikiria nini hili? Hivi hatuoni sasa hivi kwamba kuna haja ya kuchukua hatua maalum kwa watu kama hawa?

Maana sasa hivi kuna mtindo umezuka, kuna mtu anaweza kwenda Mkoani akasema ninamtaka mtoto kwa ajili akafanye kazi, nataka watoto hawa tukawaweke katika kambi za haki za binadamu au tukawaweke katika kuwatunza watoto hawa. Lakini matokeo yake utakuta mtu yule anawauza watoto wale. Huu ni udhalilishaji. Lakini Serikali imelinyamazia kimya suala hili. Sasa hili tunalisemea nini katika Azimio hili? Lakini bado ninaomba Serikali ichukue hatua na sasa hivi ni wakati muafaka hasa wa kuzuia mtindo huu ukome.

Mheshimiwa Spika, kule Uwanja wa Fisi, Dar es Salaam kulifanyika tendo ambalo mimi naipongeza sana Serikali hii. Kwa kweli hivi sasa mambo yamekaa vizuri, udhalilishaji kule haupo na kama utarudi, basi utarudi kwa mlango wa nyuma sana. Lakini tusiachie au tukalegeza kamba, tukaondoka Uwanja wa Fisi, tukapata pengine, kwenye Azimio hili bado tutakuwa hatujafanya kitu. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri na hili aliangalie ili aweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, hapa tumezungumzia sana zaidi haki ya wanawake. Wakati tunalipokea Azimio hili, mimi nilikuwa naangalia angalia hapa. Mimi nakubali wanawake wapewe haki na wengine hapa wamezungumzia hata kufikia pahali pa kusema kwamba mgawo wa mali uwe sawasawa baina ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume, wameshafika kusema hivyo.

Lakini, mimi nilikuwa napekuapekua katika hizi karatasi nilikuwa naangalia zaidi haki na wajibu ni watoto pacha. Lakini haki na wajibu, haki na uhuru wa kuabudu, hali kadhalika ni watoto pacha.

Mheshimiwa Spika, nakubali sana. Narudia tena kusema wanawake wapewe haki. Lakini pia wanawake wapewe haki pale walipoona kwamba yuko tayari kutekeleza dini yake inamwambia nini katika kugawa mali.

Narudia tena. Mwanamke apewe haki kama tunavyotaka, lakini bado vile vile apewe haki pale anapoona yeye binafsi, uaminifu wake katika dini yake unamkubali au anakubali mwenyewe kwamba kama imesema *Quran* mali igawiwe katika kifungu kadha kadha, basi mwanamke huyo apewe haki na akubaliwe kwamba afuate hivyo anavyotaka kwa sababu katika Azimio hili, hili Mheshimiwa Waziri kaliepuka hili.

Sasa, tusielee sana kwenye demokrasia. Tukielemea sana kwenye demokrasia tutafika mahali tuingie kwenye mzozo. Tutafika mahali siku moja tuone wanawake wale wanaovaa ninja , watupu mtaani wanaandamana! Kwa sababu wamenyimwa haki yao na uaminifu wao katika dini yao. Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu hili? Narudia tena, wanawake wapewe haki na nakubali na wale ambao wamesema kwamba mwanamke na mwanamme wagawiwe haki sawa na alipokufa baba, basi kutolewe na maelezo kwamba mtoto huyu apewe hiki, hiyo nakubali.

Mheshimiwa Spika, lakini narudia tena, Tanzania haina dini, Watanzania ni wenye dini. Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hili?

Kwa hiyo, naomba Azimio hili bado lituweke wazi. Tusielemee wanakotupeleka wenzetu kwamba kila mtu awe na haki, lakini basi tuwakubalie vile vile wale ambao wana utaratibu wao na huo sio utamaduni ninaozungumza mimi. Aha! Mimi nazungumzia dini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano dini yangu mie imeshaandika na imeishasema. Maana kwenye dini yetu ukisikia mwanamke haruhusiwi kusalisha, tena lisije Azimio siku moja mwanamke asalishe. Aha! Hasalishi! Maana ndiyo dini yangu ilivyosema. Hana ruhusa kukaa mbele, mwanamke kusalisha! Sasa na dini yangu vile vile inaniambia mie kwamba anapokufa baba-mtu au anapokufa mume-mtu, basi pana moja, mbili, tatu, ifuatwe!

Sasa, tunapofika pahali tukasema watu wagawane haki sawa, aha! Wanapofika wanawake wakasema na sisi tunataka haki yetu kwa mujibu wa dini yetu, waruhusiwe! Tusielemee moja kwa moja katika demokrasia. Demokrasia itatupeleka mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye demokrasia inayokubalika huko kimataifa, hiyo inakubalika. Lakini turudi pia katika hali ya ulimwengu ulivyotupeleka katika hali ya binadamu wanavyoishi na katika dini zetu mbalimbali zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono Azimio. Ahsante! *(Makofi)*

**SPIKA:** Katika orodha yangu, nimekaukiwa, kwa hiyo nawajibika kumwita mtoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kitendo cha Bunge lako Tukufu kuridhia Itifaki hii, ni ishara ya wazi kuwa Bunge linatambua haki,

nafasi, hadhi na mchango dhahiri wa wanawake katika Taifa letu. Bunge hili litakuwa limejijengea heshima kubwa sana kwa kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kauli au kwa maandishi na namna nyingine yoyote itifaki hii. Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kauli na wale ambao wamechangia kwa kuandika.

Napenda vile vile nichukue nafasi hii kuipongeza kwa moyo wa dhadi Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kupitia Itifaki hii na kwa maoni mazuri iliyotoa na hasa kwa kuunga mkono Itifaki hii. Kamati imejijengea heshima kubwa sana siyo tu kwa Bunge hili, kwa wanawake wa jamii nzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa John Paul Lwanji, kwa niaba ya Kamati kuwasilisha maoni ya Kamati na kuunga mkono Itifaki hii. Kwa umuhimu ule ule, ningependa vile vile kuishukuru na kuipongeza Kambi ya Upinzani, kwa kutoa maoni mazuri na kwa kuunga mkono Itifaki. Hii inaonyesha yanapokuja masuala muhimu kama ya kutetea haki ya watu wote hasa ya wanawake ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakinyimwa hii haki, hatuna tofauti, tofauti zetu ziko kwenye itikadi tu kwa hiyo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Iringa, yeye amesisitiza kwamba Itifaki hii sasa itasaidia sana katika kutoa msukumo katika kuangalia sheria zetu ambazo ni kandamizi na tutafanya hivyo kwa kadri tunavyoweza. Naye ameungwa mkono na wasemaji wale wengine Waheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Pwani. Vile vile Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Ninashukuru vile vile kupata mchango wa upande wa akina baba, ambao vile vile wameona umuhimu wa kuunga mkono Itifaki hii katika kutambua haki, nafasi, hadhi na wajibu wa wanawake. *(Makofi)*

Kuna Waheshimiwa Wabunge, ambao walitoa hoja/maoni yao kwa maandishi nao ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, nakushukuru sana kwa sababu katika maandishi haya naye ameunga mkono na ametuelekeza kule ambako tunapaswa sasa tutoe msisitizo na hasa katika kuangalia sheria hizi ambazo zimepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Janet Bina Kahama na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, nawashukuru wote kwa moyo wa dhati kwa sababu hakuna hata mmoja ambaye hajaunga mkono Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, kasema kwamba azimio hili litasaidia kusukuma Serikali kubadili sheria ambazo zimepitwa na wakati. Ameomba vile vile ulinzi maalum kwa ajili ya wanawake wazee hasa sehemu ambazo wakiona una macho mekundu basi badala ya kuwaenzi kwa kufanya kazi kwa nguvu na kuwa

wanapikia kuni, badala yake wanauwawa kwa ukatili. Serikali imejitahidi sana kutoa hamasa na kutoa ulinzi pale ambapo inawezekana na kwamba watoto wa kike wasibaguliwe wakati mali ya familia inapogawiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zaynab Vulu, naye ameongelea juu ya umri wa kuolewa na hili nalo linahitaji kuangaliwa katika sheria zetu na ameona kwamba tutoe elimu ya kutosha na elimu inayostahili kutoka ngazi ya chekechea mpaka ngazi ya juu.

Mheshimiwa Spika, yote ni ya kuunga mkono Itifaki. Lakini ningependa kusema tu kwamba kama alivyosisitiza Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, kuhusu *human traffic* au kwa namna yoyote ile pale wanawake wanapojikuta wako kwenye hali ambazo hazitakiwi basi Serikali kwa namna moja na Taifa kwa ujumla tutafanya kila linalowezekana kwa sheria na kwa kuona kwamba hamasa inaongezewa na elimu ili wanawake wasiendelee kupelekwa kule ambako hakutakiwi kwenda.

Lakini aliongelea vile vile uhuru wa dini, mimi ni moja wa watu ambao tunaheshimu dini na uhuru wa dini. Lakini suala la dini zaidi ni la mtu mwenyewe kwa sababu Serikali yetu ni *circular state* haina dini. Kwa hiyo, suala la dini ni la mtu mwenyewe imani yake na kwa hiyo uhuru huo tutawaachia wenyewe na hakuna Serikali ambayo itamwambia mtu kwa nini unakubali uamuzi wako utokane na imani yako ya dini bali hilo tutawaachia wananchi na uhuru wa dini yao. *(Makofi)*

Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba na mimi kwa sababu ya ukereketwa wangu niseme machache. Wanawake ndiyo wanaohifadhi, wanaoendeleza na kupitisha utamaduni na mila pamoja na taswira ya Waafrika kutoka kizazi hadi kizazi. Wanawake ndiyo wanaobeba mzigo wa umaskini katika nchi zetu. Sisi wote tunajua. Wanawake ndiyo walezi wa jamii. Hivyo basi kutambua na kuzingatia haki, hadhi, nafasi na mchango wa dhahiri wa wanawake kutaongeza ari yao ya kushiriki zaidi katika kuleta maendeleo, kuondoa umaskini na kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wote tunajua leo ukienda mashambani leo walio wengi ni wanawake. Kwa hiyo, wakisikia itifaki hii imepita nina hakika watalima zaidi na hapo hapo naomba Itifaki hii iwe changamoto kwa wanaume waweze kuungana na wanawake katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mzigo wa umaskini ni mzito hauwezi kubebwa na sehemu moja shuruti wote wawili tushirikiane.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na shukrani zangu za dhati kwako wewe na kwa Waheshimiwa Wabunge sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Katiba na Mambo ya Sheria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri iliyopo mbele yetu ni kuridhia Mkataba imekwishatolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake wa Afrika (The Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Rights of Women in Africa lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda uliopo hautoshi kuingia katika hatua nyingine ya shughuli za leo, naamua sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.36 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni.*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo *(Agreement Establishing the Africa Institute for the Environmentally Sound Management of Hazardous Wastes and Other Wastes, 2006)***

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo *(The Agreement Establishing the Africa Institute for the Environmentally Sound Management of Hazardous and other Wastes, 2004).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru *Rabuka* kwa kutuwezesha kuingia mwaka mpya na kufikia siku hii ya leo, sisi wapiga kura wetu na wananchi kwa ujumla.

Naungana na wenzangu walionitangulia kuzungumza kwa kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki ya wale wote waliofariki kutokana na ajali ya ndege iliyoanguka Mjini Mbeya Jumamosi tarehe 16 Desemba, 2006. Watu wa Mbeya tumeguswa sana na ajali hii kwani mbali na kwamba ilitokea Mbeya ndugu zetu hawa walikuwa kazini, baada ya kukagua soko maarufu la Mwanjelwa lililoungua tarehe 12 Desemba, 2006. Nawapa pole majeruhi nawaombea wapone haraka. Tunawapa pole vile vile wafanyabiashara wa soko la Mwanjelwa na wananchi wa Mbeya kwa janga hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, alikuwa ndugu yetu, mwenzetu na rafiki yetu. Tunampa pole Mheshimiwa Spika na hasa familia yake

na wananchi wa Tunduru. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azirehemu roho za marehemu wote mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii vile vile kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi za Uwaziri na Unaibu Waziri. Kwa njia ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira ambayo chini ya Uenyekiti wa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, ilijadili na kulikubali Azimio. Maoni na maagizo ya Kamati hii yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taka za sumu ni zile zenye madhara kwa binadamu na mazingira. Zinaweza kuwa ni taka ngumu, taka za majimaji au taka za gesi ambazo kutokana na asilia yake ya kibaolojia au kikemia zina madhara makubwa. Taka za sumu zina tabia zifuatazo, kuwaka zenyewe katika joto la nyuzi joto 60 Sentigredi, kulipuka, kuchuna vyuma au ngozi za viumbe hai, kusababisha madhara makubwa ya kiafya katika muda mfupi au muda mrefu zinaponywewa, kuvutwa kwa njia ya hewa au kugusana na mwili. Tabia nyingine ni kuleta maradhi ya kuambukiza na kudumu kwenye mazingira kwa muda mrefu na hivyo kusababisha madhara katika mifumo ya kiokolojia.

Mifano ya taka yenye tabia hizi ni kama vile dawa chakavu ya kilimo au kwa jina lingine viuatilifu yaani *pestsides,* taka ya vifaa vya *electronics* kama vile mabaki ya simu na kompyuta. Taka za viwanda zinazotengeneza betri, nguo na ngozi, taka za mafuta zenye kemikali au madini, *heavy metals* kutoka katika migodi au mafuta ya *transformer* zenye *plorical united by fenues* yaani *pcb.* Narudia kwamba mafuta ya *transformer* ni hatari sana na taka zinazotoka kwenye vituo vya afya. Madhara ya kiafya yanayoweza kutokea ni pamoja na magonjwa kama vile saratani, upungufu katika kukua kwa ubongo na madhara katika njia za uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko na madhumuni ya Mkataba. Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo ni moja ya vituo 13 vya mafunzo na kueneza teknolojia zinazolinda mazingira katika usimamizi na utupaji wa taka k wa mujibu wa Mkataba wa Basel wa mwaka 1989, Mkataba wa Basel unahusu udhibiti wa usafirishaji wa taka za sumu kati ya nchi na nchi na utupaji wake *(The Basel Convention on the Control of Trans Baundry Movement of Hazardous Wastes and their Disposal)*. Tanzania imeridhia Mkataba huu Aprili, 1993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la uanzishaji wa vituo vya Kanda ni kutokana na Ibara ya 14, Kifungu cha Kwanza, Ibara ya Mkataba wa Basel, ambao unazitaka nchi zilizoridhia mkataba huo kutokana na matakwa yao kuanzisha vituo vya kanda vya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia salama kwa ajili ya usimamizi na utupaji wa taka za sumu na taka zingine za kawaida. Aidha, nchi hizo zitaamua utaratibu muafaka wa uanzishaji wa mfuko wa dhamana wa kuwezesha uendeshaji wa vituo hivyo. Mkutano wa tatu wa nchi zilizoridhia Mkataba wa Basel uliofanyika Geneva Septemba,

1995 uliamua kuanzisha vituo vya Kanda katika nchi zinazoendelea na zile za Ulaya ya Mashariki.

Katika Bara la Afrika iliamuliwa vianzishwe vituo vitatu kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kifaransa, Kiarabu na Kiingereza katika nchi za Senegal, Misri na Afrika ya Kusini sawia. Katika Mkutano huo iliamuliwa pia kuanzisha kituo cha kuratibu vituo hivyo vitatu na kianzishwe nchini Nigeria. Uamuzi huu ulizingatia lugha kuu zinazotumika Barani Afrika ili kurahisisha mawasiliano. Hadi sasa jumla ya vituo 13 kama nilivyosema vya namna hii viko duniani kote na viko katika hatua mbalimbali za uanzishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa kuunda kituo cha Afrika wa Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo uliandaliwa na Sekretarieti ya Mkataba wa Basel mwaka 2003. Kwa mujibu wa Ibara ya tano ya Mkataba wa Kituo nchi za Afrika zinazozungumza kiingereza ndizo zitakazohudumiwa na kituo. Hata hivyo, nchi nyingine zitakazoridhia mkataba wa kuundwa kwa kituo na kupitishwa na Baraza la Kituo pia zitahudumiwa na kituo hata kama zinatumia lugha nyingine. Mkataba huu unahusu kwa sasa nchi 17 katika Bara la Afrika. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Botswana, Eritrea, Ethiopia, Nigeria, Namibia, Ghana, Gambia, Kenya, Lesotho, Malawi, Liberia, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Aidha, nchi za Mauritius, Msumbiji, Rwanda na Sychellys zimependa kutumia kituo hiki kwa sababu ziko karibu nacho. Shughuli za kituo hiki zitakuwa ni pamoja na kutoa mafunzo, uenezaji wa teknolojia, utoaji wa habari na ushauri, kukuza weledi kwa jamii kuhusiana na usimamizi wa taka za sumu na taka za kawaida. Kufanya utafiti na kutoa miongozi juu ya usimamizi wa taka kawaida kwa nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua madhara kwa afya na mazingira yanayoweza kusababishwa na usafirishaji na utupaji usiokubalika wa taka za sumu, Mawaziri wa Mazingira wa Afrika katika Mkutano wao maalum yaani *African Ministerial Conference on Environment Special Session* tarehe 9 hadi 10 Juni, 2003 huko Maputo, Msumbiji waliamua kuweka kipaumbele matakwa ya Kanda katika kutekeleza majukumu yatokanayo na mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Bamako wa mwaka 1991 unaohusu kupiga marufuku uingizaji katika Afrika wa Taka za Sumu na Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wake. Mkataba wa Basel ambao nimeshauelezea na mkataba wa Stockholm wa mwaka 2001 unaohusu Kemikali zinazodumu kwa muda mrefu katika mazingira.

Aidha, nchi hizi pia zimekubaliana kuboresha ushirikiano katika ngazi ya Kanda kupitia vituo vya utoaji mafunzo na uenezaji wa teknolojia mbadala katika usimamizi na utupaji wa taka. Pia ilikubalika kwamba vituo hivyo vihusike katika utekelezaji wa mpango wa mazingra wa *NEPAD* kwa kutoa huduma katika Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na kemilikali na taka za sumu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, gharama ya mkataba, kituo kitaendeshwa kwa kutegemea vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwa ni pamoja na michango ya nchi

zitakazohudumiwa na kituo, wafadhili mbalimbali na mfuko wa dhamana na Mkataba wa Basel. Michango ya nchi husika itafuata utaratibu uliowekwa na Umoja wa Afrika ambapo asilimia 50 ya gharama za uendeshaji kitachangiwa kwa kufuata Pato la Taifa na nchi husika yaani *Gross Domestic Product (GDP).*

Mkutano wa kwanza wa Baraza la Kituo, utafafanua kiasi cha mchango kwa kila nchi. Matokeo ya kuuridhia Mkataba. Kwa kuuridhia Mkataba huu wa kuanzisha rasmi kituo hiki, Tanzania itanufaika na taaluma itakayotolewa na kituo inayohusu kemikali na taka za sumu kwa lengo wa kuimarisha usimamizi wa taka hizo katika nchi yetu na nchi nyingine husika. Juhudi za pamoja katika usimamizi wa taka za sumu ngazi ya Kanda kama vile kuwa na mtambo wa kutekeleza taka za sumu na maabara teule zenye uwezo wa kuchunguza athari mbalimbali katika mazingira na afya zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni gharama kubwa kwa nchi moja moja kumudu kujenga na kuendesha mitambo au maabara za namna hiyo. Manufaa mengine kwa nchi yetu ni kama ifuatavyo, kuepuka athari kwa afya ya binadamu na mazingira zinazoweza kusabishwa na uingizaji, usafirishaji baina ya nchi au kati ya nchi na nchi na utupaji wa taka za sumu.

Pili, kupunguza uwezekano wa hasara ya fedha kwa Serikali, Taasisi zake na sekta binafsi zinazoweza kutokea kutokana na madai ya fidia kwa watu waliodhurika na taka za sumu au kemikali za hatari.

Tatu, kupata mafunzo mbalimbali kwa ajili ya viwanda kuhusu mbinu na teknolojia zinazokubalika kusimamia, kutekeleza au kutupa taka zenye sumu zinazozalishwa na vyanzo mbalimbali hususan viwanda vyetu na wadau wengine kama vile Halmashauri za Miji. Mafunzo yatawezesha kubuniwa kwa teknolojia bora na mbinu zinazopunguza utoaji wa taka zenye sumu wakati wa utengenezaji wa bidhaa na hivyo kupunguza gharama za kuendesha mitambo ya kuharibu taka.

Nne, kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine zilizoridhia Mkataba wa Basel katika juhudi za kukabili ongezeko la taka zenye sumu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kupata misaada ya vitendea kazi ili kujenga uwezo wa taasisi husika katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya nchi na nchi chini ya mkataba ya Basel na Bamako hususan uboreshaji wa sheria zetu na udhibiti wa uingizaji wa taka za sumu na sita, kuongeza nafasi za ajira kwa wataalam wa Kitanzania na kutoa nafasi kwa Taasisi za Tanzania kufanya kazi na kituo na hivyo kupata uzoefu wa Kimataifa katika suala hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba shughuli za uanzishaji wa kituo zinasimamiwa na zinaratibiwa na Dr. John Mbogoma ambaye ni Mtanzania na ana wadhifa wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti la utekelezaji wa mkataba. Kifungu cha 17 cha Mkataba huu kimebainisha umuhimu wa nchi zinazohudumiwa na kituo kutia saini na kuridhia Mkataba wa kuunda kituo. Aidha, kufuatana na kifungu cha 18 cha mkataba

huu idadi ya nchi zinazotakiwa kuridhia mkataba ili kituo kianze rasmi ni tano. Hadi sasa nchi nne zimeridhia mkataba huu. Nchi hizo ni Botswana, Mauritius, Namibia na Nigeria. Tanzania itakuwa ya tano na ikifanya hivyo kwa ridhaa ya Bunge lako Tukufu kituo kitaanza rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imelipa uwezo Bunge lako Tukufu wa kujadili na kisha kuridhia Mikataba inayohusu nchi yetu. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kuwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo.

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo *Agreement Establishing the Africa Institute for the Environmentally Sound Management of Hazardous and Other Wastes, 2004.*

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia Mkataba wa Basel kuhusu udhibiti wa taka za sumu baina ya nchi na pia imeridhia mkataba wa Bamako ambao unazuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika kuanzia tarehe 7 Aprili, 1993;

NA KWA KUWA Ibara ya 14, kifungu cha (1) cha Mkataba wa Basel unazitaka nchi zilizoridhia Mkataba huo kutokana na matakwa yao kuanzisha vituo vya Kanda vya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia salama kwa ajili ya usimamizi na utupaji wa taka za sumu na nyinginezo za kawaida na kwamba zitaamua utaratibu muafaka wa uanzishaji wa mfuko wa dhamana wa kuwezesha uendeshaji wa vituo hivyo;

NA KWA KUWA katika mkutano wa tatu wa nchi zilizoridhia Mkataba wa Basel uliofanyika Geneva Septemba, 1995 iliamuliwa kuanzisha Vituo vya Kanda kwa ajili ya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia mbalimbali zinazoendelea na zile za Ulaya Mashariki na katika Bara la Afrika vianzishwe vituo vitatu kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kifaransa, Kiarabu na Kiingereza katika nchi za Senegal, Misri na Afrika ya Kusini sawia;

NA KWA KUWA kifungu cha 17 cha Mkataba wa kuundwa Kituo kimebaini umuhimu wa nchi zilizoridhia mkataba wa Basel kuweka saini na kuridhia mkataba wa kuundwa kituo;

NA KWA KUWA katika kikao maalum cha 8 cha Baraza la Usimamizi la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP) Governing Council* kilichofanyika Gogia, Korea ya Kusini mwezi Machi, 2004 nchi kumi za Afrika zitakazohudumiwa na kituo ziliweka saini Mkataba wa kuanzisha wa kituo hiki. Nchi hizo zikiwa ni Afrika ya Kusini, Ghana, Kenya, Msumbiji, Nigeria, Rwanda, Swaziland, Tanzania, Uganda na Zambia;

NA KWA KUWA nchi yetu itanufaika na misaada itakayotolewa na nchi zilizoridhia Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na kemikali na taka za sumu kutoka kwa wafadhili mbalimbali, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa taka hizo katika nchi husika na katika Kanda, ikiwa ni pamoja na kuwa na mtambo au mitambo ya kuteketeza

sumu na maabara teule zenye uwezo wa kuchunguza athari mbalimbali katika mazingira na kwa afya;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Mkataba wa kuunda kituo hiki, mkataba huu sharti uridhiwe na nchi tano ndipo kituo kianze rasmi na kwamba hadi sasa mkataba huu umeridhiwa na nchi nne zinazohudumiwa na kituo hiki.

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ambao Tanzania itapata kwa kuridhia mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63 kifungu kidogo cha (3) na kifungu kidogo cha (e) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge hili katika Mkutano wa Sita linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo kwa mujibu wa Mkataba wa Basel yaani yaani *Agreement Establishing the Africa Institute for the Environmentally Sound Management of Hazardous and Other Wastes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana mtoa hoja Mheshimiwa Waziri. Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea. Nitamwita sasa Msemaji wa Kamati ambayo ilijadili na kupitia Mkataba huo ili aweze kuja kutoa maoni ya Kamati yake.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA – (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Kanda cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 70(ii) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 2004 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Kanda yetu ya Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri la Muungano, familia, ndugu wakazi na wapiga kura wote wa Tunduru kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aliyekuwa akishughulikia masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti, kilichosababishwa na ajali ya ndege.

Marehemu atakumbukwa daima kuwa alikuwa mchapakazi na uadilifu wake kwa moyo wake wa kujituma na kwa uongozi wake wa mfano. Sisi wote humu Bungeni ni

mashahidi wa wasifu huo wa Marehemu. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa maoni na ushauri wa Kamati naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wote kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu, Bunge letu Tukufu na Taasisi iliyomlea na kumjenga kitaaluma yaani Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Azimio hili kwa mujibu wa Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 204 ni hawa wafuatao, wa kwanza, ni Mheshimiwa Job Ndugai, ambaye ni Mwenyekiti, wa pili ni Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa James Lembeli.

Wengine ni Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Lucy Mahenga, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo,Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Anastazia Wambura, ambaye ndiyo mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilisaidiwa na Makatibu wake wawili, Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Dickson Bisile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilikaa tarehe 31 Januari, 2007 kutafakari na kujadili kwa kina maudhui yaliyomo kwenye Mkataba wa Basel wa mwaka 1989 ulioridhiwa na nchi yetu mwaka 1993. Mkataba wa Basel katika Ibara yake ya 14 kifungu cha (1) ndiyo chimbuko la Azimio hili ambalo Bunge lako Tukufu leo hii linaombwa kuridhia kwani Ibara hiyo inazitaka nchi zilizoridhia kutokana na matakwa yao kuanzisha vituo vya Kanda vya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia salama kwa ajili ya usimamizi na utupaji wa taka za sumu na nyingine za kawaida na kwamba nchi hizo zitaamua utaratibu muafaka wa uanzishaji wa mfuko wa dhamana wa kuwezesha uanzishaji wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujadili Azimio hili Kamati yangu ilizingatia zaidi katika kujua na kujadili ni kwa kiasi gani suala la uharibifu wa mazingira limekuwa kero dunia nzima kwa wanadamu, mimea, wanyama na hatimaye kuwa kikwazo kwa maendeleo ya Mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania.

Pia Kamati ilihoji ulazima wa nchi yetu kujiingiza katika masuala yahusuyo uanzishaji wa kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo. Kamati ilitafakari na kujadili vipengele vya mkataba wa kuanzisha kituo hiki na hatimaye gharama na faida zake kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilijulishwa na Wizara kwamba kituo hiki kimeanzishwa katika mji wa Pritoria nchini Afrika Kusini na kilichobakia ni ridhaa ya wanachama wasiopungua watano wa Mkataba wa Basel kutoka Mashariki na Kusini mwa Afrika ili kukifanya kituo hicho kiwe rasmi cha Kanda. Pamoja na hayo Kamati iliyohoji kwa nini Afrika Kusini ipewe Makao Makuu ya Kituo hicho wakati haijaridhia bado mkataba wa kuanzishwa kwa kituo hiki.

Vile vile Kamati ilihoji vigezo vilivyotumika kupendekeza makao makuu ya kituo hicho kuwa Afrika Kusini na siyo katika nchi nyingine yoyote. Pia Kamati ilipenda kujua kama Serikali yetu imeandaa utaratibu gani ama mbinu thabiti za zitakazotumiwa kugundua japo baadhi ya maeneo yenye taka za sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imeona zipo faida nyingi ambazo Taifa letu litazipata ambapo Bunge lako Tukufu litaridhia mkataba huu na baadhi ya faida hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Faida ya kwanza, Taifa letu litanufaika na misaada zitakazotolewa kwa nchi zitakazoridhia mikataba ya kimataifa inayohusiana na kemikali na taka za sumu kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

(ii) Faida ya pili, Taifa letu litapata mahali ambapo litaweza kuteketeza taka za sumu.

(iii) Faida ya tatu, ridhaa hii itaongezea nguvu ya uhusiano wa Taifa letu, kidiplomasia na Mataifa mengine wanachama yanatufanya tuwe na nguvu kubwa katika kutoa maamuzi yanayohusu masuala ya mazingira duniani.

(iv) Faida ya nne, Taifa letu litafaidika na ajira za Kitaifa na Kimataifa na kama tulivyokwisha kusikia kwa sasa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho ni Dr. Juma Mbogomo ambaye ni Mtanzania.

(v) Faida ya tano, kwa kutumia Idara na vitengo mbalimbali vitakavyoundwa katika kituo hiki nchi yetu itakuwa na uwezo mkubwa wa kuzitambua na kuzitathimini taka zenye sumu mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo. Pamoja na faida zilizotajwa na Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijipange kuhakikisha kwamba inakuwa na wataalam watakaoshiriki ipasavyo kufanya kazi katika kituo hiki.

(ii) Kwa kuwa Tanzania ina ukanda mrefu wa Bahari ambazo ni kilometa 800 Serikali iwe makini kudhibiti uchafuzi unaoweza kusababishwa na meli zinazosafirisha taka kupitia eneo la nchi yetu kupeleka kwenye kituo.

(iii) Kwa kuwa suala la mazingira ni mtambuka Kamati inapendekeza kuwa Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa sekta zote nchini zinaandaliwa vya kutosha kuzielewa, kuziheshimu na kuzitekeleza taratibu, kanuni na sheria zenye kulenga kuhifadhi mazingira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni na mapendekezo ya Kamati yangu kuwa kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ambayo Tanzania itapata kutokana na kituo hiki hasa katika masuala ya utunzaji wa mazingira kwa ujumla, Kamati yangu inaungana na Serikali kupitisha Azimio hili la Bunge la kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Kanda yetu kilichopo Pritoria Afrika Kusini na Usimamizi wa Taka Sumu na Nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF (k.n.y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya yote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkoani pamoja na mimi binafsi natoa rambirambi zangu kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, pamoja na watu wengine wote waliofariki katika ajali ya ndege iliyotokea Mkoani Mbeya. Mwenyezi Mungu awalinde jamaa na ndugu wa Marehemu katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali kuwa watumishi wa Kimataifa na watumishi wa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (b) (c) na 70(2) Toleo la mwaka 2004, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge kwa kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo ch Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo la mwaka 2004 *(Agreement Establishing the Africa Institute for the Environmentally Sound Management of Hazardous Wastes and other Wastes, 2004). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(2) inahusu kila nchi mwanachama kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha uzalishaji wa taka za sumu unapungua sambamba na hali halisi ya jamii kiuchumi na kiteknolojia. Tanzania miongoni mwa nchi zinazozalisha taka hizo japo kuwa ni kwa kiwango kidogo ukilinganisha na Mataifa yenye viwanda vikubwa duniani, wale wachache ambao wanatumia kemikali katika utendeji wa kazi zao za kila siku bado hawajakuwa na matayarisho mazuri ya utupaji wa taka hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazalishaji hawa wanaweza kuwa hawajui jinsi ya kuziteketeza taka hizo na kusababisha madhara makubwa kwa jamii ambazo bila kuelewa hujikuta zinaathiri sana na pengine kupoteza maisha ama wazilishaji wengine wanaelewa kabisa madhara ya taka hizo ili kutokana na udhaifu kiutendaji katika kusimamia na kuhakikisha utupaji taka utupaji salama wa taka hizo, kusababisha madhara makubwa kwa viumbe hai na pengine huleta madhara ya kudumu katika ardhi na maeneo husika. Mfano mzuri ni wa hili ni mto uliopo karibu na mgodi wa dhahabu wa Geita ambao afya za watu zimeathirika na vifo kutokea na mazingira yameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya tisa inahusu usafirishaji nje ya mipaka ya nchi, ni kweli kwa nchi maskini kama yetu ndizo zilizo katika katika hatari za kuwa jalala bila kujua kutokana na kutokuwa na teknolojia za kisasa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kambi ya upinzani inadhani Tanzania kutokuwa na vifaa vya doria katika bahari kwa sababu kuwa kama kweli zingekuwepo meli za uvuvi zingekuwa zinavua *deep sea fish* bila ya kuwa na vibali vya nchi yetu kukosa stahiki ya mapato. Hivyo basi uwezekano wa meli hizo kumwaga taka ambazo madhara yake yanaweza kuanza kujitokeza zaidi ya miaka mitano au zaidi kutokana na matumizi ya maliasili za bahari kubwa zaidi. Pamoja na mambo mengine ni bora udhibiti wa habari ukatiwa kipaumbele zaidi, kwani hakuna fidia yoyote inayoweza kulingana na uhai wa mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa usafirishaji na utupaji wa taka huwa ni haramu au siri bila ya nchi husika kuwa na taarifa na madhara yanaweza yasiwe ya wazi, hivyo ni muhimu kwetu kuwa makini kwani mkataba huu ulikuwepo lakini kwa nchi tajiri haziheshimu mikataba hii kwa nchi maskini. Mfano mzuri ni janga lililotokea katika nchi ya Ivory Coast, raia wake zaidi ya mia walipatwa na matatizo na wengine kupoteza maisha kutokana na taka za sumu kumwaga kwenye ukanda wake wa bahari. Kituo cha nchi zinazozungumza kiingereza kiko Pretoria, Afrika ya Kusini, lakini bado Afrika ya Kusini haijaridhia, hili linatupa wasiwasi. Kila nchi wanachama itatakiwa kuchangia kituo hicho lakini haieleweki ni utaratibu gani utakaotumika katika kujua kiwango cha kila nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14(1) ya mkataba huu unazitaka nchi kuridhia ili kuanzishwa vituo vya kanda ya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia salama kwa ajili ya usimamizi na utupaji wa taka za sumu na nyinginezo za kawaida. Pamoja na uamuzi wa taratibu muafaka wa uanzishaji wa mfuko wa dhamana na kuwezesha uendeshaji wa vituo hivyo.

Kambi ya Upinzani haina pingamizi na hili na inadhani utaratibu huu ni muafaka isipokuwa umechelewa, kwani makampuni makubwa hayajali uhai wa watu, yanajali faida zaidi. Hivyo kwao hutupa taka zenye athari kwa watu si jambo la kawaida ni jambo la kawaida japokuwa wanaelewa madhara yake kwa siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, sasa tutaingia katika mjadala wa mchango wa pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliokwisha kuomba kuchangia mada hii mpaka sasa wako wanne. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Cythia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, atafuatiwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi atafutia na hatimaye Mheshimiwa Godfrey Zambi, atakuwa msemaji wetu wa mwisho katika mada hii. *(Makofi)*

**MHE. CYTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana jioni ya leo kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuzungumzia kuhusu kuridhia mkataba ulio mbele yetu.

Kwanza kabisa kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya pamoja na wananchi kwa ujumla kutoka Mkoa wa Mbeya naomba kutoa pole za dhati kabisa kwa familia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na kifo cha ndugu yetu Mheshimiwia Juma Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Tunduru. Vilevile ninaomba kutoa pole kwa wale wengine wote ambao nao wamefariki ambao walikuwa pamoja katika ajali ile. Wako wengine ambao bado wako hospitali ambao ni majeruhi ninawaombea waweze kupona haraka. Ninaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Juma Akukweti, mahali pema peponi pamoja na wale wengine wote ambao waliiaga dunia, Mwenyezi Mungu atazidi kuwapokea na kuwastarehesha mahali pa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salaam hizo za pole vilevile naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Mbeya kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, ambaye amepokea wadhifa mkubwa sana kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ni sifa kubwa sana kwa Tanzania, ni sifa kubwa sana kwa wanawake, ni kazi kubwa yenye majukumu makubwa yenye changamoto nyingi sana na sisi kama Watanzania tunasema Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, ataweza kwa sababu anauwezo mkubwa. Tunamtakia kila la kheri katika utendaji wake wa kazi za siku hadi siku.

Vile vile niwapongeze Wabunge wenzetu ambao wamepata nyadhifa mbalimbali katika kipindi hiki cha hivi karibuni kuwa Mawaziri au Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali, nampa heshima kubwa sana Mheshimiwa Dr. Batlida Burian pale ambaye amekaa kama *Chief Whip,* tunajifuvunia sana sisi wenzie huku nyuma, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema maneno hayo sasa naomba niseme kwamba nimesimama hapa ili kuweza kuunga mkono kuridhiwa kwa mkataba huu wa kuunda kituo cha Afrika cha usimamizi wa taka za sumu na nyinginezo ambao ni kwa maslahi ya afya za Watanzania, lakini vile vile kwa hifadhi ya mazingira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo wa kuridhia mkataba huu tukiwa kati ya zile nchi tano ambazo tayari zimekwisha ridhia mkataba huo. Faida ya kuridhia mkataba huo tumeshazisikia na mimi moja kwa moja ninaungana nazo zote zina umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa kuteuliwa kwa Dr. John Mbogoma, kuwa *Executive Director* wa kituo hiki huko *South Africa* ni heshima kubwa sana kwa Watanzania. Napenda kuchukua nafasi kumpongeza sana kwa kuchukua nafasi hii kubwa, vile vile inatupa nafasi Mtanzania mwingine ambaye anatuwakilisha katika taasisi za Kimataifa, Tanzania tunazidi kuwa na sura nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya mkataba wa mwaka 2001 kuhusu kusimamia kekimikali zinazodumu kwa muda hapa Tanzania tunalo Baraza letu la Hifadhi na Udhibiti wa Mazingira ambayo ni *NEMC*. Kwa niaba ya Serikali taasisi hii imepewa jukumu la kutekeleza programu ijulikanayo kama *ASP* yaani ya *Africa Stoppers Program* ambayo moja ya kazi zake ni kushughulikia uondoaji wa shehena kubwa sana za dawa chakavu pamoja na udongo ulioathirika na dawa zilizozikwa. Kazi hii ni nzito kwa sababu ni ukweli mtupu kwamba hapa Tanzania dawa za aina hii zimesambaa sana katika mashamba makubwa yakiwemo mashamba ya kilimo na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na tathimini iliyofanyika miaka minne iliyopita na *NEMC* inafahamika kwamba tayari tunazo tani zipatazo 1,400 za aina hii, ni tani nyingi sana. Tani hizi za dawa hizi za sumu ziko katika maeneo tunayoishi sisi binadamu ni hatari, sasa kwa kuwa ni hatari ni lazima hatua ichukuliwe chini ya mkataba huu wa *ASP,* ni lazima sumu hizi ziondolewe. *NEMC* kama taasisi ambayo iko chini ya Serikali imepewa jukumu hili la kufanya kazi hiyo, sasa uanzishwaji wa kituo hiki ambacho tumesema kiko *South Africa,* mimi naona taasisi hii vilevile itaweza kufaidika, kwa nini itafaidika? Itafaidika kutokana na teknolojia ambayo itasambazwa na kituo hiki, teknolojia hiyo tunaihitaji Watanzania, tukubali kabisa bado tuko nyuma katika masuala ya teknolojia. Hiyo ni moja ya majukumu ambayo yamepewa kituo hiki ambacho tunakiridhia leo, lakini tukubali kabisa kwamba kazi hiyo ambayo kituo hiki kimepewa ni nzito na ni ya faida kubwa sana kama *NEMC* kama kituo wanahitaji kabisa utaalamu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kama taasisi hii ambayo tunasema kwamba ni moja ya taasisi muhimu sana hapa nchini katika usimamizi wa mazingira kutakuwa na faida ya kupata *information* yaani taarifa mbalimbali ambazo zinapatikana katika taasisi mbalimbali zilizomo katika nchi zilizoridhia mkataba huo *(information is power)* kwa hiyo, ukiwa na *information* ambayo inahusu masuala haya ya udhibiti wa dawa hizi za sumu, basi na wewe unakuwa na uwezo wa kuwaeleza watu wako ili waelewe, tatizo letu ni kwamba wananchi wetu hawafahamu wanaishi na dawa ziliyo na sumu lakini hawaelewi kwamba ni hatari kubwa, kwa hiyo, taarifa hizi ambazo nyingine tunazo na nyingine tutazipata kutokana na kituo hiki, taarifa hizo zitasambazwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile jukumu mojawapo la kituo hiki ni kufanya *research, research* ni muhimu sana yaani utafiti. Matokeo ya utafiti tunayahitaji na kwa mujibu wa taasisi yetu ya *NEMC* tunacho kitengo ambacho kinashughulikia utafiti, kwa hiyo, itakuwa ni busara sana kwa *NEMC* yenyewe kupata na kufahamu tafiti za sehemu nyingine zinasema nini. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepata upeo mkubwa sana wa namna ya kudhibiti dawa za taka na taka ambazo zina sumu. *NEMC* yenyewe

itaweza kujijengea uwezo yaani *capacity building* ambao na wao wanahitaji kabisa, wanahitaji kutoa maarifa kwa taasisi nyingine ambazo zinafanya kazi pamoja nayo. Taasisi hizo ni kama Serikali za Mitaa, yaani Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji, hawa wanahitaji kuelimishwa.

Kwa hiyo, kama taasisi yetu wenyewe yaani *NEMC* itakuwa imepata maarifa haya, ikapata teknolojia ya kisasa, ikapata uelewa wa hali ya juu basi ni rahisi kabisa kwa wao kufanya kazi kwa karibu sana na taasisi nyingine na si taasisi nyingine tu ni pamoja na wananchi ambao nimekwishaeleza kwamba wanaishi katika mazingira hatari wanafanya mambo hatari sana, wanarundika dawa nyingine kwa kuficha, kwa mfano *DDT* hiyo ninayozungumzia hapa, hayo matani mengi ninayoyazungumzia sehemu kubwa ni *DDT* ambayo ni hatari kabisa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, elimu ambayo itakuwa inatolewa na *NEMC* itasiaidia sana kuwapa maarifa wananchi pia itajenga ushirikiano pamoja na taasisi nyingine ambazo ziko chini ya nchi ambazo zimeridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutoa kama rai, kwamba kwa kuwa taasisi kama *NEMC* ambayo nasema kwamba itafaidika na itakuwa tayari kufanya kazi na kazi nyingine imeshaanza kufanyika kama hii utekelezaji wa programu hii ya *ASP* naomba sana ikiwa ni pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba ni vizuri taasisi hii ikajengewa uwezo mkubwa wa kifedha, ni muhimu kwa sababu hali ya kifedha ya taasisi si nzuri na inategemewa kufanya kazi ambazo ni nzito ambazo watu wengi wamejisahau hasa hasa katika usimamizi wa mazingira, ambazo hata watu ambao ni maarufu mpaka sasa hawaelewi maana ya udhibiti wa mazingira na hifadhi wa mazingira na umuhimu wake mpaka sasa hawaelewi.

Kwa hiyo, hii taasisi ikishirikiana na taasisi nyingine pamoja na wadau wengine kwa ujumla ina kazi kubwa ya kufanya kazi ya kusimamia mazingira na kwa kuwa tumetangaza hadharani na wananchi wote wanajua, Taifa linajua kwamba sasa ni vita, ni vita ya kupigana kabisa kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa na kuhifadhiwa. Kwa hiyo, Serikali nitaiomba na pengine kuanzia bajeti ya safari hii, kuiangalia taasisi hii kwa jicho la huruma na kuifanya ifanye kazi kwa kadri ilivyopewa meno chini ya sheria Na. 20 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono kuridhiwa kwa mkataba wa kuundwa kwa kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Taka Nyinginezo hapa nchini, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana, napenda nikushukuru Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Hilda Ngoye kama tunavyofahamu yeye ndiye Mwenyekiti wetu wa Baraza la Hifadhi ya Mazingira la Taifa (NEMC) kwa hiyo, tunakushukuru kwa mchango wako na nadhani kazi hii kubwa ipo mikononi mwako. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi atafuatia.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia Azimio hili lilipo mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Kikao hiki napenda kutoa salaam zangu za pole kwa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Wabunge na familia ya mpendwa wetu hayati Juma Akukweti, Mbunge wa Tunduru na aliyekuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kweli tumepata pigo kubwa na hasa sisi wa Kusini kwa sababu tulikuwa tunamwona huyu kama ni nyota yetu inayoongoza na sisi tukimfuata nyuma yake.

Mheshimiwa Spika, papo hapo ningependa kutoa salaam za pongezi nitoe salaam kwa mwenzetu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro ambaye ameondoka hapa nchini kwenda Umoja wa Mataifa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umaja huo. Hii ni kazi kubwa, hii ni heshima kubwa kwa Tanzania na kwa kweli haijapata kutokea katika hostoria yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, papo hapo naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa kuteuliwa kwake kuwa *Chief Whip* na mambo yote yanayoambatana na kazi hiyo. Nashukuru kwamba humu ndani ya Bunge kila wakati nitakuwa namwona kwa sababu anakaa *opposite* na mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Bernard Membe, yeye na mimi tuko karibu kabisa kwa hiyo nashukuru sana kwa kupandishwa cheo kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Nina imani kutokana na uzoefu wake kazi hiyo haitakuwa ngeni kwake wala ngumu na namwombea kwa Mwenyezi Mungu afya na neema tele katika utendaji wa kazi yake. *(Makofi)*

Mwisho lakini si kwa umuhimu Naibu Mawaziri wawili ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudance Kayombo, nawapa pongezi za dhati kutoka kwenye *back bench* na kwenda *front bench.* Sasa na ninyi mtaona maana ya mishale inayotoka *back bench. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie walau kwa kiasi kidogo Mkataba huu uliopo mbele yetu wa kuanzisha Kituo cha Usimamizi wa Taka za Sumu kule Pretoria, Afrika ya Kusini. Kwa bahati nzuri kwa kipindi kirefu nimekuwa nikihusika sana na mambo ya baharini kwa wale wasiojua mimi katika *profession* yangu ni Afisa Uvuvi kwa hiyo nayafahamu sana mambo ya bahari na baharini, nazifahamu meli mbalimbali, meli ndogo, meli kubwa za abiria za mizigo nazifahamu. Hizi meli mara nyingi zinafanya uchafuzi mkubwa sana huko baharini.

Kwanza kutokana na mabaharia waliomo mule halafu pia kutokana na uchakavu wa vitu mbalimbali wanavyovitumia mara kwa mara jalala lao ni bahari. Sasa hiyo labda ni afadhali lakini kuna hawa wanaochukua taka ili kutupa sehemu mbalimbali. Wao wapo wa aina mbili, kuna wale wanaochukua taka za kawaida hizi kwa sababu hawana sehemu ya kutupa basi huenda baharini katikati ya bahari wanafungua milango na taka hizi zinaingia baharini. Sasa wapo wengine wanaochukua taka za sumu kama mnavyojua katika viwanda vingi sana duniani vikubwa vikubwa vinazalisha taka nyingi zenye sumu. Hata mimi mwenyewe binafsi nimewahi kuziona hizi meli zikitupa taka. *(Makofi)*

Sasa nataka kusema ndugu zangu sisi katika Mkataba huu ni lazima tuwe waangalifu kweli kweli kwa sababu tuna kilometa kama 800 kutoka Mtwara mpaka Tanga ambako meli hizi zinaweza kufanya uhalifu wake.

Kwa hiyo, nataka kusema kwamba licha ya kuwa na kituo hiki Pritoria, Afrika ya Kusini sisi wenyewe kupitia Taasisi zetu kwa mfano *NEMC* Wizara hiyo ya Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii sisi wenyewe tungekuwa na utaratibu wa kuwa na aina fulani ya *inspectorate*. Iwepo *inspectorate* kwa lengo kwa kukagua mara kwa mara nini kinatokea katika bahari yetu ili kwamba tukiona dalili zile kwa sababu kama ukiona taka zinaanza tuseme sehemu fulani ukiwa na *radio call* unaweza kufahamisha *ICAO* kwamba kuna meli inatupa taka. Kwa hiyo, hii inaweza kuwezesha kuchukua hatua ili kwamba ile meli iweze kukamatwa au iweze kuripotiwa na Mataifa mbalimbali yaweze kuja kuchukua hatua dhidi ya meli hiyo. Lakini kama hatutakuwa na *inspectorate* sisi wenyewe katika nchi hii kwa kweli manufaa makubwa hatutayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema wakati umefika kama vyombo hivi havitakuwepo katika Taasisi au Wizara hii naomba sana tuhakikishe kwamba vinakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Kituo hiki ambacho kitakuwa Afrika ya Kusini, mimi ningependekeza wakati sisi tunavyounga mkono Mkataba huu tuwaeleze wenzetu Waafrika na hasa tukieleze kile Kituo cha Pritoria kwamba ingefaa katika eneo letu kuwepo na vituo vidogo vidogo kwa ajili ya kuangalia shughuli hizi za bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mini ningependekeza kiwepo Kituo kimoja Cape Town halafu unakuja juu Maputo, halafu mwisho unakuwa na kituo Dar es Salaam. Maeneo haya yako katika sehemu *strategic* kiasi kwamba kama kuna mtu yeyote ameleta hizo sumu au ana nia ya kutupa taka hizi, vituo hivi ni rahisi kuona ni kitu gani kinafanyika. Halafu tuweze kuchukua hatua. Lakini kama hatutakuwa na utaratibu wowote wa kufuatilia hii itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia kuwepo utaratibu maalum nchini wa namna ya kuteketeza taka za sumu. Hizi taka jamani tunazizalisha kwa mfano katika mahospitali yetu makubwa kama *KCMC,* Bugando, Muhimbili na kadhalika na hata katika hospitali hizi za Mikoa kuna taka za sumu zinazotokana na mabaki ya sisi binadamu zipo nyingi tu. Kwa wale wanaofanyiwa operesheni wanakatwakatwa nyama zile. Kwa upande wa wodi za wazazi kuna ma-*placenta.* Mambo kama haya kama hatuna utaratibu maalum wa namna ya kuzika na kuyafukia na kuyateketeza tunaweza kuanzisha balaa kwa sababu ni *material* ambazo kwa wepesi kabisa zinaweza kuliwa na *bacteria* au na virusi tukapata madhara mengine makubwa. Wakati huo huo taka zile ngumu ngumu za maplastiki, za vyuma na kemikali hasa ya dawa hizo nazo pia tuwe na utaratibu mzuri wa kuziteketeza ili yaungue yote na tusipate athari za *fumes* zile nazo zinakuwa na madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi katika mchango wangu ningesema kwamba hili litukumbushe na hili liweze kututayarisha kuona ni jinsi gani tunaweza kunufaika na shughuli kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kukumbusha tu kwamba kuna suala la hili la vitu kama *asbestos,* matumizi mabaya ya *mercury* na kuna matumizi ya *DDT. DDT* ni nzuri kuua mbu, lakini ikitumika kwa muda mfupi na tuki-*control* vizuri ni nzuri. Lakini ikiachiwa hivi hivi ndiyo haya aliyoyasema Mwenyekiti wa *NEMC* kwamba *DDT* inaweza kutupa madhara makubwa na kutuangamiza. Ningeomba kwa nchi tuangalie jinsi gani dawa ya namna hii tunavyoweza kupunguza madhara yake ili yasiwe makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kuchangia haya, nataka tu kusema kwamba kwa kweli naunga mkono jitihada zote za kuanzisha Kituo huku Kusini Afrika ambacho kitakuwa kinashughulikia suala lote la hizi taka sumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kama walivyofanya wenzangu na mimi nisionekane mtu wa ajabu, naomba kwa niaba ya wananchi wa Ludewa na kwa niaba yangu mimi mwenyewe nitoe salaam zangu za rambirambi kwa dhati kabisa kwa familia za Marehemu wote waliokumbwa na msiba ule uliotokea pale Mbeya hususan ndugu yetu, mpendwa wetu aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Marehemu Juma Akukweti.

Pili, naomba vilevile niwapongeze ndugu zangu mbalimbali waliopata nyadhifa mpya, aliyepata wadhifa wa Kimataifa, waliopandishwa vyeo na ndugu zangu waliokwenda kwenye *front bench* wakitoka kwenye *bench* za huku nyuma, wote nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Maliasili na Mazingira, kwa hiyo, mengi tumeyazungumza kwenye hoja ile ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Anastazia Wambura. Lakini nilidhani niseme mawili tu katika kujaribu kufafanua mambo ambayo nadhani ni vizuri tukayafahamu wakati tunaridhia Mkataba huu. *(Makofi)*

Kwanza, nitapenda kuzungumzia kuhusu suala zima la utaalam unaotakiwa ili Tanzania iweze kukifaidi Kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo kitafanya kazi ya kuratibu haina maana kwamba kitatuma wataalam katika nchi hizo husika na kufanya kazi aidha ya kuainisha taka hizo zilizopo au kujaribu kuangalia vipi zitateketezwa. Kazi yake itakuwa ni kuratibu, kutoa mafunzo, kutoa maelekezo, lakini shughuli zenyewe za kuainisha sumu hizi zilizoko ziko

kiasi gani na athari yake kwenye mazingira itakuwa ni kazi ya Taasisi zilizoko kwenye nchi husika na Tanzania ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuainisha taka za sumu kutakuwa katika maeneo mawili. Kutakuwa na zile sumu ambazo zinatokana na kuhifadhi kemikali au dawa kwa muda mrefu zikabadilika *(chemistry)* badala ya kuwa za manufaa kwa matumizi yaliyotegemewa, zikabadilika na kuwa ni hatari kwa viumbe au kwa mazingira. Taka hizo itabidi zifanyiwe tathmini moja kuainisha ziko wapi, ziko kiasi gani, athari yake ni kiasi gani na kujua kwamba zikiachwa zinaweza kuleta athari kiasi gani. Kwa kawaida tathmini ya namna hiyo kwa pamoja tunaiita kitaalam *Environmental Impact Assessment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya pili, inaweza kuwa ni kemikali au dawa ambazo yanaagizwa, lakini kama tuna utaratibu mzuri inatakiwa kabla ya dawa hazijaruhusiwa kuingia nchini zifanyiwe tathmini *(risk assessment)* ili kujua yakiletwa kwa kiasi hicho kabla hayajaja nchini kwetu yana uwezo wa kuleta athari kiasi gani na baada ya kukaa kwa muda gani au baada ya kutumiwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya tatu ya taka ndizo hizo ambazo zinaweza kusombwa kutoka nchi zinakozalishwa kwa makusudi kwa ajili ya kwenda kutupwa katika nchi nyingine. Hiyo nayo itabidi aidha, kama imepita kwa mkondo unaoeleweka zijulikane na mapema kwamba dawa na kemikali zinazoletwa zitakuwa na athari fulani nayo inahitaji aidha, *risk assessment* au *environmental impact assessment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuchangia hapa ni kwamba kazi hii ya kuainisha kufanya *risk assessment, environmental impact assessment* itakuwa ni kazi ya taasisi za kwetu hapa hapa nchini. Zikipewa mwongozo, zikipewa pengine hata rasilimali za kufanyia kazi na vitendea kazi vingine na Kituo hiki tunachokizungumzia. Sasa kuna haja basi ya nchi yetu kujiweka katika hali ya kuweza kushughulikia tathmini hizo nilizozizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu tunapozungumza utaalam huo hapa nchini ni kidogo sana. Taasisi zinazoweza kufanya tathmini hizo ni chache sana. Badala ya kungojea Kituo hicho kije kianze kufanya kazi ya kutoa mafunzo ambayo yatakuwa ya aghali sana. Ni vyema basi sisi wenyewe, Wizara zinazohusika ambazo kwa kweli tunajua mazingira ni mtambuka zitakuwa ni sekta nyingi tu kujiweka tayari kwa maana ya kuwa na wataalam waliobobea wanaoweza kufanya tathmini hizo na kuweza kuainisha na kugundua dawa hizo na kupendekeza kwa namna ipi yaweze yakateketezwa na ni wapi yakateketezwe kwa kutumia vifaa gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hili kwa sababu najua utaalamu huo hatuna na tusibweteke tukakaa tukadhania maadamu kutakuwa na Taasisi kama hiyo basi mambo yetu yote yatakwenda vizuri, si kweli. Itabidi kama alivyosema Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye kwamba Taasisi zetu za hapa nchini ikiwa pamoja na *NEMC.* Lakini najua kuna taasisi nyingine nyingi, Vyuo Vikuu na nini vipewe uwezo wa kitaaluma wa kuweza kutusaidia kufanya kazi hizi. Hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nililotaka kuchangia ni suala nzima la kuheshimu maamuzi ya wataalam kuhusu taka za sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetunga sheria za mazingira, tumeweka na taasisi kama *NEMC* ambazo zinashughulikia usimamizi wa sheria hizi. Uzoefu wangu na wenu nadhani mtakubaliana na mimi Watanzania katika ngazi zote tuna tabia ya kudharau na kutoheshimu sheria tulizotunga wenyewe, kudharau vyombo tulivyoweka sisi wenyewe hasa pale vinapotoa maamuzi kuhusiana na mazingira tunapuuza kwamba hawa wanatupotezea muda. *NEMC* sijui nini, achana na hao watu, sisi tuendelee na mambo ya maendeleo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya ndiyo yatakayokuwa yanaendelea kutokea kwa suala la taka za sumu basi tumeumia. Kwa sababu kupuuza puuza huko kutaleteleza taka hizi kuendelea kubadilika *chemistry* yake, zitaendelea kusambaa, kuleta athari nyingi na hatari kwenye mazingira na baadaye kwa sisi binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba sisi wote, sekta zote toka ngazi za juu, viongozi mpaka kwa mtu wa kawaida tuheshimu Sheria tunazoweka, tuheshimu taasisi tulizojiwekea zinazofanya kazi ya kuamua mambo mbalimbali.

Katika hili maamuzi yatakayotolewa na Taasisi kama *NEMC* kuhusiana na taka za sumu basi maamuzi yale yaheshimiwe na yatekelezwe. Lakini kuna haja ya kutoa elimu katika ngazi zote kuanzia viongozi wa ngazi za juu na hapa nasisitiza *decision makers,* Mawaziri, Makatibu Wakuu, viongozi mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge ambao tunashiriki kwa namna moja au nyingine kutoa maamuzi na wananchi wa kawaida kupewa elimu kuhusiana na taka za sumu na utendaji wa kazi wa chombo hiki ambacho leo tunataka kukiridhia kusudi kweli kiweze kusaidia nchi yetu iondokane na balaa la kuwa na takataka hizi ambazo tumezijaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine napenda kutumia mfano kwamba tunakusanya haya, tunakaa kwenye matawi halafu tunayakataa mashina tutadondoka na tutaumia kama hatutakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango huo mfupi. Mimi naunga mkono hoja hii kusudi turidhie kuanzishwa kwa Kituo hiki ili tuwe nchi ya tano tukiwezeshe kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate kuchangia angalau kwa sehemu kidogo juu hoja iliyo mbele yetu ya kuzungumzia kuridhiwa kwa Mkataba wa kuunda kituo kwa ajili ya kusimamia taka za sumu na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba na mimi nichukue nafasi hii niungane na wenzangu waliotangulia kusema. Kwanza, nitoe salaam zangu za rambirambi kwa familia za Marehemu Juma Akukweti aliyekuwa Waziri wetu pamoja na

wale aliopata nao ajali na kupoteza maisha yao. Naomba Mwenyezi Mungu azirehemu roho zao na kuziweka mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nichukue nafasi hii kuwatakia wale waliopona katika ajali hiyo na hasa yule aliyekuwa Msaidizi wa Marehemu Juma Akukweti ambaye bado tunaambiwa yuko hospitali basi aweze kupona haraka ili aweze kurejea katika shughuli zake za kawaida. Lakini naomba pia nichukue nafasi hii kwa sababu ajali ile na kama alivyosema Waziri kwamba ajali hiyo ilitokea Mbeya na kwa kuwa na mimi natoka Mbeya naomba pia nichukue nafasi hii kwa kweli niwape pole kubwa sana wafanyabiashara waliokuwa wanafanya shughuli zao katika soko la Mwanjelwa ambalo liliungua moto pale tarehe 12 Desamba, 2006 na kwa maana hiyo kupoteza mali zao nyingi pamoja na fedha taslim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii na nina hakika wengine watakuwa wananisikiliza ninapozungumza basi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wa Mkoa wa Mbeya na kwa sababu Profesa alishazungumza tuwape pole sana kwa mkasa huo uliowapata na Mwenyezi Mungu atawajaalia watapata mali nyingine kufidia ile ambayo walishaipoteza. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kwa ufupi sana niwapongeze wote ambao wamepata nyadhifa mbalimbali kama ambavyo tumekuwa tunasema katika vikao mbalimbali na nisingependa kulizungumza kwa undani sana, lakini niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya ambayo wamekabidhiwa na mamlaka mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba na mimi nichangie kwa kifupi sana. La kwanza Mwenyekiti aliyewasilisha maoni ya Kamati amesema na wengine wakasema Kituo hiki kipo Afrika ya Kusini, lakini Afrika ya Kusini yenyewe na kama walivyohoji hajaridhia kuanzishwa kwa Mkataba huo. Sasa mimi nilitaka pengine Mheshimiwa Waziri atusaidie kwamba pengine kwa nini Afrika ya Kusini haijaridhia kuanzishwa kwa Mkataba huu na hasa wao wakijua kwamba Makao Makuu ya Kituo hiki yako nchini mwao. Pengine Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa nini sisi tukiridhia Mkataba huu maana yake tunakuwa nchi ya tano kama sijakosea kwamba Mabunge yote ya nchi za Afrika ndipo sasa yanapotaka kuridhia Mkataba huu au nini. Kwa sababu inawezekana kasi ya kuridhia Mkataba wenyewe ikawa ndogo sana na pengine tusianze kulifanyia kazi mapema inavyowezekana. Pengine na hili ni vizuri Mheshimiwa Waziri angetusaidia.

Kitu kingine ambacho ningependa kukizungumzia ni pale tunaposema kemikali za sumu na za kawaida. Ninataka niseme hivi wananchi wetu wa kawaida wanajua haya. Inawezekana tukawa tunasema haya kwa manufaa yetu sisi wenyewe. Tumechukua jitihada gani za kuwaelimisha wananchi ambao ndiyo walengwa hasa juu ya suala hili. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri tunapozungumzia suala la kusimamia taka za sumu pamoja na zile za kawaida tuweke na mikakati ya dhati kabisa ya kuwaelimisha wananchi wetu tunaposema taka za sumu ambazo zinaweza zikawa na athari kwa maisha ya binadamu wa kawaida ni zipi ili waelewe. Kwa sababu nina hakika tunaweza tukawa tunahusika na bidhaa nyingine au vitu vingine ambavyo ni taka na zenye sumu kali, lakini wenyewe tusijue kwamba hizi zina sumu. Kwa maana hiyo, pengine tukawa

hatujafanya ya kutosha sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri wakati tunazungumzia kuridhiwa kwa Mkataba huu basi tuweka na mikakati pia ya kuwahi kutoa elimu kwa ajili ya wananchi wetu ambao kwa kweli wao pia ni wahusika sana katika suala hili nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala lingine kwamba wenzangu wamezungumzia suala la utaalam kwamba tuweke mikakati pia ya kufundisha wataalam na kwa kweli moja ya majukumu ya Kituo hiki ni kutoa mafunzo. Sasa kwetu sisi wenyewe tunajiandaa namna gani. Amezungumza hapa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, nimemsikiliza. Lakini na mimi nilikuwa nimeshalifikiria kwamba nilizungumze. Lakini kwamba tukitoa haya mafunzo basi kama alivyosema yatuwezeshe au yawezeshe wataalam wetu waweze kutambua hizo kemikali pengine za sumu, kwa maana hiyo kuweza kutahadharisha au kutoa elimu kwa wananchi wetu. Mimi nimewahi kusikia wataalam wapo humu ndani na huko nje wanasema kwa mfano hizi simu za mkononi tunazotumia na zenyewe zina sumu kali sana na zinapokuwa zimeharibika zikatupwa. Sasa zinapotupwa zile kemikali zake zinakuwa na athari kubwa sana kwa wananchi wetu. Sasa tuna mikakati gani kwa mfano, kuwafundisha wananchi wetu wakajifunza hilo na kweli wakatupa basi au wakatahadharishwa kwamba simu hizi kwa mfano zinapoharibika ziharibiwe namna gani na siyo kutupwa ovyo ovyo kama sasa hivi inavyotokea na kwa kweli sina uhakika kama tumekwishawatahadharisha hata wananchi wetu juu ya matumizi ya simu hizi zinapokuwa zimeharibika uhifadhi wake unakuwa namna gani.Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri inawezekana sumu nyingine tusizione moja kwa moja, lakini zikawa kwenye vyombo tunavyovitumia. Tunajiridhisha namna gani na zinapokuwa zimefikia mwisho wake tunazitunza namna gani. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri na hili pengine tuliangalie. Lakini pia nchi yetu na nchi nyingine za Afrika, nashukuru kwamba Kituo hiki kinaanzishwa tukiridhie pengine kinaweza kikatusaidia. Nchi nyingi za dunia ya tatu na pengine siyo Tanzania peke yake zimechukuliwa au zimekuwa kama sehemu ya kutupa hata baadhi hizi tunasema *cheap commodities*. Wenzetu kule Ulaya pengine au Marekani inawezekana hawazihitaji, lakini kwa sababu wanatuona sisi pengine kwa umaskini wetu tunafikiri ndizo zinazotufaa. Kwa hiyo, tunazikimbilia tunazinunua lakini kimsingi zinakuwa na madhara makubwa sana kwa wananchi wetu.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kuridhiwa kwa Mkataba huu kwanza kunaweza kukasababisha au ukawezesha nchi za Afrika zikawa na msimamo wa pamoja wa kukabiliana na haya ambayo yanafanywa katika nchi za wenzetu zilizoendelea za kuweka nchi zetu za Afrika kuwa ndipo dampo la bidhaa zile ambazo kwanza ni bidhaa rahisi na hizo ambazo zinaweza zikawa na sumu kwa ajili ya wananchi wetu. Lakini pia nilitaka nizungumzie suala la hizi takataka za kawaida. Sasa hivi tunanunua magari mengi makuu kuu kutoka nchi za wenzetu ambao wana viwanda vya kutengeneza magari. Lakini hata sehemu nyingine ambazo hazitengenezi magari lakini zinatumiwa kupitisha magari, lakini sisi tunaenda kuyanunua magari huko. Nchi nyingi za Afrika na zinazoendelea na sisi hapa Tanzania ni mashahidi magari makuu kuu yanayoingia ni mengi sana. Ukienda Dar es Salaam, ukienda katika Mikoa mingine, ukienda kwenye gereji utakuta magari mabovu unaweza ukafikiri zimepelekwa gari kutengenezwa lakini

ni mbovu zote na wala hazitegemewi zinaweza zikatengenezwa siku moja zitembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaingiza magari yanakuja hapa yanatembea wiki moja na ikizidi sana mwaka mmoja gari liko juu ya mawe. Sidhani kama hili litatusaidia sana wakati tunaridhia Mkataba huu iwapo hatutakuwa na mkakati kwamba ni magari ya namna gani tuyaingize katika nchi yetu. Ni kweli magari ni chombo muhimu cha usafiri, siyo chombo cha anasa, lakini ni magari ya namna gani tunayoyaingiza. Inawezekana sasa kama nilivyosema mwanzo wenzetu wanatumia nchi zetu kama sehemu ya kutupa mali ambazo kwao wanafikiri sasa hazina maana wacha tuwapelekee Watanzania huko, wacha tuwapelekee Waafrika huko wao wanaweza wakazitumia. *(Makofi)*

Lakini wenyewe tusijue kwamba wenzetu wanajua kwamba huko ndiko zinakokwenda kwisha. Kwa sababu wenzetu wametumia gari miaka mitano lipelekeni huko Afrika. Baada ya miaka mingine mitano hili gari limekwisha na namna ya kuzitunza hizi takataka ambayo magari yanayogeuka kuwa takataka hakuna pia njia nzuri ya kuyatunza na ndiyo haya sasa yanayotokea wakati watu wanakusanya wengine hizi nyingi zinazokuwa takataka nyingine zinabainika kuwa pengine mabomu inawezekana mabomu haya yalitoka huko au namna gani. Ilikuwa ni vizuri tukawa waangalifu lakini tukawa na mkakati wa kuingiza bidhaa ambazo tunafikiri sio za kuja kutengeneza takataka lakini ni bidhaa ambazo zinaweza zikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa sitaki kuzungumza mambo mengi, lakini nilitaka tu nimalize kwa kusema kwamba nashukuru ile taasisi inayoshughulika na udhibiti wa dawa pamoja na chakula kwamba wanapiga vita sana baadhi ya vipodozi ambavyo vinaingia katika nchi hii. Hivi vingi pia vinaweza vikawa vina sumu na kemikali ambazo hatari sana kwa afya za wananchi wetu. Nilitaka niseme pia kwamba tudhibiti uingizaji wa vipodozi pamoja na dawa ambazo zinaweza zikawa na athari kwa afya za wananchi wetu wakati tunakwenda kuridhia mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimemsikia Mwenyekiti wetu wa Baraza la Taifa linaloshughulikia na Mazingira *(NEMC),* Mama Cynthia Hilda Ngoye akizungumza kwamba Baraza hili ambalo wote tunajua umuhimu wake hata sasa hivi wakati tunazungumzia suala la hifadhi ya mazingira kwamba linapewa fedha ndogo sana. Sasa kama Baraza linapewa fedha ndogo sana tunategemea lifanye kazi kubwa hasa katika kipindi hiki ambacho tutakwenda kuuridhia mkataba. Baraza inawezekana lisiwe na nguvu, kwanza nguvu za kifedha halina uwezo wa fedha lakini pia hata uwezo wa kuzalisha wataalamu inawezekana lisiwe nao.

Mheshimiwa Mwenyekiit, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ni vizuri kwanza tukalipa Baraza uwezo wa kifedha ili liwe na uwezo pia wa kuzalisha hata wataalamu ambao wanaweza kukabiliana na haya mambo ambayo tunayazungumza sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo ninaomba na mimi niseme kwamba naunga mkono Mkataba huu wa kuridhia kuundwa kwa kituo kwa ajili ya kusimamia taka za sumu na zile za kawaida. Nashukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa familia ya Marehemu Juma Akukweti na kwamba wawe na moyo wa subira na Mwenyezi Mungu ailaze roho yake peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Wabunge wote waliochaguliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi yetu na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania tayari imeridhia mkataba wa Basel kuhusu udhibiti wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na ule unazuia uingizaji wa taka za sumu Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu itanufaika na misaada itakayotolewa kuhusiana na kemikali na taka za sumu kutoka kwa wafadhili wa Kimataifa pamoja na mitambo ya kuteketeza taka hizo. Pamoja na mafunzo tutakayoyapata ya ukusanyaji na usimamizi kabla ya kuleta madhara kwa viumbe na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bahati kwa sababu kuna uharibifu mkubwa unaofanywa na meli za nje na wanapofanya vitendo hufanya kwa siri bila kufahamika. Lakini kwa kuridhia mkataba huu tunaweza kupata vyombo vya kulinda bahari zetu ambako ndiko kwenye uchafuzi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, tuungane na wenzetu waliokubali kuridhia mkataba huu.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono kwa hoja hii ya taka za sumu, ni taka ambazo siyo watu wengi wanazifahamu. Hizi ni taka mabazo haziozi kwa urahisi. Hata pale ambapo zinaoza huwa zinatoa sumu katika kuoza kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki cha Afrika ambacho tayari kimeanzishwa huko Pretoria, Afrika Kusini ni kitu muhimu sana. Meli za aina mbalimbali ambazo zinatembelea Pwani zetu, huchafua sana bahari zetu kwa kutupa taka lakini, meli mbaya sana ni zile meli ambazo hubeba taka za sumu na kutafuta mahali pa kutupa taka hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zetu ambazo zinasimamia mazingira lazima ziwe macho kwa kufanya ukaguzi wa baharini wa mara kwa mara. Ili kuweza kusaidia

kituo kikubwa cha Pretoria, basi kuanzishwe vituo vingine vidogo vidogo kama vile Maputo, Dar es Salaam na Mombasa. Lakini pamoja na kutumia kituo hiki cha Pretoria, lazima tutazame hali yetu sisi wenyewe humu ndani nchini. Taka zinazozalishwa humu ndani ni nyingi na ni za namna mbali mbali pamoja na taka za sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi hatutaweza kudhibiti taka zetu wenyewe humu nchini basi kujiunga kwetu kwenye kituo hiki ni bure. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwamko thabiti kuhusu mazingira. Kwa kuwa swala la mazingira ni mtambuka, naomba Wizara na Idara zote za Serikali ziiunge mkono Wizara ya Mazingira katika kampeni ya mazingira na kuifanya nchi yetu mahali salama na pia kutuepusha na jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza juhudi za Wizara ya kupata Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa kituo hicho toka Tanzania. Naomba *awareness* hii iendelee kwa wananchi wengine ili Tanzania ipate watumishi wengi zaidi katika kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea sana taka za sumu toka nchi za nje tunasahau sumu inayoweza kutengenezwa na madampo yetu. Madampo yanaweza kuwa viwanda vya kutengeneza sumu ambayo inaweza kuathiri wananchi bila kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kituo kitakapoanza kazi, kifikirie pia *proper management* ya madampo katika miji ya nchi wanachama. Hivyo naomba na napendekeza kuwa Baraza la Taifa la Mazingira lianzishe uhusiano wa karibu sana na kituo hiki ili lifaidike na taaluma itayolisaidia Baraza kutawala mazingira vizuri hapa nchini kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa maelezo yako ambayo kwa kiasi kikubwa yameeleweka. Nilikuwa napenda kufahamu:-

(i) Inasemekana na imekubalika kuwa *Headquarter* ya *Africa Institute* yatakuwa Afrika ya Kusini, je, ni *on rotational basis* na je, ni kwa muda gani? *(Article IV).*

*Article (V)* inazungumzia kuwa *Members* watakao *default* kwenye *contributions,* watawajibika kwa *sanctions* za Baraza hilo. Sasa kutokana na uzoefu wa nchi yetu kuchelewa kulipa *contributions* zetu kwenye *Organizations*/Vituo/Jumuiya mbalimbali, je, hizo *sanctions* zimeeleweka ili tujue endapo itatokea *default* tusiadhirike sana au tuombe kipengele hicho kiondolewe ila nchi ziombwe kuwajibika *to their commitments rather than* kuweka *legal measures.*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo hivi sasa, kuna usalama mdogo sana juu ya utupaji taka za sumu na taka nyinginezo nchini mwetu. Wakati utaratibu wa kuridhia mkataba huo unaandaliwa, nashauri yafuatayo:-

(a) Mpango ufanyike kuchunguza kama Dampo la Tabata ambapo sasa ni makazi ya watu halileti madhara kwa wananchi wanaoishi hapo.

(b) Wizara ya Afya ina utaratibu wa kutokomeza dawa zisizohitajika, je, njia zinazotumika kutokomeza dawa hizo, hazina madhara kwa binadamu na kwenye mazingira?

(c) Kuna imani kwamba mbolea ya chumvi chumvi huharibu rutuba ya ardhi. Kwa mfano, Mkoani Ruvuma inasadikika kwamba hakuna zao linaloweza kukua na kukomaa kama mbolea haijawekwa. Je, ni kweli?

(d) Yale mabaki ya udongo baada ya kuchekecha madini (dhahabu, almasi na kadhalika) kwenye machimbo mbali mbali hapa nchini Chunya ikiwemo. Je, hayana madhara kwa binadamu na viumbe vingine hasa kutokana na dawa aina ya *Mercury* inayotumika kusafishia madini hayo?

(e) Kuna tabia ya baadhi ya makampuni hasa ya ujenzi wa barabara kubakiza vyombo chakavu kwenye maeneo ya kazi bila kuondolewa. Je, vyombo hivyo chakavu havina madhara? Kwa nini isiamuliwe vyombo vya aina hiyo kuondolewa baada ya kazi kumalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio kwa kuwa Taasisi inayoundiwa mkataba itakuwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza wewe kwa leo kuweza kuwa na bahati ya kuendesha Bunge hili badala ya Mheshimiwa Spika na Naibu Spika. Pia sina budi kupongeza Wizara hii ya Mazingira chini ya Waziri pamoja na watendaji wote katika Wizara kwa kazi nzuri na utekelezaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taka za sumu na nyinginezo zinapatikana mahali pengi hasa kwenye bahari kuu. Kutokana na meli za kigeni na vyombo vya bahari nyingine husababisha kuharibu mazingira. Kwa hiyo, naomba kuwe na elimu maalum na kuwafahamisha kwa kutumia utaalam wowote hata kwenye vyombo vya habari na vipeperushi ili ujumbe ufike na ifahamike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taka za sumu na nyinginezo huwa ni chafu lakini uchafu wowote huhifadhiwa na taka nyingine za sumu. Lakini kwa vitu vingine huwa zina faida, nyingine huwa mbolea kwa mara nyingine kwa hiyo bado kuwe na utaratibu maalum na kama wataalam tulionao watumike katika kazi zao. Tuone taka zote zinahifadhiwa na zile ambazo zitatumika zitumike na zile ambazo huleta athari basi zihifadhiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono Azimio hili liliridhiwe.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali natoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Juma Akukweti na pia nawapongeza wote waliopata nyadhifa za Kimataifa na Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani inazalisha taka nyingi zenye sumu, tofauti iliyopo ni kuwa Tanzania haina teknolojia ya kukusanya taka hizi. Matokeo yake taka hizo zimekuwa zikiathiri sana afya za wananchi ikiwa ni pamoja na *Cancer, TB* na maradhi mengine mengi, ikiwa ni pamoja na vifo/ulemavu wa kudumu na kutokana na umaskini wa nchi nyingi za Afrika, imekuwa jambo la kawaida kwa nchi tajiri kutupa taka zenye sumu kwa nchi maskini mfano Ufaransa ilivyomwaga taka zenye sumu katika Bandari ya Ivory Coast. Madhara yake ni makubwa sana na mbaya zaidi athari nyingine zinachukua muda mrefu. Uamuzi wa kuridhia mkataba huu ni muhimu sana kwani si tu utasaidia usimamizi wa mazingira bali pia afya za wananchi zitaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala mtambuka na hivyo kutokuridhia mkataba huu maana yake ni kukataa kuwa mazingira si uhai. Ni mazingira yetu yatakayotufanya tuishi salama au tufe. Kituo hiki pamoja na mambo mengine kitahusika na utafiti. Utafiti huu utahusu sana masuala ya mazingira ya kuona ni vipi nchi nyingine zinavyodhibiti taka zenye sumu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira ni uhai na kwa kuwa wote tunapenda kuishi na kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo, basi ni vyema tukawa na kituo hiki ili kweli mazingira yetu yaboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya Tanzania hatuna vifaa vya kisasa vya kugundua meli zinazomwaga taka za sumu. Basi, ni wakati sasa umefika kwa Serikali kuwa na vifaa vya kisasa ili tuweze kuona meli hizo zinapofanya uhalifu huo. Madhara ya sumu hizo kwa viumbe wa baharini ni mbaya sana lakini pia kutokana na *eco system* samaki hao huvuliwa kwa matumizi ya binadamu hali ambayo inaweza kuleta madhara kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa ya Serikali kuwa na utaratibu maalum wa kutekeleza taka. Kuna taka nyingi za sumu zinaachwa zinazagaa. Mfano mwaka juzi kuna kichaa mmoja alilipuliwa na kopo lililokuwa limetupwa hivyo katika kuchambua taka kopo lile lililipuka na alifariki. Je ni wangapi wamedhurika kwa taka za sumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja kwa kuwa litatusaidia katika kuboresha mazingira yetu kwani mazingira ni uhai na taka za sumu zina athari kubwa kwa mazingira.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambao waliomba kuchangia upitishaji wa Azimio hili, sasa tunaendelea na hatua inayofuata ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hoja hii kwa kutoa majibu ya hoja mbalimbali zilizoletwa na Wabunge halafu baadaye tuendelee na kupitisha Azimio letu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoingia katika ukumbi wako huu wa Bunge lako Tukufu jioni hii tulikuwa wachache na tumeshajipangia kwamba baada ya dakika 15 tutakuwa tumemaliza masuala yote yanayohusu Azimio hili. Kwa hiyo, imekuwa ni furaha kwetu yaani mimi na wenzangu wanaonisaidia katika usimamizi wa jambo hili kwamba tumefaidika na michango mizuri sana ya Waheshimiwa Wabunge. Niseme kwa ujumla tu kwamba kama ilivyo kawaida sisi tunachukua michango yote hii kama njia ya kutusaidia ili tuwe watendaji kazi bora na vile vile itatusaidia sana katika kuwasilisha mawazo ya nchi katika vikao vinavyohusika na taasisi kama hizi ambazo ni za Kimataifa pindi tutakaporidhia baada ya Bunge lako Tukufu kukubali azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza katika Bunge lako Tukufu ni saba ni pamoja na mwakilishi wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anastazia Wambura na vile vile Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani. Wengine ni pamoja na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, ambaye alisahau kuelezea maslahi yake katika suala hili, lakini ukamsaidia kumkumbusha kwamba yeye ni Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi na Hifadhi wa Mazingira Nchini *(NEMC)*. Mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Raynald Mrope, nimemfahamu kwa kazi nyingi za kuchangia katika nchi yetu sikujua vile vile ana fani ya uvuvi, ndiko alikoanzia kazi. Niseme tumetoka mbali lakini sikujua kama Masasi nako bahari imefika, lakini ni karibu sana na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine ni Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge mwenzangu toka Mbeya, ni Mbunge wa Mbozi Mashariki. Nilidhani sitapata michango ya maandishi, lakini michango imekuja na Waheshimiwa saba wamechangia kwa maandishi nao si wengine isipokuwa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. Nawashukuru sana wote kwa michango yote ambayo mmeitoa. *(Makofi)*

Sasa niende haraka haraka kwa kuchangia au kwa kutoa maelezo na ufafanuzi katika maeneo mbalimbali ambayo tumechangia au kwa kutoa maelezo au maamuzi katika maeneo mbalimbali ambayo yamegusiwa na wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa lile ambalo tumeulizwa kwanza na Mheshimiwa Anastazia Wambura akiiwakilisha Kamati ya Maliasili na Mazingira. Hili limeulizwa vile vile na wachangiaji wengi kwa hiyo nitalijibu hapa hapa. Ilikuwa kuwaje kituo hiki kikawa Afrika Kusini na vile vile imekuwaje kwamba wenyeji wa kituo, Afrika

Kusini hawajaridhia Mkataba huu? Maana yake ni kwamba mbona tuna haraka sisi kuridhia. Kituo hiki kiliombwa na Afrika Kusini yenyewe katika Mkutano ambao Mawaziri wa Nishati walikutana. Tukasema kwamba katika nchi zinazozungumza lugha ya Kiingereza wao si kwamba wana uwezo tu lakini vile vile tayari walikuwa na nafasi katika Chuo Kikuu cha Vista pale Pretoria ambacho kilikuwa kinaendeleza fani ya namna hii hii. Kwa hiyo, wangeweza kukikaribisha kituo hiki kwa muda kiwe pale wakati shughuli za kuanzisha kituo rasmi zikianza. Kwa hiyo, Mawaziri walikubali na kituo kikaanzishwa pale na kituo hiki kama nilivyosema kiko katika Chuo Kikuu cha Vista pale Afrika Kusini. Lakini mategemeo ni kwamba baada ya kuridhiwa na nchi ya tano na nchi yenyewe bila shaka itakuwa Tanzania basi kitaandikishwa kitapewa *legal status,* kitapewa hadhi ya kisheria ya kuwa taasisi kamili chini ya taratibu na Sheria za Afrika Kusini lakini kitaanzishwa kama kituo cha Kimataifa yaani *Inter Governmental Organization.*

Vituo vingine vile viwili cha Senegal chenyewe kimeanzishwa chini ya Wizara ya Mazingira ya Senegal ni Kituo cha Kitaifa lakini kinahudumia Mataifa mengine. Lakini kile cha Misri kimeanzishwa chini ya Chuo Kikuu cha Cairo kwa hiyo, ni kituo cha Kitaifa lakini kinahudumia nchi za Kiarabu. Kwa hiyo, hiki cha Afrika Kusini ndicho kitakuwa na hadhi ya Kimataifa. Kwa hiyo, huo ni uamuzi ambao umefanyika na sisi tunadhani ni uamuzi mzuri hautaleta matatizo katika utekelezaji. *(Makofi)*

Kuhusu Afrika Kusini ina mchakato gani kuridhia Mkataba huu? Ni kweli tulitegemea kwamba Afrika Kusini ingekuwa ya kwanza, lakini kila nchi ina taratibu zake. Wale ambao wanafanya mambo haya haraka haraka ni nchi zile ambazo Rais anaweza kuwa na mamlaka tu ya kuamua na amepewa mamlaka ya Kikatiba na kuamua kwamba anaridhia. Wengine ni *Cabinet* yenyewe inaridhia. Hapa ndipo hapo sisi tulikuwa kabla ya Bunge kuridhia Mikataba kwa niaba ya wananchi. Sasa katika nchi nyingine zinakuwa na mlolongo mrefu na Afrika Kusini ina taratibu nzuri sana za kuwahusisha wananchi wake katika shughuli zote hizi. Kwa hiyo, ina utaratibu mrefu lakini unawahusisha wananchi katika maamuzi haya hatimaye yanaenda Bungeni. Kwa hiyo, mambo ya *Public Hearing* katika mfumo wa Afrika Kusini yana uzito mkubwa sana na ndiyo maana yamechelewa lakini ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Afrika Kusini nayo iko katika mchakato kama wa kwetu na muda si mrefu itaridhia Mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Anastazia Wambura na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia wamesisitiza umuhimu wa sisi kujipanga kama nchi kujitayarisha katika kupokea hicho kituo kwa maana ya kwamba tusipokuwa na wataalamu tusipojua tunafanya nini, tusipojua tuna kemikali za aina gani zipo wapi, zina madhara gani hata kituo kiwe na wataalamu namna gani hatutafaidika. Kwa hiyo, kwa kweli hilo tunalichukua. Niseme tu kwamba katika suala hili tunashirikiana na wenzetu Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na taasisi mbalimbali na Vyuo Vikuu, taasisi zenyewe ni kama vile Taasisi ya Utafiti katika *Pesticides (TPRI)* ambayo iko Arusha na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Niseme hii Maabara imetambulika katika Kanda ya *SADC* kwamba ni Maabara ya Kitaalamu ambayo inaweza kutumika na nchi za *SADC* katika masuala haya ya kujua kemikali na aina ya sumu

mbalimbali. Kwa hiyo tayari taaluma imeanza kujijenga nchini. Tunayo. Nadhani tutazidi kuijenga na kuratibu ili tujitayarishe barabara kukipokea kituo hiki.

Suala la udhibiti wa meli zenye sumu limeelezwa na wenzetu wengi, kwa kweli ni suala muhimu sana. Niseme tu kwamba Mamlaka wa Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* imeandaa *Marine Contingency Plan* yaani tufanye nini inapotokea dharura katika uchukuzi wa majini hasa katika masuala kama vile umwagikaji wa sumu, utupaji wa sumu na vile vile mambo kama vile petroli ikimwagwa katika bandari zetu. *NEMC,* shirika letu au taasisi yetu hii imeshirikiana na *SUMATRA* na taasisi nyingine kuandaa mpango huo na kwa kweli ni mpango wa Kitaifa ambao unahusisha miundombinu kwa ujumla wake kwa maana Wizara ya Miundombinu, Ulinzi yaani Jeshi letu la Wananchi, Usalama wa Raia, Polisi na Maliasili na vile vile Mazingira na TAMISEMI kwa maana ya kwamba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika maeneo yanayozunguka, maeneo ambayo sumu hizi zinaweza zikamwagwa au athari hizi zinaweza zikatokea. Kwa hiyo, tumejitayarisha kwa namna hiyo lakini kila wakati kuna kitu tunachoweza kuboresha na tutachukua ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwamba tujipange na tujitayarishe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na taratibu za mazingira na kanuni zieleweke, hili suala limezungumziwa, limetiliwa msisitizo na Wabunge wengi. Niseme tu kwamba kuna sheria tatu ambazo sasa hivi zinatusaidia katika kudhibiti taka za sumu nchini moja ni sheria ya kuhifadhi mimea yaani *Plant Protection Act* ya mwaka 1997 na kanuni zake. Hii inasimamiwa na Wizara ya Kilimo. Nyingine ni Sheria ya Usimamizi wa Kemikali Viwandani na Majumbani yaani *The Industrial and Consumer Chemicals Act* ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004. Sheria ya tatu ni sheria mama ya mazingira ambayo ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sheria namba 20 ya mwaka 2004.

Msemaji wa Upinzani alizungumzia mengi yanayofanana na yale aliyozungumza Msemaji wa Kamati. Isipokuwa niseme tu hili la mto ulio katika eneo la Geita. *NEMC* taarifa nilizonazo ni kwamba mwaka 1997/1998 baada ya kupata taarifa kama hizi za uchafuzi wa mto kutokana na shughuli za Mgodi wa Geita ilifanya uchunguzi wa zebaki katika Mto Mabubi. Matokeo yake yalionyesha kwamba viwango vya zebaki vilikuwa chini sana. Vilikuwa kidogo kiasi cha kwamba hapakuonekana madhara yoyote. Lakini tunachukua angalizo kwamba tusifanye mara moja katika miaka kumi. Kwa hiyo, bado nitawataka *NEMC* maadamu wao wenyewe wamenipa taarifa kwamba walikwenda huko miaka kumi iliyopita waende tena miaka kumi baadaye waone hali ikoje. Kwa hiyo, tumepokea huo ushauri na tutatekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Khamis Seif amegusia kuhusu umuhimu wa taarifa wa taka za sumu au dawa ambazo baadaye zinabadilika kuwa sumu kutolewa kabla ya taka na sumu hizi hazijapelekwa kwenye nchi ambako zinatakiwa ziende ama kuharibiwa ama kwa matumizi ya aina nyingine. Suala hili linasimamiwa na Mkataba mwingine ambao sikuutaja katika hotuba yangu. Unaitwa Mkataba wa Rotterdam. Mkataba mzima huu wa Kimataifa unahusu umuhimu wa kile kinachoitwa *Prior Informed Consent* yaani huwezi ukapeleka taka za sumu au kemikali kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine mpaka ile nchi ambako zinakwenda kwanza inapata taarifa

na vile vile inakubali halafu inatoa kibali kwamba zije na taratibu za usafirishaji zinaeleweka.

Kwa hiyo, huo Mkataba wa Rotterdam ni muhimu sana na mkataba huu kwa kweli pamoja na Mkataba wa Basel mikakati hii haikufuatwa ndipo ilipotokea athari za mwaka jana mwezi Agosti, 2006 kwa matukio ya Abidjan ambapo taka za sumu takribani tani 5,000 zilipakuliwa kutoka kwenye meli na zikatupwa katika maeneo mbalimbali ya jiji la Abdijan. Sasa sisi hilo limetufundisha nini? Imetupa fundisho kwamba kama inatokea inaweza ikatokea Abdijani inaweza ikatoa Dar es Salaam, Tanga au Mtwara. Kwa hiyo, tuwe macho kwa kulinda bandari zetu lakini na katika kusimamia vilivyo bidhaa zinazoingia katika nchi yetu. Lakini pili imetuonyesha kwamba wenzetu katika nchi zinazoendelea hawana nia njema kwa sababu hizi taka zilitoka katika nchi zao. Sasa kuzileta Afrika na kuja kuzimwaga, kwanza ni dharau lakini kwa kweli ni kama ukoloni mamboleo. Hili ni suala ambalo tulikemee kwa nguvu zote lakini vile vile muhimu ni kujitayarisha sisi wenyewe kukabiliana nalo linapotokea.

Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye amenisaidia sana kueleza hii programu ya *Africa Stockpile Programme* ambayo inasimamiwa na *NEMC.* Ni mradi mkubwa ambao tunatarajia kupata takribani dola milioni 9 hivi kwa kipindi cha miaka mitatu au minne, fedha ambazo zitatoka kwa *Global Enviroment Facility (GEF)* kupitia Benki ya Dunia ili kuweza kutekeleza mradi wetu ule wa kuangalia tufanye nini na hizi tani 1,200 za madawa ambayo yameharibika. Lakini la muhimu zaidi ni kuhakikisha hatutakuwa na madawa ya namna hiyo ya kutupa kwa kiasi hicho ambayo tutaacha yaharibike. Maana yake inawezekana tulipata hizo dawa kama msaada lakini sasa inakuwa ni balaa. Lakini inawezekana vile vile tulinunua maana yake tulipoteza fedha za kigeni. Kwa hiyo, kwa hili zile dawa zote za sumu ambazo karibu zote zimeharibika hatuna njia ya kuziteketeza itabidi ziende nchi nyingine ya tatu. Kwa hiyo, tutafuata taratibu za mikataba hii na tutasaidiwa sana na kituo hiki ili tuweze kufanikisha zoezi hilo la kuteketeza hizi dawa ambazo zina athari sana kwa mazingira na afya ya binadamu. Tumepokea kilio cha *NEMC.* Tatizo ni kwamba *NEMC* ni ya kwetu, wakilia maana yake sisi wenyewe tumelia. Lakini hata hivyo kwa sababu rai imetolewa hapa Bungeni, tumeipokea na hasa kuhusu ufinyu wa fedha. Majukumu ni makubwa sana ambayo tumekipa hiki chombo. Tutafanya linalowezekana kutokana na uwezo wa Serikali kukiongezea uwezo hiki chombo. Mimi natoa ahadi kwamba katika hili kwa uwezo ambao nilionao nitalisimamia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Raynald Mrope, amezungumzia kuhusu tatizo kubwa la umwagaji wa sumu katika bahari na kupendekeza kwamba kuwe na *inspectorate* ya kukagua mara kwa mara bahari yetu. Kama nilivyosema tunajiweka pamoja na wenzetu wa Ulinzi, Usalama wa Raia, Maliasili, Miundombinu na sisi wenyewe Ofisi ya Makamu wa Rais, TAMISEMI ili tuwe na chombo ambacho kinaweza kuwa na jina ambalo sio *inspectorate* lakini chombo kinachodhibiti mambo haya pamoja na uvuvi haramu, utupaji taka za sumu, tunafanya nini ikitokea kwamba petroli au mafuta yanamwagwa katika bahari na shughuli za namna hiyo. Kwa hiyo, chombo cha namna hiyo ni muhimu na kweli kipo lakini sio kwa maana ya taasisi. Itabidi tuboreshe baada ya kupokea haya mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tuwaeleze Afrika Kusini kwamba ingefaa tuwe na vituo vidogo vidogo labda Cape Town, Maputo, Dar es Salaam nadhani amesahau na Mtwara vile vile. Tutalipokea hilo maadamu kituo kitakapoanza na sisi tukiwemo katika Baraza la kituo basi mapendekezo mengi haya tunaweza tukayaingiza. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, kituo hiki hakitafanya kazi chenyewe, kitafanya kazi kwa kushirikiana na nchi zetu. Kwa maana hiyo sisi wenyewe na vituo vyetu ndio vitakavyokuwa mtandao ambao utasimamiwa na kituo hiki. Kwa hiyo, kuliweka hili katika programu ya mpango wa kituo inawezekana na tutalizingatia tutakapoingia katika Baraza. *(Makofi)*

Amegusia vile vile suala la *DDT*. Nizungumze kwa kifupi tu hili suala ambalo wenzetu wa Wizara ya Afya wanalisimamia lakini sisi ndio tunaosimamia Mkataba wa Stockholm ambao unahusu kemikali zinazobakia katika mazingira kwa muda mrefu. Sasa *DDT* ni moja ya kemikali 12 ambazo zinadhibitiwa na Mkataba wa Stockholm ambao ni mkataba wa mwaka 2001. Madhumuni ya mkataba huo kwa kweli ni kulinda afya ya binadamu, viumbe, wanyama ikiwa pamoja na mifugo na mazingira. Mkataba huo wa Stockholm unatutaka sisi nchi tulioridhia kutumia *DDT's* kwa sababu au kwa ajili ya afya tu yaani *disease*s za *Vector control* kama vile kudhibiti mbu wanaoleta malaria. Lakini vinginevyo *DDT* haiwezi ikatumika.

Kwa hiyo, matumizi ya *DDT* katika kilimo hayaruhusiwi kabisa. Mwaka 1997 tulizuia matumizi ya *DDT* katika kilimo na kutokana na matumizi ya huko nyuma tulibakiwa na tani kama 170 za *DDT* ambazo ulikwisha muda wake. Kwa hiyo, kiasi hiki nacho tunakipeleka katika nchi nyingine zenye uwezo wa kuteketeza zenye mitambo maalum ambayo inadhibiti utoaji wa gesi zenye madhara kama vile *dioxins* na *furans* ambazo zinatokana na hii *DDT*. Lazima tujiweke katika *register* ya wale ambao tunataka kutumia *DDT* kwa kufuatana na Mkataba wa Stockholm. Lazima tuombe *exemption* ili tuorodheshwe katika *register* na tunapewa *exemptio*n ina masharti. Inabidi tuweke mkakati wa kudhibiti madhara wakati wa matumizi ya *DDT,* taratibu na sheria kwa ajili ya matumizi yaliyoruhusiwa tu na tuwe na mikakati ya kukuza njia mbadala ambazo zinatufanya tusiendelee kutumia *DDT* kama ambavyo tunafanya sasa kwa maana *treated nets,* vyandarua ambavyo tayari vina kemikali zinazoua mbu na kuendeleza usafi wa mazingira.

Sasa tutatumia *DDT* Tanzania katika maeneo yenye mlipuko mkubwa wa malaria, *epidemic areas, malaria areas* na tutahitaji kama tani tano kila mwaka kwa kipindi ambacho tutaangalia tunafanyaje ili tusiwe tunazitumia muda wote. Tutaongozwa na taratibu za *World Health Organization* na tutatumia *DDT* hasa ndani ya nyumba ili zisisambae katika mazingira. Matumizi haya yatakuwa katika Wilaya 25 ambazo zinaonyesha mlipuko mkubwa wa malaria. Lakini Wizara ya Afya inafanya utafiti mbalimbali ili kupata njia mbadala, badala ya kutumia *DDT*. Kwa hiyo, matumizi yake yataangaliwa sana na najua hili suala limezungumzwa sana na wanaharakati wa mazingira. Kwa maelezo hayo bila shaka watakubaliana na sisi kwamba maadamu dunia nzima tuliridhia hili tukaona tunaweza kuwa na hiyo *exemption* na matumizi *restricted* utaratibu mgumu nafikiri tutakuwa na usimamizi wa kutosha.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, nadhani mengine nimeshamjibu. Labda niseme tu kwamba amezungumzia suala muhimu na la msingi kabisa la kuheshimu maamuzi katika maeneo ambayo wataalamu wamepewa mamlaka ya kuamua lakini vile vile ushauri wa wataalamu katika mambo yetu ya maendeleo. Kweli nakubaliana naye kwamba tusipuuze taaluma na tusipuuze ushauri wa kitaalamu vinginevyo tutakwama. Msingi wa utawala bora ni kufuata taratibu na sheria. Ukifuata taratibu na sheria hutakosea. Vile vile maana yake ni kwamba hata wataalamu wetu lazima wafuate taratibu na sheria na kile wanachoshauri kiwe kile ambacho kweli wametumia uwezo wao na juhudi zao pamoja na elimu yao, wanasema hapa ndipo mwisho. Lakini angalizo vile vile ni kwamba wataalamu wetu wasitufikishe mahali ambapo nao wanayumba yaani kwamba atakuja mtaalamu mwingine anaiambia Serikali hapana na hana ushahidi kamili kwamba walichokushauri sivyo sasa ukianza kuwa na wasi wasi na taasisi yako ndiyo maana unaweza ukaachwa kando. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema ni kama pande mbili za sarafu, Serikali na sisi viongozi tuheshimu maamuzi ya wataalamu pale walipopewa mamlaka ya kuamua, tuheshimu ushauri wao. Lakini upande wa pili ni kwamba nao watalaamu wajijengee taaluma na watoe ushauri ambao tuseme *beyond the reproach* yaani kwamba hauwezi ukawa wa wasi wasi, wakisema Waziri tumekushauri, wanasema hapa ndio mwisho hapa ndio tumesimama. Hapo tunaweza kuiheshimu taasisi na vile vile Serikali itaziheshimu hizo taasisi na taasisi zitajiheshimu zenyewe. Kwa hiyo, nakubaliana na hoja ya msingi ya kuheshimu maamuzi ya wataalamu. Nadhani alikuwa na maana sio kuhusu taka za sumu tu katika vikao vyetu ametueleza kuhusu vile vile kuheshimu ushauri wa wataalamu katika masuala ya *environmental impact assessment.* Hilo tumelipokea lakini kwa maana ya msingi ule ambao nimeuweka nilioueleza. Elimu kwa ngazi zote kwa maana ya uongozi, sawa katika masuala ya mazingira, masuala ya *risk assessment.* Yote haya ni masuala ambayo tunayapokea.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, ameuliza kwa nini Afrika Kusini haijaridhia, nimetoa maelezo. Kasi ya kuridhia ni ndogo ni kweli lakini nadhani tumeshaanza kituo kila mtu anasema kitaanza, kitaanza, sisi Watanzania tukiwa wa tano tutaridhia halafu wengine wote watakuja. Naamini au tunakuwa na nguvu na sisi ya kuwashawishi wale ambao hawajaridhia. Tunajiandaaje nafikiri tunasema taasisi zipo nyingi *TPRI,* Mkemia Mkuu wa Serikali na Viwanda kama vile Kiwanda cha Saruji cha *Wazo Hill* ambacho kinatekeleza aina nyingi ya taka za sumu ambazo hazitoi moshi wenye sumu. Takataka nyingi tunaziteketeza pale. Kwa hiyo, kina uwezo huo. Zile ambazo hatuwezi kama nilivyosema tunazipeleka nje.

Amezungumza suala la msingi sana kuhusu Tanzania na nchi zinazoendelea kuwa dampo ya kemikali, vifaa, mashine ambazo zimekwisha muda wake katika nchi zilizoendelea lakini zinaletwa kwetu kama msaada. Lakini nyingine ni zile ambazo matumizi yake tunaona ni ya kawaida sana lakini zina sumu. Nimeeleza hapa taka za sumu ninazozielezea ni pamoja na zile za simu za mkononi hizi ni taka za *electronic*, zikishaisha muda wake ni sumu zile. Naomba msizifungue fungue halafu mkaanza kuwapa watoto wasichezeechezee. Kitu kingine ni kompyuta. Ni balaa. Sasa tumeanza kuangalia uwezekano wa kuwa na protokali au itifaki ya Kimataifa ya kutuwezesha tuone

jinsi gani ya kudhibiti utupaji au nchi zilizoendelea kuwa dampo ya kompyuta zilizokwisha muda wake kutoka nchi zilizoendelea. Wengi wetu hapa ikiwa pamoja na mimi Waheshimiwa Wabunge tumepata maombi au msaada. Tumeambiwa kuna kompyuta 2,000 ziko hapa hazijaisha muda wake ni *secondhand* njoo uzichukue au tunataka kutuma kama msaada kutoka London au Marekani. Mimi ushauri wangu zikataeni. Zinakuja kama dampo kabisa ni njia mojawapo ya kutupa taka za sumu zinatokana na kompyuta zilizokwisha kwenye nchi zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu mmoja aliponiambia anataka kunipa msaada wa kompyuta 200 zilizotumika nilisema samahani sana wananchi wa Rungwe Mashariki wanahitaji kompyuta mpya. Nitakuwa tayari kupokea sita mpya kuliko 200 ambazo zimetumika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari sana, ni taka za sumu hizi. Nafikiri hili vile vile itabidi tuwe na mwongozo wa Kitaifa. Lakini katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP)* hili tumeanza kulijadili kwa sababu ni suala la Kimataifa baadaye tutalileta kama suala la Kitaifa, tudhibiti namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kompyuta kila baada ya miezi sita kuna *model* mpya. Sasa kwa nini na sisi kama kuna maendeleo ya haraka namna hiyo kwa nini sisi tupate kompyuta za miaka mitatu, minne iliyopita ambazo baada ya muda mfupi tu hazina kazi. Tunaishia kuzipeleka Vingunguti au Mtoni au Pugu Kajiungeni kama dampo. Ni madhara makubwa kwa afya za binadamu. Hili nilitaka nilisisitize tu. Nadhani watachukia sana hawa ambao wanatupa msaada. Lakini wakati mwingine ni vizuri uwe na kiburi. Sio vizuri kukubali kila kitu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza, niseme tu kwamba sisi tumeyapokea yote. Mengi na yote yaliyokuwa yameandikwa yatakuwa katika *Hansard* tutayajibu kama ilivyo kawaida yetu kwa maandishi na vile vile tutayatekeleza kama ushauri katika shughuli zetu za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Waziri mtoa hoja amehitimisha hoja yake na ametoa hoja na imeungwa mkono na sasa basi kwa hatua ya mwisho nitawahoji Waheshimiwa Wabunge katika azimio ambalo liko mbele yetu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwahoji ili nijue wale wote wanaoafiki Azimio hili sasa liridhiwe na Bunge na wale ambao hawataafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo cha Usimamizi wa Taka za Sumu na Nyinginezo liliridhiwa na Bunge)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa mezani kwangu shughuli zilizopangwa kufanyika katika siku hii ya leo naona zote zimekamilika na sina shughuli nyingine yoyote hapa mezani. Lakini nichukue tu nafasi hii kuwapa pole naona katika *session* ya leo jioni tumepata shida sana ya kurudi Bungeni kwa sababu ya mvua sana iliyonyesha leo mchana. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu mvua tumeililia ili iweze kutusaidia katika mambo mengi, ila tu tuombe isiwe imeleta madhara mengine kwa sababu imenyesha sana leo hapa Dodoma.

Baada ya kuyasema hayo ninalo tangazo moja tu hapa mezani nalo linatoka kwa Mheshimiwa Anna Makinda, Naibu Spika na Mwenyekiti wa *TWPG,* ameniomba nitoe taarifa ya kikao. Anasema: “Mwenyekiti ninaomba uwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Uzinduzi wa Mpango Mkakati *(Strategic Plan)* ya *TWPG* kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati hii mara tu baada ya Kikao cha Bunge leo jioni tarehe 1 Februari, 2007 yaani mara baada ya kikao hiki. Kikao kicho kitafanyika ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili, jengo la Utawala, ninaomba sana Wajumbe hao wa Kamati hiyo ndogo ya maandalizi wahudhurie bila kukosa.” Kwa hiyo, hilo ni tangazo naomba ile Kamati, Mheshimiwa Susan Lyimo nakuona na wale wenzako wote usiache kuhudhuria kikao hicho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo sasa naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.02 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 02 Februari, 2007 saa tatu asubuhi)*